**29 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 29 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, aulize swali lake.

Na. 188

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Kijiji cha Koresa – Vunjo

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kijiji cha Koresa, Kata ya Vunjo?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini. Aidha, Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi viporo pamoja na ujenzi wa vituo vya afya vipya kwenye maeneo ya kimkakati ikiwemo Kituo cha Afya cha Koresa katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa wananchi wa Kijiji cha Koresa wanapata huduma za afya kwenye Kituo cha Afya cha Himo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza, Kituo hiki cha Koresa kimeahidiwa na Serikali muda mrefu. Kwa hiyo, naamini kwamba, kwa sasa katika bajeti ya mwaka huu unaokuja kitapata fedha. Je, unaweza ukatupa kauli ya kwamba kituo hiki lini kitapewa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni Kituo cha Afya kule Kirua Vunjo Mashariki. Kirua Vunjo Mashariki hakuna kituo cha afya na wananchi wa pale wanafuata huduma hiyo maeneo ya mbali sana; Himo au Kirua Vunjo Magharibi na wananchi hao walikuwa hawana kiwanja, lakini wamechanga na wamenunua kiwanja cha ekari tano. Sasa tunaomba Serikali ijipange na iniambie kama wako tayari sasa kujenga kituo cha afya kwenye Kata hii ya Kirua Vunjo Mashariki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba, Serikali inatambua, naye mwenyewe alishawasilisha maombi ya kujenga Kituo cha Afya cha Koresa na tayari tumeshakiingiza kwenye orodha ya vituo vya afya vya kimkakati. Nakuhakikishia tu kwamba, mara baada ya fedha kupatikana tutahakikisha tunazipeleka kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile kwa sababu, ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba kinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kituo hicho cha Afya Vunjo Mashariki kwenye kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshawaelekeza Wakurugenzi wetu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufanya *mapping* ya maeneo ya kata za kimkakati zenye idadi kubwa ya wananchi, umbali mkubwa kutoka kituo cha huduma cha jirani au eneo la kijiografia ambalo ni tata kwa ajili ya ujenzi wa vituo. Kwa hiyo, tutakwenda kufuatilia hicho kituo tuone kama kinakidhi vigezo ili kiweze kupata fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, wananchi wa Kata ya Kerenge, Kijiji cha Mayuyu, wanahemea huduma ya afya kwa umbali mrefu sana kutoka kwenye makazi yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza jengo la zahanati ambalo wananchi wameshajitolea na kufikia hatua ya kutandaza mkanda wa chini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Sekiboko, anafuatilia sana masuala ya afya katika Mkoa wake wa Tanga, pamoja na zahanati hiyo. Namhakikishia tu kwamba tayari tumeshaainisha hicho kituo,

tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kumalizia zahanati hiyo ili wananchi wapate huduma karibu zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Bunge lililopita tuliandika maeneo ya kujenga vituo vya afya, nami kwenye Jimbo langu la Bunda nimeandika Kituo cha Afya Mihingo. Je, ni lini sasa hizo fedha za Kituo cha Afya Mihingo zitatoka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, na nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. Tulipitisha hapa karatasi kwa ajili ya kuandika kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, orodha ile tunayo ofisini, inafanyiwa kazi, inafanyiwa makadirio ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeainisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere ni suala la muda tu, tutakwenda kukamilisha utekelezaji wa ujenzi wa kituo hicho, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ni lini Serikali itakamilisha miundombinu ya Kituo cha Afya Nakatunguru katika Wilaya ya Ukerewe ili kiweze kuwa na hadhi, kwa sababu mpaka sasa hivi hakina wodi ya wanawake, wodi ya watoto, wodi ya wazazi na miundombinu siyo rafiki sana? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna vituo vya afya ambavyo vina upungufu wa miundombinu hususani wodi za wanaume, wodi za wanawake na wodi za watoto. Tumeshaanza utaratibu wa ujenzi wa majengo ya awali kwa awamu ya kwanza na baadaye tutakwenda awamu ya pili kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo ambayo yanapungua. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo hicho tutakipa fedha zikipatikana kwa ajili ya kukamilisha majengo ambayo yanapungua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tarehe 18 Oktoba, 2023 Mheshimiwa Rais alifanya ziara Tabora. Katika ziara hiyo kwenye mkutano wa hadhara, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mchengerwa alitangaza kwamba, tayari fedha zimepatikana kwa ajili ya kujenga vituo 214 nchi nzima. Sikonge walikuja wataalam Mwezi wa 12 wakaainisha maeneo matatu; Kiloleli, Ipole na Usunga...

**MWENYEKITI:** Uliza kwa kifupi.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, ni lini vituo hivyo vitajengwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha afya ambacho ni cha kimkakati katika Jimbo la Sikonge ni miongoni mwa vituo 214 ambavyo vitaanza ujenzi wake mwaka huu wa fedha kupitia Benki ya Dunia. Kwa hiyo, nakuhakikishia kwamba, kipo kwenye orodha, na tupo katika hatua za mwisho za kuanza utekelezaji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, Kata ya Ilemba na Muze ni kata za kimkakati ambazo tumeleta mapendekezo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kujenga kituo cha afya. Je, ni lini mtaleta fedha hii kujenga vituo vya afya katika kata hizo? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hiyo ya Ilemba na kata nyingine ambazo amezitaja, nashukuru kwamba wameshaleta mapendekezo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na Menejimenti ya Halmashauri ya Sumbawanga Vijijini. Namhakikishia kwamba, tunaendelea kutafuta fedha na pia, tunakwenda kuona gharama stahili ambazo zinatakiwa ili tuweze kuanza utekelezaji kwa awamu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mtunda kwenye Jimbo la Kibiti ni moja ya kata za kimkakati kujengwa kituo cha afya kufuatia athari ya mafuriko iliyokuwa imeikumba kata hii. Je, ni nini mpango wa haraka wa Serikali wa kuweza kujenga kituo cha afya katika Kata ya Mtunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata hiyo ya Mtunda ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Kibiti ni kweli, ameshaleta orodha hiyo

kwenye lile jedwali ambalo tumeainisha kata za kimkakati, na Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo haya ambayo yamepata mafuriko, baada ya maji kuondoka tutakuwa na mkakati mahususi kabisa kwa ajili ya kuhakikisha tunarejesha huduma za kijamii katika hali ya kawaida, zikiwepo huduma za afya. Kwa hiyo, tutaweka kipaumbele katika eneo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nauliza leo kwa mara ya tisa kuhusu Kituo cha Afya Kabwe. Nataka kufahamu, kwa kuwa bajeti yako tayari tumeshamaliza, ni lini mtaenda kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kabwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza kwa mara ya tisa. Inaonesha ni namna gani yuko *serious* na Kituo cha Afya cha Kabwe. Namhakikishia tu kwamba, Serikali iko *serious* zaidi kuhakikisha wananchi wa Kata ya Kabwe wanapata huduma bora za afya na tayari tumeshaanza kuweka kwenye bajeti. Kwa hiyo, ni suala la muda tu, tutakwenda kutekeleza kukamilisha kituo kile, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kwenye swali linalofuata. Namwita Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 189

**Ujenzi wa Hospitali Mpya ya Wilaya ya Ulanga**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Hospitali mpya ya Wilaya ya Ulanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilianza kutoa huduma mwaka 1905 kama Kituo cha Afya na baadaye kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali. Aidha, hospitali hii ni miongoni mwa hospitali kongwe 50 ambazo Serikali ilizifanyia tathmini, kwa ajili ya ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 27.9 za ukarabati wa hospitali kongwe 31 zilizobaki ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Ulanga, ambayo imepokea shilingi milioni 900 ambapo ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali unaendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasham, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ikiwa Serikali imetoa shilingi milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Ulanga, wakati mimi mwakilishi wa wananchi nimesema hospitali ni kongwe na haikarabatiki na wao wameamua kunipa, sijui hayo maamuzi wanakuwa wameyatoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Waziri haoni umuhimu wa kwenda kwenda nami katika Jimbo la Ulanga kuangalia hospitali hii na kuona uhalisia wa kile ambacho mimi nakiongea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati na ujenzi wa Hospitali za Halmashauri unategemea hali ya hospitali ilivyo na pia ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Salim Hasham kwamba hospitali ile ni kongwe na ni ya muda mrefu, lakini tathmini ya wataalam inaonesha kwamba, kuna tija zaidi kama tutafanya ukarabati na ujenzi wa baadhi ya majengo katika eneo lile lile badala ya kwenda kuanza eneo lingine ambalo lingekuwa lina *cost implications* kubwa zaidi. Pia ingeongeza sana gharama za watumishi na vifaa tiba kwa sababu, tungekuwa na hospitali ya zamani pia na hospitali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, bado hatujachelewa. Tutakaa sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mbunge na wataalamu kule tushauriane, na kama kuna umuhimu wa kujenga hospitali nyingine, tutaangalia vigezo hivyo na kwenda na hatua inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kupitia kuona hospitali hiyo pamoja na huduma nyingine katika jimbo lake, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Wilaya ya Bunda, mwaka juzi, 2022, aliagiza hospitali nyingine ya halmashauri ijengwe katika Jimbo la Mwibara. Je, hospitali hiyo itajengwa lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

maelekezo ya viongozi wetu wa kitaifa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa shughuli zetu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kajege kwamba, tayari Serikali imeshaweka mpango na itaenda kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kujenga hospitali katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abood, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Manispaa ya Mkoa wa Morogoro inazidiwa na wagonjwa. Ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro ya Wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kwamba ifikapo Ijumaa, ndani ya wiki hii, atuletea taarifa tuone wamefikia hatua gani katika ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro, wamekwama eneo gani na gharama kiasi gani inahitajika, ili tukubaliane kwa pamoja na kuhakikisha kwamba, tunakwamua mkwamo huo na hospitali hiyo ikamilike kwa wakati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye swali lingine. Namwita sasa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita, aulize swali lake.

Na. 190

**Ujenzi wa Nyumba za Watumishi Katika Halmashauri Mpya Nchini**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa kipaumbele cha ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Halmashauri mpya ikiwemo *Geita DC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024, Serikali imetoa shilingi bilioni 48.66 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 201 za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13.85 zilitolewa kwa halmashauri mpya 31 zilizohamisha makao makuu kwenda kwenye maeneo yao ya utawala ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Geita iliyopokea shilingi milioni 390 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu za Wakuu wa Idara na moja ya Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetengewa shilingi bilioni 1.30 kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba 24 za Wakurugenzi wa halmashauri na shilingi bilioni 6.72 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 35 za Wakuu wa Idara. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya nyumba 97 za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara zilikuwa zimekamilika. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika Halmashauri ya Geita, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Mimi sikuuliza swali la kisera, nimeuliza swali la jimbo langu. Ukitaja shilingi bilioni 44, kwanza unanichongea kwa wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, kweli tumepokea fedha, shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi, lakini baadhi ya halmashauri tulizohamanazo, zile halmashauri 31 tulipewa shilingi milioni 150, wengine wameshaongeza shilingi milioni 300 mpaka shilingi milioni 350, unakuta nyumba za

Wakurugenzi zina mpaka *swimming pool,* zina mageti, zina *fence* na kila kitu; lakini halmashauri yangu ina shilingi milioni 150. Ni lini utaongeza pesa ili tuwe na uwiano na wale uliowapelekea shilingi milioni 330? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama kwa miaka mitano tutajenga nyumba tatu kwa hizi halmashauri ambazo tulizirudisha vijijini, Wakuu wa Idara wapo 18, *it means* kuna miaka 30 huko mbele ili watu wetu wawe ndani. Ni lini Serikali itakubaliana na mawazo tunayoyatoa humu Bungeni kwamba yapo mashirika ya Serikali kama *National House, Watumishi House* ziingie mkataba na hizi halmashauri, kwani tuna uwezo wa kulipa hata kidogo kidogo ili waweze kujenga kwa mara moja tuepukane na hili suala la kupewa nyumba tatu kwa miaka mitano? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetoa taarifa kwa upana kwa maana ya sura ya kitaifa ili wananchi wajue kazi kubwa inayofanywa na Serikali yao katika ujenzi wa miundombinu ya nyumba za watumishi, lakini pia katika majengo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua kuna baadhi ya halmashauri waliongezewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi au Wakuu wa Idara pale ambapo fedha haikutosha. Moja ya jukumu la Mkurugenzi ni kuwasilisha taarifa rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI akielezea hatua iliyofikiwa baada ya kuanza utekelezaji na fedha kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Geita awasilishe andiko linaloelezea hatua waliyofikia kwenye ujenzi na kiasi gani cha fedha kinahitajika ili Serikali iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia fursa za *Watumishi Housing* na *National Housing* kuingia mikataba na kukubaliana kujenga nyumba za Wakuu wa Idara na watumishi wengine ili waanze kulipa kwa awamu. Kwa hiyo, ni suala tu la wao kutekeleza, lakini Serikali ilishatoa maelekezo na kuna baadhi ya halmashauri ambazo tayari zilianza kutekeleza utaratibu huu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga nyumba za watumishi hasa kada ya ualimu na kada ya afya katika Jimbo la Lushoto? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu, Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mpango mkakati wa kujenga nyumba za watumishi hususan wa sekta ya afya na elimu katika shule na katika vituo vyetu na utekelezaji umeshaanza. Shule nyingi zimeendelea kujengewa nyumba za walimu na pia vituo vya afya, hospitali na zahanati zinaendelea kujengwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Jimbo lake la Lushoto tutahakikisha pia tunaendelea kutoa kipaumbele kuhakikisha kwamba nyumba hizo zinajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu baada ya kugawana na Halmashauri ya Mji wa Mbulu, wamehamia katika mji wa Dongobesh na wamekamilisha jengo la utawala. Sasa ni lini Serikali itawajengea Watumishi wa Halmashauri ya Mbulu nyumba za kuishi? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumkumbusha na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwamba waanze wao kupitia mapato ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba za watumishi wakati wakisubiri Serikali kwenda kuunga mkono na kukamilisha nyumba hizo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Nyang'hwale, lakini jengo lile ni zuri, kuna thamani nyingi iliyopo pale. Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kuweka uzio kwa ajili ya kulinda mali zote zilizo pale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio. Fedha hizo zinaweza zikatoka katika mapato ya ndani ya halmashauri, kwa hiyo, Mkurugenzi aanze kutekeleza hilo, lakini pia linaweza likatoka Serikali Kuu kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulize swali lake.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Kama hayupo, kwa niaba yake Mheshimiwa Yahya Mhata, kwa niaba ya Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, endelea.

Na. 191

**Hitaji la Walimu wa Sayansi Mtwara Mjini**

**MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza Walimu wa Masomo ya Sayansi kwa Shule za Sekondari Mtwara Mjini?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri walimu wa masomo mbalimbali wakiwemo wa masomo ya Sayansi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023, Serikali iliajiri walimu wa masomo ya Sayansi 8,425 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata walimu 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 wa masomo mbalimbali wakiwemo wa sayansi ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo Manispaa ya Mtwara Mikindani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Halmashauri hii ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kwa kweli ina changamoto kubwa sana. Mfano, hapa ninapozungumza

kuna baadhi ya shule ina mwalimu mmoja tu wa *chemistry*, kuna baadhi ya shule ina mwalimu mmoja tu wa *physics*...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba wakati umefika, katika huu mgao wa walimu, Halmashauri hii ya Mtwara Mikindani ikapewa kipaumbele zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nakwenda kwenye Halmashauri yangu ya Nanyumbu. Katika halmashauri hii, hali ndiyo mbaya zaidi ya huko. Hapa ninapozungumza, hata ufaulu wa wanafunzi ni mbaya. Mfano katika mitihani iliyopita kati ya wanafunzi 998 ni wanafunzi 19% tu ndiyo waliofaulu masomo ya sayansi. Je, Serikali haioni haja sasa kwa hii Mikoa ya Kusini ikapewa kipaumbele kupatiwa walimu wa sayansi ili vijana nao wapate haki ya kusoma masomo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu mkubwa wa walimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, mwaka huu Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000. Sasa katika mgao huo, Serikali itaweka jicho la kipekee katika jimbo hili kwa ajili ya kuhakikisha kwamba walimu hao wanaweza kupatikana ili kupunguza upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafahamu umuhimu wa kuwa na walimu na hasa walimu wa masomo ya sayansi na kwa sababu Serikali tayari inaajiri walimu 12,000, kwa hiyo, itaangalia jimbo lako

kwa jicho la pekee ili kuona kwamba walimu wanapatikana ili kupunguza ukali wa upungufu kwenye jimbo lako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Zipo halmashauri ambazo zina uwezo wa mapato na zina uwezo wa kuajiri walimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kugatua suala la ajira ya walimu liende kwenye halmashauri ambazo wanaweza wakaajiri na wakaweza kuwalipa walimu badala ya kusubiri mgao wa kitaifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na mambo mengine inasimamia suala la ugatuzi kwa maana ya *D by D* na inapenda sana kuona halmashauri zinaweza kuwa na uwezo na ubunifu wa kutengeneza mapato makubwa ya ndani na kuweza kujiendesha zenyewe. Kwa hiyo, mawazo ya Mheshimiwa Mbunge ni mawazo mazuri, tunayachukua sisi kama Serikali, tutayachakata na tunaamini kwamba yataweza kutekelezeka.

**MWENYEKITI:** Naomba maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Chikoyo, endelea.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Jina langu ni Kikoyo siyo Chikoyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza. Wilaya ya Muleba tumejenga zaidi ya shule 30 mpya, lakini walimu wamebaki wale wale. Serikali ina mpango gani mahususi kwa Wilaya ya Muleba kutupatia walimu wa ziada?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba kumekuwa na shule nyingi mpya ambazo zimejengwa ambazo zina uhitaji mkubwa wa walimu. Tayari Serikali imeanza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya msawazo wa walimu kutoka kwenye shule zile za zamani kuwahamishia kwenye shule hizi mpya. Pia Serikali inatumia njia ya kuajiri walimu ili kufidia upungufu katika maeneo ya shule hizi mpya na hata zile shule za zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itaendelea na mikakati hii ili kuhakikisha shule zote zinazojengwa zinaweza kupata walimu ili wanafunzi waweze kupata elimu iliyo bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa. Shule ya Sekondari Indoombo ina walimu watano tu. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha ili kukidhi uwiano unaokubalika kitaifa na kimataifa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umeshalijibu hilo hebu jibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu mwaka huu tuna ajira mpya za walimu, kwa hiyo, katika mgao ule tutaangalia

kipekee pia kwenye jimbo lake naye aweze kupata mgao wa walimu hao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeanza kupeleka maabara za kompyuta kwenye shule zetu za sekondari nchini: Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sasa wale walimu wanajengewa uwezo ili kompyuta hizi ziweze kufanya vizuri zaidi na wanafunzi waweze kupata uelewa wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba pamoja na ujenzi wa miundombinu na kupatikana kwa vifaa mbalimbali muhimu katika elimu, pia itawajengea uwezo walimu wake ambao wote wanatoa huduma kwa wanafunzi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa masomo ya sayansi katika Mkoa wa Rukwa hususan Shule ya Sekondari ya Mazwi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali katika mwaka huu wa fedha itaajiri walimu 12,000, kwa hiyo katika mgao wa walimu hawa Serikali itaweka jicho la kipaumbele na la kipekee kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo katika shule zilizopo katika Mkoa wa Rukwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Namwita Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, Mbunge wa Micheweni, sasa aulize swali lake.

Na. 192

**Ujenzi wa Nyumba za Askari wa Jeshi la Uhamiaji Micheweni**

**MHE. ABDI HIJA MKASHA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Nyumba za Askari wa Jeshi la Uhamiaji Wilaya ya Micheweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Baran.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imekamilisha taratibu za kufunga mikataba ili kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi sanjari na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Uhamiaji Wilaya Micheweni. Gharama ya utekelezaji wa mradi huu ni kiasi cha shilingi 2,695,937,724.80, ikijumuisha gharama za mkandarasi kiasi cha shilingi 2,549,937,724.80 na mshauri elekezi kiasi cha shilingi 146,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukamilisha taratibu za ununuzi, tayari Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi 1,250,000,000 ili kuanza utekelezaji wa mradi huu. Aidha, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri wa miradi ya maendeleo kwa wananchi wake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkasha, swali la nyongeza.

**MHE. ABDI HIJA MKASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza ambalo lina sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Naomba nitoe taarifa katika hili Bunge kama ndani ya Wilaya yetu ya Micheweni bahati nzuri Ofisi ya Uhamiaji tunayo lakini kubwa ni suala zima la makazi kwa wale askari wetu. Je, ni lini ujenzi huu utaanza?

(b) Je, Waziri yupo tayari kufuatana nami ili twende akajionee uhalisia wa hali ilivyo katika eneo lile? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ujenzi wa majengo haya ya makazi ya Askari wa Uhamiaji katika Wilaya ya Micheweni itaanza katika mwaka wa fedha 2023/2024 na tayari tumetenga shilingi 1,250,000,000 ili kazi ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu kuongozana na Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari kuongozana naye kwenda Micheweni baada ya Bunge la Bajeti, kwa hiyo, asiwe na wasiwasi. ahsante sana, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama shida iliyopo Micheweni Wilaya ya Rungwe pia ina tatizo kama hilo la wafanyakazi wa uhamiaji kutokuwa na makazi ya kudumu ya wafanyakazi wale. Ni lini Serikali itapeleka fedha ili kuwasaidia Askari wale na siyo tu wa Uhamiaji, hata Askari Polisi kwani nyumba zao zimechakaa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Askari wake wote wa Uhamiaji na Askari wote wanakaa makazi yaliyo bora. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jinsi fedha itakavyopatikana, tutatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba ya makazi kwa ajili ya askari wa Wilaya ya Rungwe, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam, swali la nyongeza

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchakavu wa nyumba za Polisi zilizopo Finya, Basra maeneo ya Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa nyumba hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nia ya dhati ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Askari wake wote; Askari wa Uhamiaji na Askari Polisi, wote wanakaa kwenye makazi ambayo ni bora. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jinsi fedha zinavyopatikana, tutatenga fedha awamu kwa awamu kuhakikisha Wilaya ya Wete pia inapata ukarabati wa nyumba za Askari wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kazi gani zimefanyika kwenye shilingi 1,250,000,000 ambazo Serikali imepeleka kwenye Wilaya ya Micheweni kama jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri linavyosema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu, pengine Mheshimiwa Mbunge hajasikia vizuri, ni kwamba katika mwaka wa fedha huu wa 2023/2024 baada ya kusaini mkataba huu sasa, itaanza kazi ya ujenzi wa nyumba za makazi za askari hawa wa Uhamiaji. Kwa hiyo, kiasi hicho kilichotengwa cha shilingi 1,250,000,000 kitaanza utekelezaji wake mara baada ya kusaini mkataba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu hili sasa naliuliza kwa mara ya tatu na Serikali inaahidi, lakini hakuna kinachofanyika. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba, wananchi wamefanya kila juhudi kuweza kujenga boma na limefikia kwenye *lintel,* lakini tayari kuna maboma sita pale kwa ajili ya Askari: Je, ni lini watakamilisha kazi hii ili kituo kile kianze kufanya kazi na tayari kuna nyumba sita ambazo zina Askari, lakini wanakwenda mbali na kituo hakijaanza kutumika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa kazi kubwa walioifanya ya ujenzi wa maboma kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ambayo wananchi walishaianza, Serikali inaunga mkono na nitapata fursa ya kukaa na Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hicho niweze kuzungumza naye kuona namna bora ya kumalizia maboma haya ambayo tayari wananchi wameshayajenga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu hatuna kabisa nyumba za Askari; Askari Polisi pamoja na Askari wa Uhamiaji. Je, ni lini Serikali itajenga nyumba hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Minza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba askari wetu wote wanakaa kwenye makazi bora. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia kwenye mwaka huu wa fedha, kama Mkoa wa Simiyu hauna kituo kabisa, basi tuangalie kwenye mwaka wa fedha unaokuja ili kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi pamoja na Uhamiaji. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda sasa Wizara ya Kilimo, nimwite Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, aulize swali lake.

Na. 193

**Mradi wa Umwagiliaji - Msufini Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji katika Kijiji cha Msufini Kata ya Hembeti Mvomero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji ya Msufini yenye jumla ya hekta 1,000 iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero inakabiliwa na changamoto ya banio kuachwa na mto ambao ndiyo chanzo chake kikuu cha maji sambamba na mchanga kujaa kwenye mto huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mradi wa Msufini ili kujua gharama halisi za utekelezaji wa mradi huu na miundombinu sahihi itakayohitajika ili kukabiliana na changamoto zilizopo sasa. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa skimu hii utanufaisha wakulima 320.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa tuna skimu za umwagiliaji ambazo ujenzi wake ulianza muda mrefu sana na skimu hizi hazifanyi kazi ikiwemo Skimu ya Lukenge ambayo ina wakulima zaidi ya 3,000 na Skimu ya Luhindo ina wakulima zaidi ya 2,400; tarehe 25 Machi, mlitangaza *tender* ya kumpata mzabuni wa kununua pampu mbili kwa ajili ya kwenda kufunga kwenye hizi skimu. Je, ni lini Serikali itakamilisha kazi ya kutafuta hizi pampu na kwenda kufunga ili skimu hizi ziweze kufanya kazi na kuwasaidia wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Mlali, Kijiji cha Mlali tuna skimu ambayo inajiendesha kienyeji, ina wakulima zaidi ya 400 na ni skimu ambayo ina hekta zaidi ya 500. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuwatuma wataalamu wa umwagiliaji kwenda kufanya tathmini ili skimu hii iweze kupanda hadhi na iweze kupangiwa bajeti ili kuiboresha hii skimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Skimu za Lukenge na Ludigo ambapo tuliweka pampu katika tenda na zimeshafika mkoani, ninachomwagiza tu *RM* wa Mkoa wa Morogoro ni kuzipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ambayo ilichelewesha ni hizi mvua zilizokuwa zimezidi sana, ndiyo maana walishindwa kupeleka, kwa sababu unaweza kupeleka halafu vikaharibika tena. Kwa hiyo,

kwa sababu mvua zinaendelea kupungua, maana yake tutaendelea kuzikamilisha ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Skimu ya Mlali, tutawatuma wataalamu ili waende pale wakafanye tathmini na upembuzi yakinifu ili watuletee gharama halisi na kuijenga kisasa ili mradi uweze kutumika kwa wananchi wote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tuna Skimu ya Mbwasa na Skimu ya Udimaa ambazo tayari Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu. Je, ni lini sasa Serikali itatangaza tenda za ujenzi wa hizi skimu mbili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba skimu zote mbili ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ikiwemo ya Mbwasa zipo katika mchakato wa kumtafuta mkandarasi hivi sasa tunavyozungumza. Kwa hiyo, mchakato ukishaisha, maana yake sasa tutasaini mkataba ili zianze ujenzi wake, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Serikali tunayoimalizia ilitenga fedha za *feasibility study* na ujenzi wa Skimu za Netrom, Makeresho, Bolutu, Kikafu Chini, Mwera, Kalali, Bwana Mganga, Mtambo, Ismail, Longoi, Mapacha pamoja na ujenzi wa *common using facilities*. Je, ni lini sasa Serikali itaanza *feasibility study* na ujenzi wa miradi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mchakato wa *feasibility study* unaendelea, nikuhakikishie tu kwamba miradi yote ambayo tuliiweka katika bajeti, washauri elekezi wametafutwa kwa ajili ya hiyo kazi ambayo inafanywa sasa hivi. Kwa hiyo, nikuondoe shaka tu kwamba watu wa Makeresho watapata huduma yao pamoja na maeneo mengine yote uliyoyataja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Skimu ya Umwagiliaji ya Ruaha Mbuyuni imebomoka kwa muda mrefu sasa na inawahudumia wananchi zaidi ya 10,000 pale. Ni mpango gani wa Serikali kuhakikisha kwamba ukarabati wa haraka unafanyika ili wale wananchi waendelee kunufaika na shughuli zao za kilimo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua changamoto ya Skimu ya Ruaha Mbuyuni na tutairekebisha haraka iwezekanavyo. Changamoto kubwa zilikuwa ni hizi mvua ambazo zilikuwa zinaendelea. Kwa hiyo, hatuwezi kuiacha kwa sababu tunajua umuhimu wa hii skimu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Namwita sasa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 194

**Kuimarisha Kilimo cha Minazi Ukanda wa Pwani**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuimarisha kilimo cha Minazi katika Ukanda wa Pwani ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* imefanya utafiti na kuanzisha aina mpya ya mbegu ya minazi iitwayo *East African Tall (EAT)* ambayo inastawi katika maeneo ya ukanda wa Pwani na kuvumilia magonjwa. Baada ya kupatikana kwa mbegu hiyo, Serikali katika msimu wa mwaka 2023/2024 imeiwezesha *TARI* kuzalisha miche 140,000 ambayo itasambazwa kwa wakulima katika Halmashauri za Wilaya za ukanda wa Pwani kuanzia mwezi Oktoba, 2024.

Aidha, jumla ya mbegu za nazi 18,000 zinatarajiwa kusambazwa kwenye vitalu vya Halmashauri za Ruangwa, Mtwara Vijijini, na Muheza. Katika msimu wa 2024/2025 *TARI* inatarajia kuzalisha miche 200,000 ya aina hiyo ya nazi na kusambaza kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kupitia taasisi zake itaendelea kutoa elimu ya kanuni bora za kilimo cha nazi na teknolojia za uthibiti wa visumbufu vya nazi kwa maafisa ugani na wakulima katika wilaya zote zitakazopatiwa miche mipya kwa ajili ya kufufua mashamba ya nazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali, lakini bado kuna changamoto. Kwa kuwa, zao la nazi ni zao la kiuchumi katika ukanda wa Pwani na Zanzibar, minazi mingi imekuwa ikifa kwa kushambuliwa na magonjwa na hakuna juhudi mbadala. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuinusuru minazi inayokufa na inayoshambuliwa na magonjwa katika ukanda wa Pwani na Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa minazi mingi ni ya muda mrefu na hasa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Mtwara, Tanga na Zanzibar na inakufa na hakuna juhudi yoyote ya kuimarisha zao la minazi: Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu katika mashule pamoja na vyombo mbalimbali vya habari ili kuimarisha zao hilo la mnazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Kilimo moja ya kazi kubwa tunayoifanya ni kwamba tumeandaa mipango wa muda mfupi, mpango wa kati na mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ambayo tunaendelea nayo sasa hivi ni kuendelea kufanya tafiti ili kukabiliana na magonjwa. Ndiyo maana ukiona katika jibu la msingi tumepata mbegu mpya ambayo inaweza kukabiliana na magonjwa ya nazi, kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo kwa wakulima wote wa Kanda za Pwani na tutaendelea kutuma wataalamu wetu waendelee kufanya tafiti kukabiliana na hayo magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, tutaendelea kutoa elimu mashuleni na huo ndiyo mpango tuliokuwanao sasa hivi, isipokuwa tu tutaongeza kasi ili uweze kuanzia *level* ya shule kwa maana ya wanafunzi mpaka kufika kwa wanakijiji ambao ni wakulima, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, kwa kifupi.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza mara kwa mara hapa Bungeni kuhusu nini mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo katika kuimarisha kilimo cha vanilla ili wakulima wa vanilla wa Mkoa wa Kagera waweze kunufaika na zao hili? Kwa hiyo, ningependa kupata kauli thabiti ya Serikali, ni nini itakwenda kufanya ili kuhakikisha kilimo cha vanilla kinanufaisha wakulima wa Mkoa wa Kagera? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Wizara ya Kilimo sasa hivi tuna mpango wa kuwaita wadau wote wa sekta ya vanilla wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wakulima pamoja na wafanyabiashara ili tuweze kukaa pamoja na kujadiliana kuona namna bora ambayo tunaweza tukasaidia kukuza kilimo cha

vanilla. Miongoni mwa mipango tuliyonayo ni pamoja na kutafuta masoko na kuongeza bei ya vanilla ili wananchi wetu waweze kunufaika zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunakwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, namwita sasa Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, aulize swali lake.

Na. 195

**Shughuli za Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania – *TCU* Zanzibar**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani kuimarisha shughuli za *TCU* Zanzibar ili kupunguza usumbufu kwa wadau wa elimu Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* inatekeleza majukumu yake yote katika pande zote mbili za Muungano. Majukumu hayo yanahusisha utoaji wa mafunzo kwa Viongozi na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vilivyopo Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu masuala ya elimu ya chuo kikuu, ikiwemo Uongozi na Usimamizi wa Vyuo Vikuu, Uandaaji wa Mitaala inayokidhi mahitaji ya soko, Mbinu Bora za Ufundishaji na Uthibiti Ubora wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, katika kipindi cha Juni, 2023 hadi Machi, 2024 viongozi na wahadhiri 48 kutoka vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar wamepata mafunzo yaliyojumuisha viongozi na wahadhiri kutoka vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 49 vilivyosajiliwa chini ya *TCU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCU* kila mwaka hufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu yake. Kutokana na tathmini hiyo, mikakati ya uboreshaji huwekwa kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya *TCU* katika pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa *TCU* ni taasisi ya Muungano inayowakilisha Zanzibar na Tanzania Bara: Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni busara kama kutakuwa kuna mkakati wa maana wa kuweza kuboresha na kupanua wigo wa uwakilishi wa Zanzibar ndani ya chombo cha *TCU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa *TCU* ni taasisi ya Muungano ambayo haina ofisi Zanzibar, kitu ambacho kinakwamisha na kuchelewesha kazi za vyuo vikuu pamoja na wahitimu wa vyuo vikuu kutoka Zanzibar: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga ofisi Zanzibar pamoja na kuwa na Afisa Masuuli wa *TCU* ili kuimarisha uratibu kwa upande wa Zanzibar? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa upande wa uwakilishi kwa maana ya ule wa kitendaji katika ngazi ya utendaji, taasisi yetu ina uwakilishi mzuri kutoka upande wa Zanzibar kwa sababu tuna Wajumbe wale wa Bodi ya *TCU* pamoja na Kamati zake, tuna uwakilishi wa kutosha kwa sababu baadhi ya Wajumbe wanatoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na kuwa na ofisi, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi utaratibu wa taasisi yetu jinsi unavyofanya kazi ni kwa njia ya mtandao. Kwa hiyo, haijalishi mtu yuko umbali gani awe Zanzibar, awe Mkoa wowote au hata nje ya nchi, bado anaweza aka-*access* mtandao huo na kufanya *application* na kufanya kazi zote kupitia mtandao.

Mhshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua wazo lake la kuweza kuwa na ofisi kule Zanzibar ili kurahisisha utendaji kazi wa taasisi yetu hii ya Muungano. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako. Tunakwenda Wizara ya Maliasili na Utalii, nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, aulize swali lake.

Na. 196

**Ajira katika Hoteli za Serengeti na Ngorongoro**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, Chuo cha Utalii Dar es Salaam na Vyuo vingine vya utalii vimetoa wafanyakazi wangapi ngazi ya Menejimenti katika Hoteli za Serengeti na Ngorongoro?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro zipo hoteli zinazotoa huduma za malazi za kudumu 13. Kati ya hizo, 12 zimeajiri Mameneja wazawa na moja imeajiri Meneja ambaye ni raia wa kigeni. Kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kati ya hoteli 31 zinazotoa huduma za malazi za kudumu 22

zimeajiri Mameneja wazawa na tisa zimeajiri baadhi ya Mameneja ambao ni raia wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Chuo cha Taifa cha Utalii *(NCT)* kinatoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Diploma ambayo yanawezesha wahitimu wengi kuajiriwa katika kada ya utendaji na baadhi katika kada za usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kuwa Chuo cha Taifa cha Utalii kwa sasa hakitoi mafunzo kwa ngazi ya shahada na kimekuwa na changamoto ya kutoa wafanyakazi katika ngazi ya menejimenti kwenye hoteli, kwa hali hiyo, hoteli nyingi zinazotoa huduma za malazi zimeajiri Watanzania katika ngazi ya menejimenti waliomaliza kozi za utalii katika vyuo vingine nchini ikiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, baada ya kumpata Mkuu wa Chuo Dar es Salaam ambaye ameanza kutangaza habari za chuo hicho, Chuo chetu cha Utalii - Dar es Salaam kinajiandaa kuwa kituo cha umahiri. Je, Serikali imefikia hatua gani katika mipango yake ili kuona kabisa kwamba watoto wanaotoka pale wanakuwa mahiri kweli kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu wahudumu wetu, yaani wanaita *Wazungu Customer Care,* Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba vijana wetu wote wanaomaliza Vyuo vya Utalii vya Binafsi na vya Serikali wanapata mafunzo kazini ili watoe huduma bora katika mahoteli yetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo chetu cha Utalii kilichopo Dar es Salaam na matawi yake kule Arusha na Mwanza, kimefanya maboresho katika mitaala ya mafunzo ili kuongeza umahiri wa wahitimu wetu katika sekta ya utalii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kuimarisha mitaala hii, tunayo imani kubwa sasa kwamba mafunzo yatakayotolewa na umahiri wa wahitimu wetu utakuwa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye eneo la *customer care*, ni kweli imekuwepo changamoto ya wahudumu wetu kulalamikiwa mara kwa mara. Nataka nimhakikishie kwamba jambo hili linafanyiwa kazi kwa umakini mkubwa na kama anafuatilia kwa ukaribu huduma sasa hivi za watu wetu zimeanza kuimarika kwa kiasi kikubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunakwenda Wizara ya Ujenzi, namwita sasa Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Kilave.

Na. 197

**Ujenzi wa Barabara Pembezoni mwa Reli ya *SGR***

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami pembezoni mwa reli ya *SGR* wakati ujenzi unaendelea?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017, hifadhi ya reli ni meta 30 kutoka katikati ya reli kila upande. Katika eneo hili hairuhusiwi kujenga barabara kwa matumizi ya kawaida. Hivyo, haitawezekana kujenga barabara ya lami pembezoni mwa reli ya *SGR*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Serikali. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *ring road* katika Mkoa wa Dar es Salaam?

Swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za ziada au nyingi zaidi kwa ajili ya barabara na mifereji ya kutosha katika Mkoa wa Dar es Salaam hasa katika Jimbo la Temeke, ukizingatia sasa hivi mvua zinavyonyesha, Temeke haipitiki, tumekuwa hatuwezi kufanya tena biashara; lini Serikali mtatenga fedha za kutosha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kujenga *ring road* Dar es Salaam, upo kwenye *masterplan* na tayari tunafanya usanifu kuanzia Bunju unakuja Kibamba kwenda Kisoko kuja Chanika mpaka Temeke Kigamboni. Kwa hiyo, mpango huo *(masterplan)* upo na sasa hivi tumesham-*engage* Mhandisi Mshauri anafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mifereji na kutenga fedha nyingi, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali inafanya kazi kubwa sana kwa sasa kuzijenga hizi barabara. Katika *design* yoyote katika usanifu wowote ni kweli kwamba tunajenga barabara hizo. Changamoto iliyopo ni kwamba unapojenga barabara mpya ambazo zinakuwa za kiwango na

mifereji, pengine zile barabara nyingine ambazo zinakuwa mifereji yake haijajengwa, zinashindwa kupokea yale maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya sasa hivi katika usanifu ni kuhakikisha kwamba tunashirikiana watu wa *TANROADS* na wenzetu wa *TARURA* ili wanaposanifu ile miradi iendane, ikiwa ni pamoja na kupeleka maji na kuyaweka yanapostahili ili kutokuleta hiyo changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameielezea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nimewaona wote, lakini muda wetu umepita sana. Nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunakwenda Wizara ya Afya, namwita sasa Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 198

**Hitaji la Watumishi na Vifaa Tiba Hospitali ya Mkoa wa Geita**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi pamoja na Vifaa Tiba katika Hospitali ya Mkoa wa Geita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Geita ina jumla ya watumishi 349. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepeleka watumishi 22 wa kada mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita. Pia Serikali imepeleka vifaa tiba vyenye thamani

ya shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chagula, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza. Hospitali za Wilaya ya Nyang'hwale, Mbogwe, Bukombe na Chato hazina madaktari bingwa wa watoto na akina mama. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka madaktari bingwa wa watoto na akina mama katika hospitali hizi ili tuweze kupunguza msongamano wa wagonjwa uliopo katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Geita? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambayo anaifuatilia sana hospitali yake ya Mkoa wakati wote pamoja na namna ambavyo anajua mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye Wilaya za Mkoa wake wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza kwenye miongozo ya Wizara kuna utaratibu wa rufaa; na kila *level* ya hospitali ina aina gani ya kada inahitaji kwa *level* fulani ya elimu. Mimi na mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Dugange tutakaa naye tumweleze na tuone namna ya kushirikiana na kuelekeza namna ya kushauri wananchi, inapotokea mambo mbalimbali yanayohitaji baadhi ya aina ya madaktari wafanye nini kwa wakati huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa ya Watendaji katika Hospitali ya Mkoa ya Kitete

Tabora. Serikali ina mpango gani wa kutuongezea wafanyakazi wenye weledi katika hospitali yetu ili waweze kutoa huduma thabiti kwa wananchi wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kuboresha na kama ambavyo umesikia, hata mwaka huu upo utaratibu kwamba wataajiriwa watumishi wengine. Ndiyo maana wiki iliyopita nilikuwa pale, ni kwa ajili ya kuhakikisha tunaboresha huduma kwenye Hospitali yetu ya Kitete. Mheshimiwa Waziri wa Afya alinituma pale nimekwenda, nimeangalia matatizo mbalimbali yaliyohitaji kuchukua uamuzi pale tumechukua uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwambam kwa maelekezo ya Waziri wa Afya, pale Hospitali ya Wilaya ya Kitete itakaa vizuri kama Waheshimiwa Wabunge mlivyotegemea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Katiba na Sheria, namwita sasa Mheshimiwa Noah Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, aulize swali lake.

Na. 199

**Ujenzi wa Mahakama - Kata ya Bwawani**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Mahakama Kata ya Bwawani katika Jimbo la Arumeru Magharibi?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha majengo ya Mahakama katika maeneo mbalimbali nchini, hususan Mahakama za Mwanzo. Kwa sasa tunazo Mahakama 960 nchi nzima, baadhi zikiwa na majengo chakavu na ya zamani, hivyo yanahitaji kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Bwawani kwa sasa wanapata huduma za Mahakama katika Mahakama ya Mwanzo ya Nduruma ambayo kwa sasa inafanya kazi kwa kutembelewa. Mahakama hii ya Nduruma ipo umbali wa kilomita 15 kutoka Bwawani na inasajili wastani wa mashauri 120 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa kuzingatia umuhimu, katika mwaka wa fedha 2023/2024 tunajenga Mahakama ya Mwanzo Maji ya Chai katika Jimbo la Arumeru. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Bwawani utazingatiwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 kulingana na mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yenye mkanganyiko wa kimaeneo, naomba kusema kwamba eneo la Maji ya Chai halipo katika Jimbo la Arumeru Magharibi, lipo katika Jimbo la Arumeru Mashariki. Kwa hiyo, Maji ya Chai siyo Arumeru Magharibi. Jambo lingine, kilometa 15 alizotaja hapa, siyo sahihi. Naomba kwenda kwenye maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika maeneo hayo kulikuwepo na changamoto ya kiusalama zaidi na Serikali ikaamua

kwa maana ya Jeshi la Polisi kupeleka Kituo cha Polisi katika eneo la Kata ya Bwawani: Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Mahakama ili kuhakikisha kwamba kuna amani na utulivu katika maeneo hayo na haki ipatikane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kulikuwepo kuna suala la mradi wa ujenzi wa Mahakama kwa kata ambazo zipo ndani zaidi, na tukaorodhesha ikiwemo Kata hiyo ya Bwawani. Je, mradi huo umekufa au haupo tena?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, najua tunapozungumzia Majimbo au Halmashauri kwenye upande wa Mahakama huwa tunakwenda kwenye mwelekeo wa kiwilaya ndiyo maana tumeweza kuitaja Wilaya ya Arumeru, lakini nimemwelewa vizuri, tutaweza kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuweka sawa maeneo haya ambayo ameona kama yana mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa Kituo cha Polisi na hivyo kuhitaji Mahakama. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni nia ya Serikali kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi ili waweze kupata haki kwa wakati. Hata hivyo, nia yetu hiyo njema inategemea upatikanaji wa fedha, ndiyo maana Mahakama imekuja na mpango wa ujenzi wa Mahakama katika maeneo mbalimbali. Kadiri fedha zinapopatikana, maeneo hayo yataendelea kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa kata hizi, ndiyo maana nimemwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka 2026/2027, eneo analolisema tutaweza kulizingatia katika ujenzi wa Mahakama. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Una swali lingine hapo bado. Nimwite sasa Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 200

**Ujenzi wa Mahakama mpya Kata za Chala na Kate – Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama mpya katika Kata za Chala na Kate Jimbo la Nkasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania inaendelea kuboresha miundombinu ya majengo ya Mahakama hususan kwa ngazi ya Mahakama za Mwanzo ambako ndiko kwenye changamoto kubwa ya uhaba na uchakavu wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata za Kate na Chala wanapata huduma za Mahakama ndani ya kata zao katika Mahakama ya Kate na Chala japo majengo ya Mahakama hizi ni chakavu. Kulingana na mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama, katika mwaka wa fedha 2023/2024 tunajenga Mahakama ya Mwanzo Namanyere na katika mwaka wa fedha 2024/2025 tutajenga Mahakama ya Mwanzo Kate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Mahakama ni kujenga majengo ya Mahakama za Mwanzo katika maeneo ambayo hakuna kabisa huduma za Mahakama ili kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za kimahakama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nina swali moja la nyongeza. Kata ya Kipande na Kata ya Sintali wananchi wanatembea umbali mrefu na wanatumia muda mrefu kufuata huduma za Mahakama. Lini mtajenga Mahakama katika Kata ya Sintali na Kipande? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wapo wananchi wanatembea umbali mrefu hasa kwenye maeneo yenye mtawanyiko wa watu kama Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, kadri tutakavyopata fedha tutaendelea kupeleka huduma hizi za Mahakama kwenye maeneo ambayo hayana kabisa ikiwemo kata hizi alizozitaja za Kipande na Sintali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya mwisho, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Namwita Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aweze kuuliza swali lake.

Na. 201

**Mgogoro wa Ardhi wa Rwanyabara – Bukoba Vijijini**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi wa Rwanyabara baina ya mwekezaji na wananchi wa Kijiji cha Bushasha Bukoba Vijijini?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008, uongozi wa Kijiji cha Bushasha kilichopo katika Wilaya ya Bukoba uligawa ardhi yenye ukubwa wa ekari 242 kwa wawekezaji ambao ni Ndugu Deusdelt Rwehabura na Kampuni ya *Kagera Tea Company Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hatua hiyo, familia ya Ndugu Sosthenes Ntagalinda Kajwahula ilifungua Shauri Na. 104/2008 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Bukoba dhidi ya Halmashauri ya Kijiji cha Bushasha ikidai ardhi iliyogawiwa kwa wawekezaji hao ni yao. Tarehe 20 Desemba, 2015, shauri hilo liliamuliwa ambapo familia ya Ndugu Ntagalinda ilipata tuzo ya kuwa wamiliki halali wa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uamuzi huo wa Baraza, wananchi waliokuwemo ndani ya eneo hilo wameendelea kulalamika kwenye ngazi mbalimbali za Serikali, hivyo uongozi wa ngazi ya Mkoa na Wilaya umeanza taratibu za kuzikutanisha pande husika kwa ajili ya suluhisho la ardhi hiyo nje ya mfumo wa Mahakama. Natoa rai kwa wananchi waliopo katika eneo hilo kuwa na subira wakati Serikali ikitafuta njia nyingine ya kumaliza mgogoro uliopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu ni wa muda mrefu na Serikali ya Mkoa na Wilaya ina taarifa ya mgogoro huu na walishindwa kuukamilisha mpaka wakafika hatua hii. Mimi nasema kwamba kwa hatua ambayo Serikali inapanga kwamba sasa wamalize huu mgogoro ambao ni wa kijamii,

mtu hawezi akawa na eka 240 akidai ni chifu na huku wanakijiji wanadai ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naitaka sasa Wizara yenyewe kwa sababu mmekuwa mnaonesha kumaliza migogoro hii, sasa mwende ninyi wenyewe mkasaidie hawa watu wa Mkoa na Wilaya ambao walishindwa kwa muda mrefu. Mwende mkahakikishe mnamaliza mgogoro huu ili mwekezaji apate eneo lake na wanakijiji wapate eneo lao waweze kukaa kwa amani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge tunauchukua na tunakwenda kuufanyia kazi. Nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge tutakwenda huko kwenye eneo la tukio ili tuone kwa kushirikiana na Mkoa tunamalizaje jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na maswali ya leo yamekwisha. Nina matangazo machache hapa. Tangazo la kwanza ni wageni ambao wametutembelea leo.

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri, Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria.

Kwanza ni Katibu Mkuu, Ndugu Mary Makondo, wa pili ni Mheshimiwa Jaji Mstaafu Ndugu Mathew Mwaimu, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ahsante na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni wa tatu ni Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, wa nne ni Ndugu Patience Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za

Binadamu; wa tano ni Ndugu Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)*, anayefuata ni Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali, anayefuata ni Profesa Kennedy Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anayefuata ni Ndugu Bibiana Kileo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka na mwingine ni Ndugu George Mandepo, Katibu Mtendaji Tume ya Utumishi wa Mahakama, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Frank Kanyusi - Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu *RITA*, Ndugu Irene Lesulie - Naibu Kabidhi Wasii Mkuu, Ndugu Onorius John Njole - Mwandishi wa Sheria Mkuu, Ndugu Eva Kiaki Nkya - Msajili Mkuu wa Mahakama, Ndugu Saulo Malauri - Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Msaada wa Kisheria, Ndugu Mary Shirima - Mtendaji wa Mahakama Kuu na Profesa Sist Mramba - Mkuu wa Chuo cha Uanasheria kwa Vitendo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wabunge kutoka Bunge la Vijana la Jumuiya ya Afrika Mashariki, yupo Ndugu Eva Maganga Gerald, Ndugu Mary Ng'Ida Severe, Ndugu Carlyn Laizer na Ndugu Sikitu Elson, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo mgeni mwingine wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Ndugu Getrude Gwarasa ambaye ni Afisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Wilaya ya Uyui, karibu sana. *(Makofi)*

Tunawakaribisha sana kwenye Bunge letu watendaji wote wa Mahakama mliotutembelea leo. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni 107 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye ni shemeji yake kutoka Mkoa wa Iringa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambaye ni mpigakura wake kutoka Mlandizi, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Mwanza, wapo pale juu. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Venant Daud ambao ni wafanyabiashara wa mbao na milango kutoka Igalula, Wilaya ya Uyui Mkoa wa Tabora wanaoishi Dodoma, wapo pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 93 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni viongozi wa UWT Wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga. Wapo pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile kuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi 58 na walimu tisa wa Shule ya Sekondari Mji Mpya kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 30 na walimu wanne wa Shule ya Awali na Msingi Dolphine kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kutoka kwa Katibu wa Bunge angependa kuwafahamisha kwamba Wizara ya Katiba na Sheria wapo viwanja vya Bunge leo tarehe 29 Aprili, 2024 kwa ajili ya kutoa elimu ya sheria mbalimbali na huduma za msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya *Mama Samia Legal Aid Campaign.*

Aidha, *RITA* wanatoa elimu kuhusu huduma za usajili, ufilisi, udhamini, elimu kuhusu kuandika na kuhifadhi wosia pamoja na mirathi. Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kutembelea mabanda hayo, ukitilia maanani kwamba kuna suala la mirathi.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu kwa sasa, tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kuja kusoma Bajeti yake. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, karibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mfuko wa Mahakama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake aliouonesha katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha uongozi wake, kimsingi tunashuhudia maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya sheria, ambapo tumeshuhudia kuimarika kwa mfumo wa utoaji haki, huduma za msaada wa kisheria, kukuza na kulinda haki za binadamu na watu pamoja na misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu ili amjaalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa ambayo umekuwa ukiifanya, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge vema, kwa umahiri na weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya pekee, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(Inter Parliamentary Union)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais

kutekeleza majukumu yao katika Wizara mbalimbali katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 ambao ni Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na ameendelea kuwa msaada mkubwa sana katika Wizara yetu. Pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, ninawatakia kila la heri viongozi wote walioteuliwa katika kutekeleza majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Bibiana Joseph Kileo, Naibu Mkurugenzi wa Mashitaka na Alice Edward Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na Mheshimiwa Jaji Winfrida Beatrice Koloso, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria ambao hawa wote wameapishwa jana na wako tayari kufanya kazi na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiwemo tena Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu; na Dkt. Khatib Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara. Timu hii yote ni muhimu sana, ni timu ambayo iko imara kabisa katika kutekeleza majukumu yetu, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma - Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani - Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania,

Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mheshimiwa Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hao, napenda pia kuwashukuru Wakuu na Watendaji wa Taasisi za Wizara wakiwemo Mheshimiwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Prof. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Profesa Sist Mramba, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Balozi Profesa Kennedy Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na Bwana Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Dkt. Boniphace Luhende Wakili Mkuu wa Serikali; Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bi. Irene Lesulie, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bwana George Nathaniel Mandepo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bwana Mohamed Khamis Hamad, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake. Aidha, kwa namna ya pekee, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati wote ninapokuwa ninatekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru wadau wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ambayo Wizara imekasimiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ila siyo kwa umuhimu, naomba kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuliwakilisha Bunge hili na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa majukumu ya Wizara yameainishwa katika ibara ya 17 na 18 ya kitabu cha hotuba yangu. Masuala yaliyozingatiwa na maeneo ya kipaumbele katika mwaka wa fedha 2023/2024 yameainishwa katika ibara ya 19 na 20 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara pamoja na taasisi zake ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 12.68. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya shilingi bilioni 7.5 zimekusanywa, sawa na 59.29% ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2023/2024, ambayo ni sawa ya 71.15% ya lengo la kipindi cha miezi kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 383.62 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 97.82 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 176.15 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 109.66 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi bilioni 44.11 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 65.54 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 273.63, sawa na 71.33% ya shilingi bilioni 383.62 zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka

wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 75.99 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 157.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 40.14 ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara na taasisi zake ilibainisha masuala mahsusi ya kipaumbele ambayo yametekelezwa kama ilivyoainishwa katika ibara ya 25 hadi 142 ya kitabu cha hotuba yangu. Aidha, baadhi ya masuala yaliyotekelezwa ni pamoja na suala zima la kuratibu mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara ya Katiba na Sheria, kwa imeshirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ambapo tumeandaa Rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kutoa Elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mkakati huo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata uelewa wa Katiba, ikiwa ni pamoja na kufahamu haki na wajibu wao kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi April, 2024 Wizara imetekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika mikoa mitatu ya Ruvuma, Simiyu na Singida, na hivyo kufanya jumla ya mikoa sita ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu na Singida kufikiwa tangu kuzinduliwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kampeni hiyo, jumla ya halmashauri takribani 42, kata 452 na vijiji na mitaa 1,348 vimefikiwa. Aidha, jumla ya wananchi 415,597 wamefikiwa katika ngazi za vijiji na maeneo ya vizuizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa leo tarehe 29 na kesho tarehe 30 kama ulivyotangaza, Wizara

imeweka mabanda hapa katika viwanja vya Bunge ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wa Bunge kupata elimu na huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara na taasisi zake ikiwemo *RITA*. Hivyo nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutembelea mabanda hayo kwa ridhaa yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya Mfumo wa Haki Jinai, Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Kuwalinda Watoa Taarifa na Mashahidi Sura ya 446 kwa lengo la kuiboresha ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoa taarifa na mashahidi unaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imeandaa mkakati wa kutekeleza mapendekezo ya tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha taasisi za haki jinai nchini (Taasisi za Haki Jinai). Mkakati na mpango kazi huo umewasilishwa kwenye Kamati ya Kufuatilia Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Mawakili wa Serikali. Miongozo hiyo ilizinduliwa tarehe 22 Mei, 2024 na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongozo hii ni Mwongozo wa Uandishi wa Sheria *(Legislative Drafting Manual),* Mwongozo wa Utengenezaji wa Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mwongozo wa Upekuzi na Usimamizi Mikataba *(Contract Manual),* Mwongozo wa Utoaji wa Ushauri wa Kisheria, Mwongozo wa Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya, Istilahi za Kisheria na Tafsiri ya Majina ya Sheria Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Zanzibar; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuandaa mapendekezo na marekebisho ya sheria zinazohusiana na masuala ya uchaguzi na demokrasia ambazo ni: -

(a) Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani (Na. 1) ya Mwaka 2024;

(b) Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (Na. 2) ya Mwaka 2024; na

(c) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa (Na. 3) ya Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miswada ya marekebisho ya sheria hizi iliwasilishwa na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu na kisha kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo miswada hiyo ilisainiwa na kuwa sheria kamili zitakazoimarisha masuala ya uchaguzi wa viongozi wa kisiasa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika vikao na majukwaa matatu ya haki za binadamu na watu ya kikanda na kimataifa ambapo taarifa ya jitihada za mafanikio ya Serikali ya kulinda na kukuza haki za raia kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ziliwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inaendelea na uhakiki wa sheria zilizokamilika na kutafsiriwa kwa mara ya kwanza ambapo jumla ya sheria takribani 258 zimekamilika kwa tafsiri ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa rasimu ya taarifa ya nchi kuhusu Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2006, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981 na Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika wa Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki na kuweka mazingira yanayohakikisha usawa katika upatikanaji wa haki kwa wote na kwa wakati, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mipango iliyolenga kufanikisha jukumu hili

muhimu kwa kushughulikia masuala manne muhimu ambayo nitayataja kama ifuatavyo: -

(a) Kufanya mapitio ya mfumo wa haki jinai na kuandaa mpango wa marekebisho ya sheria ambazo zinatoa mianya ya ama kucheleweshwa upatikanaji wa haki au ukandamizaji katika upatikanaji haki;

(b) Kuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri yaliyosajiliwa Mahakamani ili kupunguza na hatimaye kumaliza kabisa mlundikano wa mashauri Mahakamani;

(c) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali; na

(d) Kutekeleza mradi wa maboresho ya mifumo ya huduma za Mahakama kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Mahakama imeshughulikia jumla ya mashauri takribani 196,592. Kati ya mashauri hayo, mashauri 133,823 yamesikilizwa na kuhitimishwa na mashauri 62,769 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Aidha, mashauri yanayoendelea kusikilizwa, mashauri ya umri mrefu ni takribani 2,087 sawa na asilimia tatu ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, hadi kufikia Aprili 2024, miradi iliyokamilishwa ni Mahakama za Wilaya zifuatazo; Ulanga, Kwimba na Liwale. Ukarabati wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Maswa, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo Usevya (Mlele), Nyakibimbili (Bukoba), Mahenge (Kilolo), Newala Mjini (Newala), Madale (Dar es Salaam) Kinesi (Rorya) na Luilo (Ludewa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya Mahakama yanayoendelea kujengwa na kukarabatiwa ni kama ifuatavyo: -

(i) Tunaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki, sita; vya Katavi, Songea (Ruvuma), Songwe, Njombe, Simiyu na Geita;

(ii) Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo tatu, ambazo ni Ilangala (Ukerewe), Mbalizi (Mbeya) na Machame (Kilimanjaro);

(iii) Kuendelea kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya sita ambazo ni Kibiti (Pwani), Nachingwea (Lindi), Simanjiro (Manyara), Hanang (Manyara), Mbulu (Manyara) na Tunduru (Ruvuma);

(iv) Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia 61%;

(v) Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya Ubungo ambapo utekelezaji wake umefikia 98%;

(vi) Ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma ambapo ukarabati umefikia 49%;

(vii) Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ambapo hadi sasa umefikia 97.3%;

(viii) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kabanga (Ngara) unaendelea na upo 97%;

(ix) Ujenzi wa nyumba 48 za Majaji eneo la Iyumbu Dodoma ambapo ujenzi umefikia 98%; na

(x) Kuendelea kwa ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu, jijini Dodoma ambapo ujenzi umefikia takribani 53%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Serikali imesajili jumla ya watoa huduma 46 walioomba kuthibitishwa kama Watoa Huduma za Utatuzi wa Migogoro kwa Mjia Mbadala, ambapo Waendesha Maridhiano watatu, Watoa Huduma za Majadiliano watatu, Wapatanishi 13 na Wasuluhishi 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, hadi Aprili, 2024 wapo Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala *(Alternative Dispute Resolution)* wapatao 576. Kati ya hao, Waendesha Maridhiano 38, Watoa Huduma za Majadiliano 60, Wapatanishi 185 na Wasuluhishi 293.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania *(Tanzania International Arbitration Centre)*. Taasisi hiyo, itakuwa na kituo kimoja ambapo kituo hicho kitaanzishwa kwa kuanza na Kituo cha Dar es Salaam ambapo tayari jengo kwa ajili ya kuanzisha kituo hicho limepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie Taasisi ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania *(Law School of Tanzania)* ilisajili jumla ya wanafunzi 1,242 sawa na asilimia 82.8 ya lengo la udahili wa wanafunzi 1,500 kati ya kundi la 37 na 38. Aidha, wahitimu 15 waliofanya mitihani ya Astashahada ya Wasaidizi wa Sheria walifaulu na kutunukiwa Astashahada ya Wasaidizi wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 tunacho Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto *(Institute of Judicial Administration)* ambacho kimedahili jumla ya wanafunzi 958 wa Astashahada na Stashahada ya Sheria ambayo ni sawa na 73.7% ya lengo la udahili wa wanafunzi 1,300. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 608 walihitimu mafunzo ya ngazi ya Astahashada na Stashahada ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu mapitio na marekebisho ya sheria mbalimbali, lengo likiwa ni kuboresha ufanisi na kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya sheria.

Katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa na kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali katika sekta za sheria *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill No. 4 of 2023)*. Katika kipindi hicho Sheria 22 za sekta ya sheria zilifanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai. Sera hiyo itajumuisha haki na masuala mbalimbali katika mnyororo wa haki jinai ikiwemo utoaji wa taarifa za matukio ya uhalifu, masuala ya ushahidi yataingia katika hiyo Sera ya Haki Jinai, uchunguzi wa uhalifu, ufunguaji wa hati za mashtaka, uendeshaji wa mashtaka, utoaji wa hukumu pia tutauingiza katika Sera ya Haki Jinai, usimamizi wa wafungwa magerezani na urejeshwaji wa wafungwa uraiani baada ya kumaliza kifungo au kupata msamaha wa adhabu ya kifungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 tunacho kitengo maalum cha kuimarisha mfumo wa uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imepitia mikataba 18 ya kukuza na kulinda uwekezaji kati ya Tanzania na nchi mbalimbali kwa lengo la kubaini iwapo inakidhi mahitaji ya sasa ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imeandaa na kusambaza Rasimu ya Mwongozo wa Usajili wa Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za nchi katika sekta zinazohusika na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa uzingatiwaji wa sheria tajwa ambapo mikataba mitano inayohusu uwekezaji katika madini na fukwe za bahari imesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha uwezo wa taasisi na utoaji wa hudma za sheria hususan utoaji haki, Wizara imeandelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imenunua na kusambaza zaidi ya *set* 24 za *video conference,* kompyuta za mezani takribani tano, kompyuta mpakato 86, *printer* 13 na televisheni moja kwa ajili ya Mahakama ya Tanzania, Magereza mbalimbali, Ofisi ya

Taifa ya Mashtaka na Taasisi ya Afya ya Akili ya Mirembe sehemu ya Isanga ili kuimarisha huduma za TEHAMA katika utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa mifumo hiyo ya huduma za utoaji haki kwa njia ya TEHAMA, umehusisha uanzishaji wa kituo cha huduma kwa wateja *(contact center)* kwa ajili ya kupokea taarifa na malalamiko kuhusu huduma za utoaji haki kupitia namba maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuitaja hii namba maalum ambayo tumeianzisha Wizarani *(contact center)*. Wale wote wenye changamoto wanaweza wakapiga namba hii na kutoa taarifa za changamoto zao na kupewa maelekezo stahiki. Namba hii ni 0262160360.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma za kisheria imeimarishwa ikiwemo Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Mawakili Mahakamani *(e-wakili),* Usajili na Usimamizi wa Huduma za Madalali wa Mahakama *(e-court broker),* Usikilizaji wa mashauri Mahakamani kwa njia ya kidijitali inayoonesha kuzungumza na kuonana ana kwa ana pasipo kukutana katika eneo moja (*virtual conference),* Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Bodi za Wadhamini *(e-RITA)* na Unukuzi na Tafsiri *(Transcription and Translation System-TTS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara imeendelea na utekelezaji wa mkakati wa pili wa Taifa wa Haki Mtoto kwa kufanya kikao cha tatu cha jukwaa la Haki Mtoto. Pia, Wizara imewajengea uwezo watoto, wasajili wasaidizi, wasaidizi wa kisheria, Viongozi wa Serikali za Mitaa, Viongozi wa kidini na kimila katika kushughulikia masuala yanayohusiana na masuala ya ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Mahakama na yenyewe imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya tume na Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama ngazi ya mikoa na wilaya kwa kutoa mafunzo elekezi kuhusu Kanuni za Maadili za Maafisa Mahakama na Kanuni mpya za uendeshaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama wa Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2023/2024 jumla ya Wajumbe takribani 91 kutoka Kamati za Maadili kwa Maafisa Wilaya na Mikoa kwa Mikoa ya Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Tanga, Katavi na Rukwa, walijengewa uwezo kuhusu uendeshaji wa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala bora, Serikali kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Sekta ya Sheria Na. 11 ya 2023 ilifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la maboresho haya ni kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za uandishi wa sheria, urekebu na ufasili wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilihakiki kuchapisha jumla ya sheria ndogo 885 ikilinganishwa na sheria ndogo 631 zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufani. Jumla ya kesi za jina 27,205 ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ikilinganishwa na kesi 32,609 zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023. Aidha, jumla ya kesi 16,928 sawa na asilimia 62 zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi 18,485 sawa na 57% ya kesi zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi 680 katika Mahakama za Watoto *(Juvenile Courts)* ambapo kesi 454 zilihitimishwa sawa na 67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi 6,649

katika Mahakama Kuu ya Tanzania ikilinganishwa na kesi 6,425 zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, kesi 2,408 zilihitimishwa sawa na asilimia 36 ikilinganishwa na kesi 2,629 zilizohitimishwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 41 ya kesi zilizoendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi 2,905 za jinai katika Mahakama ya Rufani ikilinganishwa na kesi 1,535 zilizoendeshwa kipindi kama hicho katika mwaka 2022/2023. Kati ya kesi hizo, kesi 414 zilihitimishwa sawa na 14% ya kesi zilizokuwa zikiendeshwa ikilinganishwa na kesi 267 zilizohitimishwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na 17% ya kesi zilizokuwa zikiendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi kubwa 64 katika Mahakama Kuu, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi 90 zilizoendeshwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, kesi 24 zilihitimishwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na kesi 40 kimsingi zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishughulikia jumla ya majalada 16,854 kutoka vyombo vya upelelezi ambapo majalada 11,255 yaliandaliwa hati za mashtaka sawa na 67% ya majalada yaliyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya majalada 16,854 yaliyopokelewa, majalada 1,138 yalifunguliwa na majalada 3,439 yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi. Hivyo, kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 kuwa 15,832 sawa na asilimia 94 ya majalada yaliyopokelewa. Vilevile, majalada 1,022 yalikuwa yanaendelea kufanyiwa kazi kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kusimamia urejeshwaji wa watuhumiwa wa

uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika mwaka 2023/2024 Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi nane kutoka nchi za Uturuki, India, Afrika Kusini wawili na Kenya mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tanzania imetuma jumla ya maombi saba ya kuomba wahalifu katika nchi ya Kenya wawili, Afrika Kusini mmoja, Saudi Arabia mmoja, India mmoja, Uganda mmoja na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo mmoja. Hii ni mikataba ya *extradition*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuthibitika kuwa watuhumiwa wagonjwa walitenda makosa wakiwa na ugonjwa wa afya ya akili, Mahakama haikuwatia hatiani. Hivyo, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya maombi 14 yaliwasilisha Wizarani ambapo amri ya kuwaachilia wagonjwa hao wa afya ya akili ilitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza mpango wa kutenganisha shughuli za mashataka na upelelezi kwa kuendelea kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali na kuendelea kutoa vibali vya kuendesha mashtaka kwa waendesha mashtaka kutoka katika ofisi na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina jumla ya Mawakili 663 pamoja na Waendesha Mashtaka waliopewa vibali na Mkurugenzi wa Mashtaka wapatao 1,095 nchi nzima. Pia jumla ya wataalamu 233 wanaohusika na upelelezi katika maeneo ya maandishi, picha, alama za vidole na milipuko wametangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendesha na kuendelea kuiwakilisha Serikali katika kuendesha mashauri mbalimbali ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2024 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya madai 7,813 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauri takribani 762 yalimalizika. Aidha, katika ya mashauri ya madai yaliyomalizika, mashauri 719 yalihitimishwa Mahakamani na Mashauri 43 yalihitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishinda jumla ya mashauri 705 yenye madai ya fedha na kufanikiwa kuokoa fedha za Serikali jumla ya shilingi bilioni 396.20. Vilevile, imeokoa jumla ya shilingi bilioni 10.21 zilizotokana na mashauri 43 yaliyohitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama. Hivyo kufanya kiasi kilichookolewa kwa kushinda Kesi za Madai na kufanya majadiliano nje ya Mahakama kuwa jumla ya shilingi bilioni 406.41.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imewezesha Serikali kushinda katika mashauri matano yaliyoendeshwa ndani ya nchi na shauri moja la kimataifa ambapo Serikali imeokoa jumla ya shilingi bilioni 38.26 kutokana na kushinda mashauri hayo ya usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imehitimisha mashauri tisa ya usuluhishi kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama ambapo Serikali imeokoa jumla ya shilingi trilioni 1.5. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kuendesha mashauri ya usuluhishi 160 katika vyombo na mabaraza mbalimbali ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, imesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa 1,520,899 pamoja na vyeti vya vifo 25,783. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 *RITA* imesajili jumla ya watoto 678,371 wenye umri wa chini ya miaka mitano katika Mikoa ya Kigoma, Kagera na Dar es Salaam na kufanya idadi ya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano waliosajiliwa kupitia mpango huu kufikia 9,609,664.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kiwango cha usajili katika kundi hili kimeongezeka, hapa ni watoto *under five years* kutoka 13% mwaka

2012 hadi 68% mwaka 2024. Tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametupa maelekezo kwamba watoto chini ya umri wa miaka mitano wasajiliwe na kupata vyeti vya kuzaliwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kutoa rai kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha watoto wanapozaliwa wanasajiliwa ikiwa ni sehemu ya haki ya mtoto pamoja na kuingiza taarifa hizo kwenye kanzidata ya *RITA* ili Serikali ipate takwimu za watoto waliozaliwa kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia wakala, imeendelea kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati kwa wananchi, hususan katika masuala ya mirathi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Aprili, 2024 *RITA* imeandika na kutunza wosia 118 na kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusiana na faida za kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya mirathi inayojitokeza katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa, nchi mwenyeji wa Kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika kikao hicho ambacho kilifanyika pale Arusha, jumla ya wadau 1,860 walishiriki. Baadhi ya manufaa kwa Tanzania kuwa nchi mwenyeji wa kikao hiki ni pamoja na masuala ya utalii na kuingiza fedha za kigeni takribani dola za Marekani 7,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola. Mkutano huo ulifanyika pale Zanzibar kuanzia tarehe 04 hadi 08 Machi, 2024. Aidha, mkutano huo ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wageni takribani 188 kutoka katika nchi mbalimbali takribani 34 Wanachama wa Jumuiya ya Madola walishiriki. Yapo manufaa ambayo Tanzania imenufaika kwa kuwa nchi mwenyeji wa kikao hiki ikiwemo kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekamilisha ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa ya Shinyanga, Manyara, Katavi na Rukwa. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea na ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Njombe na Geita. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Mwanza ambapo mpaka sasa tumefikia 68% na Arusha 12%. Haya ni majiji yetu katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na taasisi zake inatekeleza afua zenye lengo la kuchangia mapambano dhidi ya rushwa. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 miongozo mitatu imezinduliwa ambayo ni Mwongozo wa Kuwajali na Kuwalinda Mashahidi *(Witness Care and Protection Guidelines),* Utaifishaji na Urejeshaji Mali *(Asset Forfeiture and Recovery)* na Usaidizi wa Kisheria wa Pande zote katika Masuala ya Jinai *(Mutual Legal Assistance in Criminal Matters)* kwa Waendesha Mashitaka na Wapelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la miongozo hii ni kuwawezesha Waendesha Mashitaka na Wapelelezi kuwa na uelewa wa kutosha wa masuala ya ulinzi wa mashahidi, urejeshaji na utaifishaji mali pamoja na ushughulikiwaji wa maombi ya usaidizi wa kisheria kwa pande zote katika masuala ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Maboresho ya Utendaji wa Maendeleo ya Rasilimali Watu iliyo chini ya Wizara na Taasisi zake imeainishwa katika Ibara ya 131 hadi 142 ya Kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kila mafanikio kuna changamoto na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake imekabiliwa na changamoto mbalimbali, kama nilivyoeleza katika Ibara ya 143 na 144 ya Kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara na taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria na utoaji haki kwa umma ili kuendana na Mipango ya Sekta

ya Sheria nchini na Mipango ya Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele ambayo yameainishwa yanapatikana kwenye ibara ya 145 ya Kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza vipaumbele tulivyoainisha, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na mafungu yote ya Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimeainishwa katika ibara ya 146 hadi 153 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara na taasisi inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 12.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 441,260,152,000. Kati ya fedha hizo shilingi 112,423,492,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, shilingi 223,164,341,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 105,672,319,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti kwa kila fungu umeainishwa kwenye vitabu vya randama za mafungu husika, ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

(i) ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mfuko wa Mahakama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa kazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizochini ya Wizara pamoja na Mahakama ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(ii) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fadhili zake ikiwemo kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(iii) ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Pongezi**

(iv) ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu. Aidha, katika kipindi cha uongozi wake, tunashuhudia maendeleo na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria, ambapo tumeshuhudia kuimarika kwa mfumo wa utoaji haki, huduma za msaada wa kisheria, kukuza na kulinda haki za binadamu na watu pamoja na misingi ya utawala bora. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

(v) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu.

(vi) ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasilisha hotuba ambayo imefafanua utendaji wa Serikali kwa mwaka 2023/2024 na kutoa mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote waliowasilisha hotuba za Wizara wanazozisimamia kwa mawasilisho yao mazuri.

(vii) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri na weledi mkubwa. Aidha, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani.

(viii) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu katika Wizara mbalimbali katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 ambao ni- Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; Mhe. Jerry William Silaa (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

Vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya

Nchi na Mhe. Zainab Athumani Katimba (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ninawatakia kila la heri viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

**Salamu za Pole**

(ix) ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mhe. Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Zanzibar na Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naungana na Waheshimiwa wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wote. Aidha, Wizara inawapa pole wananchi wa jimbo la Mbarali kwa kifo cha Mhe. Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wao. Vilevile, Wizara inawapa pole wananachi wa jimbo la Kwahani, Zanzibar kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, AMINA.

(x) ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na ajali na maafa katika maeneo mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Itakumbukwa pia mnamo tarehe 3 Desemba, 2023 kulitokea maafa ya maporomoko ya matope katika mji wa Katesh mkoani Manyara, yaliyosababisha athari kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo kwa baadhi ya Wananchi wenzetu, athari katika makazi, mali na rasimali nyingine. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa waathirika wa maporomoko hayo. Aidha, naomba kutoa pole kwa waathirika na manusura wote wa matukio yote yaliyotokea nchini katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Shukrani**

(xi) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiwemo Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu; na Dkt. Khatibu Malimi Kazungu,

Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Wizara.

(xii) ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, napenda kumshukuru Mhe. Prof. Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania.

(xiii) ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hao, napenda pia kuwashukuru Wakuu na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara wakiwemo Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Prof. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Prof. Sist Mramba, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Mhe. Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali; Bw. Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bi. Irene Lesulie, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini; Bw. George Nathaniel Mandepo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mhe. Jaji Mstaafu Mathew P. Mwaimu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bw. Mohamed Khamis Hamad, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Bw. Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(xiv) ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuwashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, kwa namna ya pekee, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa. Pia, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru wadau

wote wa wizara kwa ushirikiano wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu ambayo Wizara imekasimiwa na Serikali.

(xv) ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho ila siyo kwa umuhimu, naomba kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Mkoa wa Njombe.

## B. DIRA NA DHIMA

(xvi) ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni "Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa". Aidha, Dhima ya Wizara ni "kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa".

## C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

(xvii) ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)*. Taasisi nyingine ni Tasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

(xviii) ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 534/2021 majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria ni:-

(i) Kutunga sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;

(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba;

(iii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;

(iv) Uandishi wa sheria;

(v) Kuendesha mashtaka ya jinai;

(vi) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi;

(vii) Usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;

(viii) Kuratibu masuala ya haki za binadamu na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

(ix) Kuratibu usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini;

(x) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria;

(xi) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri asili na maliasilia za nchi;

(xii) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xiii) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na

(xiv) Kuratibu majukumu ya taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

## D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

(xix) ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia Dira na miongozo

mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ambayo ni pamoja na; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (2030); Mpango wa Maendeleo wa Afrika (2063); Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati akifungua Bunge la 11 mwaka 2021; maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mipango Mikakati ya Wizara na taasisi zake wa mwaka 2021/2022-2025/2026.

(xx) ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2023/2024, Wizara ilibainisha masuala ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Kuratibu Mchakato wa Katiba Mpya;

(ii) Kutekeleza Mkakati wa Kutoa Elimu ya Katiba kwa umma;

(iii) Kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (*Mama Samia Legal Aid Campaign*) kwa wananchi kote nchini;

(iv) Kufanya marekebisho ya Sheria za Uchaguzi na Demokrasia;

(v) Kuwasilisha taarifa kwenye vikao 16 na majukwaa ya Haki za Binadamu na Watu katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa;

(vi) Kutekeleza Programu ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika utoaji Haki Nchini;

(vii) Kuwasilisha taarifa tatu (3) za nchi kuhusu Utekelezaji wa Mikataba mitatu ya Haki za Binadamu ambayo Serikali imeridhia;

(viii) Kuendelea kutafsiri Sheria za nchi kutoka lugha ya Kingereza kuwa katika lugha ya Kiswahili;

(ix) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;

(x) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro;

(xi) Kuimarisha mfumo wa elimu ya sheria;

(xii) Kuratibu mapitio na marekebisho ya sheria za sekta ya sheria;

(xiii) Kuandaa sera mahsusi zinazosimamia mifumo ya utoaji haki;

(xiv) Kuendelea kuimarisha mfumo wa uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi;

(xv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria nchini;

(xvi) Kuendelea na ujenzi wa vituo jumuishi vya taasisi za sheria;

(xvii) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kikatiba na utawala wa sheria;

(xviii) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki nchini;

(xix) Kuimarisha mifumo ya kuhamasisha, kuzingatia na kulinda haki za binadamu na watu;

(xx) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto 2020/2021-2024/2025;

(xxi) Kuendelea kuimarisha Usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu pamoja na shughuli za ufilisi na udhamini;

(xxii) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya;

(xxiii) Kufanya Tafsiri, Uandishi na Urekebu wa sheria;

(xxiv) Kutoa ushauri wa kisheria na kufanya Upekuzi na Marejeo ya Mikataba;

(xxv) Kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa kesi za jinai;

(xxvi) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai;

(xxvii) Kuimarisha mfumo wa utaifishaji mali, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu;

(xxviii) Kuimarisha utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

(xxix) Kuratibu, kusimamia na Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi; na

(xxx) Kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

## E. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### *(i) Makusanyo ya Maduhuli*

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi **12,676,201,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na ada ya watoa huduma za msaada wa kisheria, ada za kusajili mashauri, ada za mawakili na faini zinazotokana na mashauri mbalimbali pamoja na pango la ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 7,515,601,174** sawa na asilimia **59.29** ya lengo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2023/24 ambayo ni sawa ya asilimia **71.15** ya lengo la kipindi cha miezi kumi kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.1.**

***(ii) Bajeti Iliyoidhinishwa***

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 383,619,511,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 97,815,618,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, **Shilingi 176,148,324,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 109,655,569,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo **Shilingi 44,112,800,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 65,542,769,000.00** ni fedha za nje **(Kiambatisho Na.2).**

***(iii) Fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi***

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imepokea jumla ya Shilingi **273,632,590,744.49** sawa na asilimia **71.33** ya Shilingi **383,619,511,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka 2023/2024. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi **75,993,267,798.68** ni kwa ajili ya mishahara, Shilingi **157,498,293,263.99** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **40,141,029,681.52** ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha ya miradi ya maendeleo inajumuisha Shilingi **9,712,560,484.37** fedha za ndani na Shilingi **30,428,469,197.15** ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha

zilizopokelewa na Wizara na Taasisi kwa kipindi hicho zimeainishwa katika **Kiambatisho Na. 3a na 3b.**

## F. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE

24. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara na Taasisi zake ilibainisha masuala mahsusi ya kipaumbele ambayo yametekelezwa kama ifuatavyo:-

### *(a) Kuratibu Mchakato wa Katiba Mpya*

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya kikatiba na utawala wa sheria kwa umma kupitia vyombo vya habari vikiwemo redio, televisheni, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara. Aidha, jumla ya wananchi **267,323** wamefikiwa na elimu ya katiba na uraia kwa umma kupitia maadhimisho ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Wiki ya Sheria, Wiki ya Msaada wa Sheria, makongamano, warsha, semina na midahalo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa elimu imeainisha masula ya kikatiba yanayohitajika kujumuishwa kwenye mitaala ya elimu.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mfumo wa utoaji elimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa upande wa Tanzania Bara, na Afisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kutoa Elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma. Mkakati huo unalenga kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa Katiba ikiwa ni pamoja na kufahamu haki na wajibu wao kwa Taifa na kuwawezesha kushiriki katika mijadala ya kikatiba. Rasimu hiyo itajadiliwa na kufanyiwa uamuzi ndani ya Serikali kabla ya kuanza kutumika.

### *(b) Kuratibu na kusimamia masuala ya upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi kote nchini*

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa elimu ya sheria na huduma za kisheria nchini, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (***Mama Samia Legal Aid Campaign***). Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imefikia Mikoa mitatu (**3**) ya Ruvuma, Simiyu na Singida na kufanya jumla ya Mikoa Sita (**6**) ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu na Singida kufikiwa tangu Kampeni hii izinduliwe rasmi tarehe 27 Aprili, 2023 na Mheshimiwa Kassimu Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Halmashauri **42**, Kata **452** na Vijiji/Mitaa **1,348** imefikiwa. Aidha, jumla ya wananchi **415,597** (Wanaume **216,589** na Wanawake **199,008**) wamefikiwa katika ngazi za vijiji na maeneo ya vizuizi.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, jumla ya wananchi **2,775** (Wanaume **1,258** na Wanawake **1,517**) walisajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini – RITA. Aidha, katika Kampeni hiyo, Wakala ilitoa elimu kwa wananchi **14,156** kuhusu usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na umuhimu wa kuandika wosia.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kampeni hii, migogoro **4,546** iliyohusu ardhi (**1,828**), ndoa (**486**), mirathi (**393)**, ukatili wa Kijinsia (**393**), matunzo ya watoto (**518**), masuala ya kijinai (**168**), masuala ya madai (**330)**, migogoro ya ajira (**231**), migogoro mingine ya kisheria (**199**) ilipokelewa ambapo kati ya hiyo migogoro **516** ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia ya usuluhishi na upatanishi. Migogoro **4,030** inaendelea kufanyiwa kazi katika mamlaka mbalimbali za kimahakama na kiutawala.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria imesaidia kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu masuala ya kisheria ikiwemo haki na wajibu wao, utatuzi wa migogoro ya ardhi, madai, jinai, masuala ya haki za binadamu na utawala bora, ulinzi wa haki za makundi mbalimbali kama wanawake na watoto na

kuimarisha ulinzi na amani miongoni mwa jamii; kuleta utangamano katika familia na tija katika jamii kwa wananchi kushiriki zaidi katika shughuli za kujiongezea kipato katika uzalishaji kwa kupunguza muda mwingi wanaotumia kufuatilia migogoro katika Mahakama.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupokea maoni kuhusu uimarishwaji wa huduma ya msaada wa kisheria, ikiwa ni pamoja na maoni ya Bodi ya Taifa ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria, kuhusu uboreshwaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 na Kanuni zake za Mwaka 2018. Aidha, Wizara imefanyia kazi maoni yaliyotolewa na wadau na Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria. Baadhi ya marekebisho yaliyofanyika kutokana na maoni ya wadau ni kufutwa kwa ada ya usajili kwa Wasaidizi wa Kisheria; na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania kutumia wanafunzi wake kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika maeneo wanayokwenda kufanya mazoezi ya uwandani. Aidha, Wizara inaendelea kufanyia kazi maoni na mapendekezo mengine yaliyopo.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa huduma za msaada wa kisheria, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Msaada wa Kisheria nchini, ilifanya Kongamano la Msaada wa Kisheria la Mwaka 2023 katika Mkoa wa Dodoma. Lengo kuu la kongamano hili lilikuwa ni kuendelea kuwaweka pamoja wadau wa msaada wa kisheria na Serikali na kujadiliana namna bora ya kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi kupitia huduma za msaada wa kisheria nchini. Kongamano hili lilihudhuriwa na washiriki **122** (wanawake **80** na wanaume **42**).

*33.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki katika Kongamano la Kikanda la Nchi za Asia, Pasifiki na Afrika lililofanyika nchini India. Kongamano hili lilihudhuriwa na Mawaziri wa Sheria, Majaji Wakuu na Maafisa wengine wa Serikali na Taasisi zisizo za kiserikali. Katika kongamano hili, uzoefu ulionesha kwamba baadhi ya nchi zimejikita katika kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa mashauri ya jinai pekee na nyingine zikijikita katika masuala ya madai pekee. Aidha, kwa nchi zenye Mfuko wa Msaada wa Kisheria, uzoefu ulionesha kuwa nchi hizo

zina uwezo wa kutanua wigo wa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo ya pembezoni. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau inafanya tathmini ili kuona uwezekano wa kuwa na Mfuko wa Msaada wa Kisheria nchini.

*34.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya Kongamano la Mtandao wa Huduma za Msaada wa Kisheria wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kongamano hili lilihudhuriwa na washiriki **50** (Wanaume **17** na Wanawake **33**) kutoka nchi za Kenya, Tanzania Bara na Zanzibar, Rwanda, Burundi na Uganda. Kupitia Kongamano hili wajumbe walijadili na kuainisha fursa zilizopo katika upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yao.

*35.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Wizara ilishiriki kutoa elimu ya sheria na huduma za msaada wa kisheria wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria, Siku 16 za Kupinga Ukatili na Siku ya Maadili na Haki za Binadamu na maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Kupitia maadhimisho hayo, jumla ya wananchi **406** (Wanaume **260 na** wanawake **146)** walifikiwa na kupatiwa elimu ya sheria katika masuala ya ardhi, ukatili wa kijinsia, mirathi na wosia, haki na wajibu. Aidha, jumla ya vipeperushi na vijitabu **670** kuhusu masuala ya mirathi, wosia, talaka, ardhi, haki za wanawake na watoto, msaada wa kisheria, na utajili asilia viligawiwa kwa wananchi bure wakati wa maadhimisho hayo. Aidha, wanafunzi **200** wa Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma walijengewa uwezo kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kwa lengo la kujilinda wao binafsi na kushughulikia masuala hayo katika jamii zinazowazunguka.

*36.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kujenga uwezo kwa wadau mbalimbali kuhusu masuala ya msaada wa kisheria. Jumla ya wadau **366** kutoka makundi mbalimbali walijengewa uwezo. Makundi hayo yanajumuisha Watendaji wa Halmashauri, Kata, Mitaa na Vijiji **44**, Wajasiriamali wanawake **40**, Waandishi wa Habari na Wanahabari **28,** Wasaidizi wa Kisheria **92**, Viongozi wa dini na viongozi wa kimila **74**, wajumbe wa Mabaraza ya Kata **48** na Wasajili wasaidizi wa watoa huduma za msaada wa kisheria **40**. Mafunzo haya kwa pamoja yalilenga kuimarisha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria

kwa wananchi kupitia wasaidizi wa kisheria na watendaji katika ngazi za kijamii. Aidha, waandishi wa habari na wanahabari walijengewa uwezo kuhusu namna ya kutoa taarifa za masuala ya ukatili wa kijinsia na kufuatilia upatikanaji haki kwa manusura.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuimarisha mfumo wa usajili wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria na Wasaidizi wa kisheria nchini kwa lengo la kuhakikisha huduma za usajili zinaboreshwa, kuwa na takwimu sahihi za wanufaika wa huduma za msaada wa kisheria, kuwa na mfumo thabiti wa taarifa za wadau wanaoshughulika na masuala ya wananchi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma mahali walipo kwa haraka na kwa ufanisi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya Mashirika **99** ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na Wasaidizi wa Kisheria **589** walisajiliwa katika Mikoa **26** ya Tanzania Bara. Idadi hii inafanya kuwa na jumla mashirika **270** na wasaidizi wa kisheria **2,114** waliosajiliwa nchi nzima.

### *(c) Kusimamia Mfumo wa Haki na Utoaji Haki*

38. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usimamizi wa mifumo na masuala ya usalama na kuwezesha upatikanaji haki, Wizara inafanya mapitio ya Sheria ya Kuwalinda Watoa Taarifa na Mashahidi, Sura ya 446 kwa lengo la kuiboresha ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoa taarifa na mashahidi. Vilevile, Wizara imefanya tathmnini ya kuanzisha mfuko wa kuwalinda mashahidi na watoa taarifa kwa lengo la kuwa na mfumo bora wa kitaasisi utakaohakikisha ulinzi na usalama wa mashahidi na watoa taarifa.

39. ***Mheshimiwa Spika**,* katika kufanya mapitio ya Mfumo wa Haki Jinai, Wizara imechambua taarifa ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini, baada ya uchambuzi huo Mkakati wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume tajwa umeandaliwa ambao umejumuisha majukumu ya Wizara pamoja na wadau wengine zikiwemo taasisi zilizo chini ya Wizara. Vilevile, Wizara imeandaa Mpango Kazi wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume na Mpango Kazi wa Marekebisho ya Sheria ambazo Tume

ilipendekeza sheria hizo kufanyiwa marekebisho ili zikidhi matakwa ya utoaji haki. Mipango Kazi hiyo imewasilishwa kwenye Kamati ya Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa Miongozo mbalimbali kwa ajili kuboresha utendaji wa Mawakili wa Serikali. Miongozo hiyo ilizinduliwa tarehe 22/5/2024 na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongozo hii ni Mwongozo wa Uandishi wa Sheria (*Legislative Drafting Manual*), Mwongozo wa Utengenezaji wa Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mwongozo wa Upekuzi na Usimamizi Mikataba (*Contract Manual*), Mwongozo wa Utoaji wa Ushauri wa Kisheria, Mwongozo wa Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya, Istilahi za Kisheria na Tafsiri ya Majina ya Sheria Kuu.

### *(d) Kufanya marekebisho ya Sheria za Uchaguzi na Demokrasia*

41. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwezesha kutungwa kwa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali ya Sheria za Sekta (*The Legal Sector Laws* (*Miscellaneous Amendments*) *Act No. 11 of 2024*) ambayo pamoja na masuala mengine ilirekebisha Sheria za zinazogusa masuala ya demokrasia. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; na Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewezesha kutungwa na kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi na demokrasia ambazo ni:- Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani (Na. 1) ya Mwaka 2024;

(i) Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani (Na. 1) ya Mwaka 2024;

(ii) Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (Na. 2) ya Mwaka 2024; na

(iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa (Na. 3) ya Mwaka 2024 (*The Political Parties Affairs Laws Amendment Act No. 03 of 2024*).

***(e) Kuwasilisha taarifa kwenye vikao na majukwaa ya Haki za Binadamu na Watu katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa***

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika vikao na majukwaa ya haki za binadamu na watu ya kikanda na kimataifa ambapo taarifa za jitihada na mafanikio ya Serikali za kulinda na kukuza haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ziliwasilishwa katika vikao vifuatavyo:-

(i) Kikao cha **53** cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika tarehe 19 Juni hadi 14 Julai 2023 Geneva-Uswisi ambapo Serikali iliwasilisha maelezo kuhusu mabadiliko ya tabianchi na haki ya kupata chakula kwa kueleza mifumo na sera zilizopo katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030;

(ii) Kikao cha **54** cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika tarehe 11 Septemba hadi 13 Oktoba, 2023 Geneva-Uswisi ambapo Serikali iliwasilisha maelezo kuhusu namna inavyotekeleza haki ya maji safi na salama, haki za wazee, namna inavyosimamia kemikali hatarishi, haki ya maendeleo, na kujumujisha masuala ya jinsia katika kazi zote za Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kwa kuwa na Sera, Sheria, mikakati, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 kwa lengo la kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030; na

(iii) Kikao cha **55** cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia tarehe 24 Machi hadi 6 Aprili, 2024 Geneva Uswisi na Serikali ilieleza namna ambavyo inalinda, inahifadhi na kukuza haki za binadamu kuhusu watu wenye ulemavu wakiwemo watu wenye ualbino,

uhuru wa kushirikiana, haki ya kuishi katika mazingira safi na salama na suala la mabadiliko ya tabia nchi.

***(f) Kutekeleza Programu ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika utoaji Haki Nchini***

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na uhakiki wa sheria zilizokamilika na kutafsiriwa kwa mara ya kwanza ambapo jumla ya Sheria Kuu **258** zimekamilika tafsiri ya awali. Hivyo, Mpango kazi umeandaliwa kwa ajili ya kuzifanyia uhakiki na kuzitangaza Sheria hizo ili zianze kutumika. Aidha, zipo Sheria **46** ambazo zimetafsiriwa na tafsiri yake imetumia lugha ya kitaalam zaidi (mfano Sheria ya Famasi Sura ya 311). Hivyo, Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta ili sheria hizo zitafsiriwe kwa Kiswahili sanifu.

***(g) Kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mikataba mitatu ya Haki za Binadamu ambayo Serikali imeridhia***

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa rasimu ya taarifa ya Nchi kuhusu Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2006, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981 na Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika wa Mwaka 2003.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu haki za binadamu kwa lengo la kujua haki, uhuru na wajibu wao kwa mujibu wa Sheria za kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, elimu imetolewa kama ifuatavyo:-

(i) Wizara iliandaa Kikao Kazi kuhusu Mfumo wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia tarehe 17 hadi 20 Julai, 2023 mkoani Morogoro ili kuwajengea uwezo wadau **49** kutoka katika

Wizara na Idara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Washiriki walijengewa uwezo katika masuala ya haki za binadamu ikiwemo uaandaji na uwasilishaji wa taarifa za nchi za utekelezaji wa mikataba na itifaki ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia.

(ii) Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Kitaifa ya Siku ya Wakulima Nanenane kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti, 2023 mkoani Mbeya ambapo ilitoa elimu kwa washiriki **221** (Wanawake walikuwa **122** na Wanaume **99**) kuhusu haki za binadamu na wajibu wa jamii kwa mujibu wa Ibara ya 12 hadi 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa iliyoridhiwa na Serikali na haki hizo kuwepo kwenye Katiba na Sheria za Tanzania.

(iii) Wizara ilishiriki kwenye Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa yaliyofanyika mkoani Dodoma kuanzia tarehe 05 hadi10 Desemba, 2023. Maadhimisho hayo yalifanyika kuanzia tarehe 5 hadi 9 Desemba, 2023 ambapo wananchi **113** (Wanaume **77**, Wanawake, **24** na Watoto **12**) walipatiwa elimu kuhusu haki za binadamu na watu, unyanyasaji wa kijinsia, migogoro ya ardhi, migogoro ya ndoa na masuala ya mirathi.

(iv) Wizara ilitoa elimu kuhusu haki za binadamu kwa umma kwa jumla ya wananchi **107** (Wanawake **68** na Wanaume **39)** katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 11 Machi, 2024 mkoani Dodoma.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha Julai, 2023

hadi Aprili, 2024 THBUB ilikuwa inachunguza jumla ya malalamiko **964,** katika kipindi hicho malalamiko **141** yalifungwa. Aidha, malalamiko **823** yanayoendelea na uchunguzi ambapo kati ya hayo malalamiko **336** yanahusu uvunjwaji wa haki za binadamu, malalamiko **450** yanahusu ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na malalamiko **37** yanahusu makundi maalum.

47. ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara kupita THBUB imeendelea kutoa Elimu kwa Umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Jumla ya vipeperushi **3,110** vilitolewa kwa wananchi waliotembelea katika Ofisi za Tume, maadhimisho ya Wiki ya Wakulima, Wiki ya Sheria na Semina za Viongozi wa Vilabu vya haki za binadamu. Aidha, vipindi **21** viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia redio na televisheni. Pia, matamko manne (**4**) kuhusu haki za binadamu yalitolewa, matamko hayo yalihusu:-

(i) Usafirishaji haramu wa binadamu duniani, tamko hilo lilitolewa tarehe 30 Julai, 2023 wakati wa Siku ya Kimataifa ya Kuelimisha Umma kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu duniani;

(ii) Kutambua mchango wa wanawake katika nyanja mbalimbali za maendeleo, tamko hilo lilitolewa tarehe 31 Julai, 2023 wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke wa Afrika;

(iii) Viashiria vya uvunjifu wa amani na umoja wa kitaifa wakati wa mjadala kuhusu uwekezaji wa Kampuni ya *DP World* nchini; na

(iv) Watu wenye ulemavu na masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, tamko hilo lilitolewa tarehe 03 Desemba, 2023 wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu.

48. ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia THBUB ilifanya kikao kazi pamoja na wadau **53** kutoka Asasi za Kiraia (AZAKI) na taasisi za Serikali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la kikao hicho lilikuwa kupata maoni kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Maputo pamoja na kuangalia jinsi Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali nchini ilivyoangaza utekelezaji wa Itifaki ya Maputo ya mwaka 2003. Majadiliano kuhusu Itifaki hiyo yalijikita katika hoja ya iwapo kuna hajaya nchi yetu kuwa na Sheria Mahsusi inayohusu itifaki hii, ambayo nchi iliiridhia mwaka 2007 au sheria zilizopo zinajitosheleza. Tume inaendelea na uchambuzi ili ishauri ipasavyo kuhusu suala hili.

49. ***Mheshimiwa Spika**,* Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa Kanda ya Afrika Mashariki, ilifanya semina moja **(1)** ya mafunzo ya haki za binadamu kwa viongozi wa vilabu vya haki za binadamu na walezi wake kutoka vyuo vikuu na vyuo vya kati ambapo jumla washiriki **70** walijengewa uwezo kuhusu masuala ya haki za binadamu na wajibu.

50. ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara kupitia THBUB ilifanya makongamano mawili **(2)** kwa kushirikiana na Taasisi za elimu na wadau wa Haki za Binadamu ikiwemo Chuo Kikuu cha Iringa ambapo jumla ya wanachuo **300** na wakufunzi watatu **(3)** walishiriki. Kupitia makongamano hayo, wanachama wapya **178** walijiunga na Klabu ya Haki ya Binadamu na Utawala bora. Aidha, kongamano la pili lilifanyika na Wadau wa Haki za Binadamu katika kuadhimisha Miaka **75** ya Tangazo la Dunia kuhusu Haki za Binadamu. Kupitia Kongamano hilo, jumla ya washiriki **105**, walijengewa uelewa katika masuala mbalimbali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

51. ***Mheshimiwa Spika**,* katika kipindi husika, Wizara kupitia THBUB, ilifanya ufuatiliaji wa ufanisi wa taratibu za kushughulikia malalamiko katika taasisi za Serikali za utoaji haki zisizo za kimahakama katika Mikoa ya Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Unguja. Taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Ofisi ya Kazi Mkoa, Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania na Mifuko ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Kupitia tathimini

hiyo, Tume iligundua kuwa taasisi za Serikali za utoaji haki zisizo za kimahakama zinakabiliwa na uhaba wa rasilimaliwatu na fedha, wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya huduma na majukumu ya taasisi hizo, na baadhi ya taasisi kuwa na Ofisi katika ngazi za mikoa tu. Tume ilizishauri taasisi hizo kubainisha mahitaji na kuwasilisha katika mamlaka husika maombi ya kuongezewa rasilimaliwatu na fedha ili ziwe na ufanisi katika kuhudumia wananchi.

***(h) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati***

**(i) Usikilizaji wa Mashauri**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 kulikuwa na jumla ya mashauri **196,592** mahakamani; kati ya hayo **52,056** ni mashauri yaliyokuwepo mwanzoni mwa Julai, 2023 na mashauri **144,536** yalifunguliwa. Kati ya mashauri **196,592** yaliyokuwepo, mashauri **133,823** yalisikilizwa na kuhitimishwa na mashauri **62,769** yanaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, mashauri yenye umri mrefu Mahakamani ni **2,087** sawa na asilimia **3** ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani. Aidha, katika mashauri yaliyopo Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani umri mrefu ni miaka miwili (**2)**; Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya umri mrefu ni mwaka mmoja (**1)**; Mahakama za Mwanzo umri mrefu ni miezi sita (**6**)**.**

**(ii) Kuendelea Kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika Ngazi Mbalimbali**

53. ***Mheshimiwa Spika***, Mahakama ya Tanzania imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026). Hadi kufikia Aprili 2024, Miradi iliyokamilika ni Mahakama za Wilaya ya Ulanga, Kwimba na Liwale; Ukarabati wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Maswa: Ujenzi wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo Usevya (Mlele),

Nyakibimbili (Bukoba), Mahenge (Kilolo), Newala Mjini (Newala), Madale (DSM), Kinesi (Rorya) na Luilo (Ludewa).

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia Aprili, 2024 hali ya ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali ya Mahakama ni kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki sita (**6**) ambavyo ni Katavi Songea (Ruvuma), Songwe Njombe, Simiyu na Geita;

(ii) Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo tatu (**3**) ambazo ni Mahakama ya Mwanzo: Ilangala (Ukerewe), Mbalizi (Mbeya) na Machame (Kilimanjaro);

(iii) Kuendelea kwa ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya sita (**6**) ambazo ni Mahakama ya Wilaya; Kibiti (Pwani), Nachingwea (Lindi), Simanjiro (Manyara), Hanang (Manyara), Mbulu (Manyara) na Tunduru (Ruvuma);

(iv) Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia **61**:

(v) Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya Ubungo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia **98**;

(vi) Ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma ambapo ukarabati umefikia asilimia **49;**

(vii) Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ambapo hadi sasa umefikia asilimia **97.3**;

(viii) Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo KabangaNgara unaendelea na upo asilimia **97** katika hatua ya ukamilishaji (*finishing stage)*;

(ix) Ujenzi wa nyumba **48** za Majaji eneo la Iyumbu Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia **98** kwa Majengo yote; na

(x) Kuendelea kwa ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu, jijini Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia **53**.

### (iii) Mifumo ya TEHAMA katika Huduma za Mahakama

55. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 maboresho ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Mahakama yameendelea kwa lengo la kuimarisha upatikanaji haki kwa wananchi. Hadi kufikia Aprili, 2024 Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri umeboreshwa. Mifumo ya *e-project management, e-library, ewakili, e-court broker, process server na Judicial portal* imefuatiliwa na kufanyiwa maboresho. Aidha, matumizi ya TEHAMA yameimarika katika utoaji haki ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Unukuzi na Tafsiri (*Transcription and Translation System-TTS*); *e-case management;* na *virtual conference*.

### *(i) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro*

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali imesajili jumla ya watoa huduma **46** walioomba kuthibitishwa kama Watoa Huduma za Utatuzi wa Migogoro kwa njia mbadala, ambapo Waendesha Maridhiano **3**, Watoa Huduma za Majadiliano **3**, Wapatanishi **13** na Wasuluhishi **27**. Hivyo, hadi aprili, 2024 wapo Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala **576**, kati ya hao, Waendesha Maridhiano **38**, Watoa Huduma za Majadiliano **60**, Wapatanishi **185** na Wasuluhishi **293.**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na taratibu za kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania (*Tanzania International Arbitration Centre*), hadi kufikia Aprili, 2024 Andiko la Kuanzisha Kituo hicho limeandaliwa ikiwa ni pamoja na kuainisha mapendekezo ya muundo wa taasisi; gharama za kuanzisha na kuendesha taasisi; mifumo ya ushirikiano na taasisi nyingine zinazohusiana na masuala ya usuluhishi Tanzania. Taasisi hiyo itakuwa na Kituo Dar es Salaam ambapo tayari jengo kwa ajili ya kuanzisha Kituo hicho limepatikana.

### *(j) Kuimarisha Mfumo wa Elimu ya Sheria*

**Taasisi ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Taasisi Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (*Law School of Tanzania – LST*) ilisajili jumla ya wanafunzi **1,242** sawa na asilimia **82.8** ya lengo la udahili wa wanafunzi **1,500** kwa kundi la 37 na 38. Aidha, katika kipindi husika, Taasisi imetoa wahitimu **272** wanaostahili kusajiliwa kuwa Mawakili na kufanya idadi ya wahitimu waliopata mafunzo kupitia Taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia **8,717**. Vilevile, Taasisi ilipata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na kuanzisha programu ya mafunzo ya watoa huduma ya msaada wa kisheria ngazi ya cheti. Aidha, wahitimu **15** waliofanya mitihani ya Astashahada ya Wasaidizi wa Sheria walifaulu na kutunukiwa Astashahada ya Wasaidizi wa Sheria.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Wasajili Wasaidizi wa Msaada wa Kisheria imetoa huduma ya msaada wa kisheria kwa watu **7,270** wakiwemo wanaume **3,810** na wanawake **3,460** sawa na asilimia **52.41** na asilimia **47.59** mtawalia. Katika idadi hiyo, watu wazima walikuwa **7,071** (**97.26**%) na watoto walikuwa **199** (**2.74**%). Maeneo yaliyopatiwa msaada wa Kisheria ni Migogoro ya ndoa **1,694,** ardhi **1,663,** Madai **1,621,** Mirathi **796,** Jinai **683,** Masuala ya Biashara **241** na Migogoro mingine mchanganyiko **572**. Aidha, Taasisi itaendelea kuboresha na kuimarisha usimamizi wa wanafunzi wakati wa mafunzo uwandani ili wananchi wengi hususan katika maeneo ya pembezoni waweze kupata msaada wa kisheria.

***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania, wananchi **195** (Wanawake **81** na Wanaume **114**) wamepatiwa msaada wa kisheria na elimu ya sheria imetolewa kwa wadau **700** wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. LST kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imefanya mapitio ya mtaala wa mafunzo ya uanasheria

kwa vitendo ambao utaanza kutumika rasmi Julai, 2024. Mapitio hayo yana lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo na kuwajengea wanafunzi umahiri kulingana na mahitaji ya sasa ya soko. Mapitio hayo yamefanyika kwa dhana ya mabadiliko kwa kuzingatia maendeleo katika jamii.

**Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto**

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (*Institute of Judicial Administration – IJA*) kimedahili jumla ya wanafunzi **958** wa Astashahada na Stashahada ya Sheria ambayo ni sawa na **73.7**% ya lengo la udahili wa wanafunzi **1,300.** Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi **608** walihitimu mafunzo ya ngazi ya Astahashada na Stashahada ya Sheria.

61. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha watumishi wa Mahakama na watumishi wengine wa Sekta ya Sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha katika kutimiza wajibu wao wa utoaji haki kwa ufanisi, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (*Institute of Judicial Administration – IJA*) imeendelea kutoa mafunzo endelevu na elekezi kwa watumishi wa Mahakama na wadau wa Sekta ya Sheria nchini. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, Chuo kimeendelea kutekeleza jukumu lake la kuratibu mafunzo elekezi kwa Majaji wapya saba **(7)** wa Mahakama ya Rufani na **20** wa Mahakama Kuu pamoja Mahakimu wapya **39** kupitia Mahakama ya Tanzania.

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, IJA imeratibu mafunzo endelevu kwa maafisa **274** wa Mahakama yakiwemo ya kubadilishana uzoefu juu ya uhalifu wa mtandaoni pamoja na uhalifu wa kifedha**;** mafunzo ya utekelezaji wa amri za fidia, faini na gharama katika mashauri ya jinai kwa Maafisa Mahakama **147;** mafunzo ya kubadilishana uzoefu katika kushughulikia mashauri ya ndoa kwa Maafisa Mahakama **104;** mafunzo ya namna ya kushughulikia utekelezaji wa wosia na usimamizi wa mirathi kwa Maafisa Mahakama **104;** mafunzo ya kubadilishana uzoefu katika kushughulikia mashauri

ya uchaguzi kwa Maafisa Mahakama **132;** mafunzo ya programu ya ushauri maalum wa kitaaluma kwa Maafisa Mahakama **40;** Mafunzo ya wakufunzi ya namna ya kuepusha kurejesha majeraha ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto kwa Maafisa Mahakama **11** na mafunzo kwa njia ya mtandao kwa Mahakimu **100** wenye mamlaka ya ziada; na mfumo wa usimamizi wa mashauri na ujuzi wa uongozi kwa Maafisa Mahakama **398**.

63. ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2023/2024, IJA imetoa mafunzo mbalimbali kwa wadau wa mnyororo wa utoaji haki yakiwemo ya Madalali na Wasambaza Nyaraka za Mahakama **70;** maandalizi na matumizi ya jukwaa la kufundishia kwa njia ya mtandao kwa Watumishi **37** wa Mahakama; mafunzo ya namna bora ya kushughulikia mashauri ya wanyamapori na makosa yanayofanana na hayo kwa Mahakimu, Wapelelezi na Waendesha Mashtaka **331;** mafunzo ya kuandaa, kutengeneza na kutumia maudhui ya kwenye mtandao kwa ajili ya kufundishia na kujifunza kwa Watumishi **19** wa Mahakama; mafunzo ya namna bora ya kushughulikia mashauri ya watoto kwa Makarani **27** wa Mahakama**;** na mafunzo ya ujuzi wa kompyuta (*computer literacy*) na stadi za msingi/awali za kidigiti (*Basic Digital Skills*) kwa Waandishi Waendesha Ofisi na Wasaidizi wa Kumbukumbu **1,785.**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, IJA ilishiriki katika matukio mbalimbali kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo; kikao cha 6 cha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu juu ya majadiliano kuhusu haki za binadamu kilichofanyika nchini Algeria; mdahalo wa makosa ya uhalifu wa Kupangwa wa Kimataifa Unaovuka Mipaka, uliofanyika Jijini Dodoma; kikao cha majadiliano juu ya Masuala ya Rushwa na Uhuru wa Mahakama yaliyofanyika katika Jiji la Prague nchini Czech; Kongamano la Majaji wa eneo la Bahari ya Hindi kuhusu Uhalifu wa Baharini nchini Shelisheli (Sychelles); Mafunzo ya mtandao juu ya Sheria ya Wakimbizi ambayo yaliandaliwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kimahakama (JIFA). Pia, IJA iliandaa Kongamano (*Symposium*) la Maafisa wa Mahakama na wadau wengine lililohusu makosa ya uhalifu wa kifedha kwa udhamini

wa Programu ya Kitaifa ya Kuzijengea Uwezo Taasisi za Umma zinazohusika na Kupambana na Rushwa Tanzania.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya majukumu ya Chuo ya Uongozi wa Mahakama ni kuandaa majarida na machapisho yanayohusiana na Sekta ya Sheria au masuala ya kimahakama. Katika mwaka 2023/2024, IJA iliandika na kuzindua kitabu kinachoitwa Ndoto Iliyotimia: Maisha ya Jaji Robert Habesh Kisanga; na Kitabu cha Mkusanyiko wa Mashauri ya Ukatili wa Kingono kwa Watoto ya Tanzania na Ireland kwa ushirikiano na Taasisi ya *Irish Rule of Law International (IRLI);* Mwongozo wa Mafunzo ya Mashauri ya Watoto kwa Wasaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama kwa kushirikiana na UNICEF na kutoa chapisho la Utamaduni wa Mahakama.

***(k) Kuratibu mapitio na marekebisho ya sheria***

66. ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara imeendelea kuratibu mapitio na marekebisho ya Sheria mbalimbali. Lengo likiwa ni kuboresha ufanisi na kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Sheria. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa na kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali katika Sekta ya Sheria *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Ammendments) Bill No. 4 of 2023)*. Katika kipindi hicho Sheria **22** za Sekta ya Sheria zilifanyiwa marekebisho kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho Na.4**.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya mapitio ya mfumo wa sheria na tathmini ya utekelezaji wa Sheria kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria zinaakisi mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia. Tume imefanya mapitio ya mfumo wa sheria zinazosimamia makosa dhidi ya maadili kwa kufanya utafiti katika mikoa **18** ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Katavi, Kigoma, Tabora, Mwanza, Geita, Mara, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Taarifa ya utafiti imekamilika na kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji.

68. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Sanaa nchini inakua kwa kasi na kuajiri vijana wengi na kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuongeza Pato la Taifa, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutunga sheria ili kusimamia haki za kazi za Sanaa. Katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya tathmini ya Sheria zinazosimamia Hakimilki na Hakishiriki zikiwemo, Sheria ya Hakimilki na Hakishiriki, Sura ya 218; Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230; Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Sura ya 204; Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria ya Usimamizi wa Tozo na Ushuru, Sura ya 147 na Sheria ya Makosa Mtandaoni, Sura ya 443. Dhumuni la tathmini lililenga kupima kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yamefikiwa katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Sanaa inakua ya kibiashara na yenye tija kwa wasanii na Taifa kwa ujumla. Tathmini hiyo imehusisha wadau wanaosimamia utekelezaji wa Sheria za Hakimilki na Hakishiriki katika Mikoa mitano (***5***) ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Dodoma na Mwanza. Taarifa ya tathmini hiyo itawasilishwa serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imetekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia namna ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai kwa kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia dhamana ikiwemo Sheria zilizofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Kudhibiti Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200; Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi, Sura ya 446; Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11; Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95; Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141; Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 322. Aidha, Tume imefanya mapitio ya Sheria za Adhabu ya Viboko na tathmini ya utekelezaji wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 hususan Kifungu 91(1) kinachohusiana na uondoshaji mashauri mahakamani (*nolle proseque*) pamoja na tathmini ya Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mfumo wa Haki Jinai nchini, Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa ili kubaini upungufu uliopo na kupendekeza makosa yanayostahili kuwa ya uhujumu uchumi na makosa yasiyostahili kuwa ya uhujumu uchumi.Utafiti huo umefanyika katika Mikoa Sita (**6**) ya Dodoma, Dar Es Salaam, Arusha, Manyara, Mara na Mwanza.

***(l) Kuandaa Sera Mahsusi Zinazosimamia Mifumo ya Utoaji Haki***

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa sera na sheria zinaandaliwa ili kuimarisha upatikanaji haki na kutoa mchango kwa maendeleo ya Taifa, Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai. Sera hiyo itajumuisha masuala mbalimbali katika mnyororo wa haki jinai ikiwemo utoaji taarifa za matukio ya uhalifu; ushahidi; uchunguzi wa uhalifu; ufunguaji wa hati za mashtaka; uendeshaji wa mashtaka; utoaji wa hukumu; usimamizi wa wafungwa magerezani; na urejeshwaji wa wafungwa uraiani baada ya kumaliza kifungo au kupata msamaha wa adhabu ya kifungo.

***(m) Kuendelea Kuimarisha Mfumo wa Uangalizi wa Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi***

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara ilitoa mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu masuala ya uangalizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi kwa Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi, wanaohusika na uangalizi na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi na uwajibikaji katika ulinzi na matumizi ya utajiri asili na maliasilia za nchi, usimamizi wa mikataba, na itifaki baina ya Tanzania na nchi nyingine kwa kuzingatia Sheria za Uangalizi wa Utajiri Asili na Maliasilia za nchi Sura ya 449 na 450.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kushiriki katika majukumu ya kupitia mikataba mbalimbali inayohusu uwekezaji kwenye utajiri asili na maliasilia za nchi baina ya Tanzania na nchi nyingine ambapo katika kipindi cha mwezi April, 2024 Wizara

kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepitia mikataba ya uwekezaji **18** kwa lengo la kubaini iwapo inakidhi mahitaji ya sasa ya kiuchumi na kijamii. Vilevile, katika kipindi tajwa Wizara imeandaa na kusambaza Rasimu ya Mwongozo wa Usajili wa Mikataba ya Utajiri asili na Maliasilia za nchi katika sekta zinazohusika na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa uzingatiwaji wa Sheria tajwa ambapo mikataba mitano (**5**) inayohusu uwekezaji katika madini na fukwe za bahari imesajiliwa.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi April,2024 Wizara imepokea taarifa kutoka sekta **10** zinazosimamia masuala ya utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo zimetoa taarifa ya namna ambavyo Sheria na Sera za sekta husika zilivyozingatia misingi ya Sheria za Uangalizi wa utajiri asili na Maliasilia za nchi ambayo ni Mamlaka ya nchi ya kudhibiti na kumiliki utajiri asili na maliasilia za nchi; uvunaji na matumizi endelevu ya utajiri asili na maliasilia kwa vizazi vya sasa na vijavyo; Msingi wa wananchi kunufaika na utajiri asili na maliasili; Misingi ya ushirikishwaji wa wananchi katika matumizi na uvunaji wa utajiri asili na maliasilia; pamoja na msingi wa mgawanyo wa mapato na uwazi katika mikataba ya utajiri asili na maliasilia. katika kipindi husika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Madini pamoja na Shirika la Maendeleo la Taifa ilitembelea mradi wa Liganga na Mchuchuma uliopo Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe. Ziara hiyo, ililenga kutembelea eneo la mradi kuonana na wananchi wanaozunguka eneo hilo ili kutambua afua zinazoweza kuwasaidia wananchi kiuchumi pindi mradi huo utakapoanza kwa kuzingatia Sheria za Utajiri asili na maliasilia za nchi, kusikiliza kero za wananchi wa eneo la mradi na kubaini changamoto mbalimbali za kisheria zinazokwamisha utekelezaji wa mradi huo.

### *(n) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria nchini*

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mfumo wa utoaji haki, Wizara imetoa vifaa vya TEHAMA kwa taasisi za haki jinai ambavyo ni:

(i) Seti 24 za ***Video Conference*** kwa ajili ya kuendesha mashauri kwa njia ya mtandao kwa Mahakama ya Tanzania ambazo zitafungwa kwenye Mahakama 24 za Mikoa; na

(ii) Jumla ya Kompyuta za mezani tano (**5**), Kompyuta mpakato **86,** printa **13** na televisheni moja (**1**) zimetolewa kwa ajili ya magereza ya Njombe, Ludewa na Msalato; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na Taasisi ya Afya ya Akili ya Mirembe sehemu ya Isanga ili kuimarisha huduma za TEHAMA katika utoaji haki.

76. ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja (*Contact Centre*) kwa ajili ya kupokea malalamiko, taarifa na maoni kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali wa utoaji haki. Lengo la kuanzishwa kituo hiki ni pamoja na kuhakikisha wananchi wanaondolewa adha ya kusafiri umbali mrefu na gharama kubwa kufuatilia haki zao. Kituo hiki kimeanza kutumika tangu Februari, 2024 kupitia namba **0262160360** na tayari kituo kimepokea malalamiko **24** ambapo hadi Aprili, 2024 malalamiko hayo yamefanyiwa kazi.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) imeendelea kusogeza na kuimarisha utoaji wa huduma kwa mwananchi kupitia TEHAMA. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 huduma za usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Bodi za Wadhamini zimewezeshwa kupatikana kidijitali (eRITA) na mwananchi anaweza kutuma maombi popote alipo bila kufika ofisi za Wakala na kuchagua Ofisi ya Wilaya iliyokaribu kwa ajili ya kupata huduma ya cheti cha kuzaliwa, kifo, ndoa, talaka, leseni ya kufungisha ndoa na cheti cha usajili wa Bodi ya Wadhamini.

78. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi husika Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) imeunganisha na kuwezesha kubadilishana taarifa ya mifumo yake na Taasisi tisa **(9)** za Serikali ambazo ni: - Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, Mahakama Kuu ya Tanzania, Wizara ya Katiba na Sheria, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Bodi ya

mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Vilevile, katika kuhakikisha matukio ya vizazi na vifo yanasajiliwa kwa wakati, Wakala imeunganisha mfumo wa usajili wa vizazi na vifo na mfumo wa" GoTHoMIS" unaosimamiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Mfumo wa DHIS2 wa Wizara ya Afya ili kuwezesha kupatikana taarifa za matukio ya vizazi na vifo pindi yanapotokea. Vilevile, taarifa za huduma zinazotolewa na Wakala zinapatikana kidijitali kupitia Basi Mtandao la Serikali (GovESB). Aidha, Wakala inatarajia hadi kufikia Desemba, 2024 iwe imeunganisha wadau wote wanaohitaji na kutumia taarifa za RITA.

***(o) Kuendelea na Utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto 2020/2021-2024/2025***

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto kwa kufanya kikao cha tatu cha Jukwaa la Haki Mtoto, ambapo masuala mbalimbali kuhusu haki za mtoto yalijadiliwa, ikiwemo kuendelea na mpango wa kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji na upatikanaji haki kwa mtoto nchini. Vilevile, kuendelea kuratibu kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa mtoto kwa njia ya mitandao ikiwa na lengo la kuhakikisha mtoto anakuwa katika mazingira mazuri na salama, ikizingatiwa kuwa mtoto ni taifa la leo na kesho. Pia, katika kutekeleza Mkakati huu, Wizara imeendelea na mpango wa uratibu wa utoaji huduma za msaada wa kisheria hususan katika masuala ya ukatili dhidi ya mtoto nchini kwa kuwajengea uwezo watoto, Wasajili Wasaidizi, Wasaidizi wa Kisheria, Viongozi wa Serikali za Mitaa, Viongozi wa kidini na Kimila katika kushughulikia masuala yanayohusiana na ukatili dhidi ya mtoto. Vilevile, Jukwaa hili limeweka mkakati wa kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto wanaokinzana na sheria kwa kuwapatia Mawakili wa kuwawakilisha katika mashauri yaliyo mahakamani.

***(p) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya***

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya kwa kutoa Mafunzo elekezi juu ya Kanuni za Maadili za Maafisa Mahakama na Kanuni Mpya za Uendeshaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama wa Wilaya na Mikoa. Katika kipindi husika, jumla ya wajumbe **91** kutoka Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama wa Wilaya na Mkoa kwa Mikoa ya Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Tanga, Katavi na Rukwa walijengewa uwezo kuhusu uendeshaji wa kamati za Mikoa na Wilaya.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilifanya ziara katika Mikoa ya Kagera, Geita na Morogoro. Lengo la ziara hiyo ni kujitangaza kwa wananchi na watumishi wa Mahakama ili wajue Sheria iliyounda Tume, Muundo, Mamlaka pamoja na majukumu ya Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya. Aidha, Tume ilitoa elimu kwa Umma katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Januari, 2024 jijini Dodoma ambapo jumla ya washiriki **81** walipata elimu.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama ngazi za Mikoa na Wilaya, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilifanya ziara kwenye Mikoa minne (**4**) ya Dodoma, Singida, Shinyanga na Simiyu. Lengo la ziara hiyo ni kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama pamoja na elimu kwa umma kuhusu uwepo wa Kamati hizi. Aidha, watendaji wa Tume walifanya ukaguzi kwenye mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu na Mara kwa Lengo la kuangalia namna Kamati zinavyotekeleza majukumu yake pamoja na kupokea maoni ya kuboresha utendaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa Mahakama.

### *(q) Kufanya Tafsiri, Uandishi, Uhakiki wa Mikataba na Urekebu wa sheria*

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji haki na utawala bora, Serikali kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Sekta ya Sheria, Namba 11/2023 ilifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuanzisha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Lengo la maboresho haya ni kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za uandishi wa sheria, urekebu na ufasiri wa sheria. Maboresho haya pia, yanalenga kuhakikisha upatikanaji wa sheria, kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu sheria, na hivyo kuiwezesha nchi kutekeleza mipango ya maendeleo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwandishi Mkuu wa Sheria inaendelea kukamilisha taratibu za kiutawala ili kuwezesha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi Sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi iliandaa Miswada **14**. Miswada iliyoandaliwa ni kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na.5**. Aidha, Miswada ya Sheria **15** ilijadiliwa na kupitishwa kuwa Sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hizo ni kama zilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na.6**.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilihakiki na kuchapisha jumla ya Sheria Ndogo **885**, ikilinganishwa na Sheria Ndogo **631** zilizohakikiwa na kuchapishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia **40**. Sheria hizo zinajumuisha Kanuni **138**, Amri **420**, Notisi **323** na Matamko manne **(4)**. Orodha ya Sheria Ndogo zilizoandaliwa kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 zinaonekana kwenye **Kiambatisho Na.7**. Lengo la kutengenezwa kwa sheria ndogo ni kufafanua kwa kina na kwa undani maudhui yaliyobainishwa kwenye Sheria Kuu.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya Sheria Kuu **74** zimefanyiwa ufasiri kwa awamu ya pili. Sheria hizo zinasubiri kufanyiwa uhakiki wa mwisho na kuchapishwa kati Gazeti la Serikali **(Kiambatisho Na.8).**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha urekebu wa Sheria Kuu **446** kwa lengo la kutoa toleo la urekebu la Sheria Kuu la mwaka 2023 (*Revised Edition 2023*). Toleo hili lipo katika hatua za mwisho za uchapishaji na utengenezaji wa Juzuu linalotarajiwa kuzinduliwa Juni, 2024.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya Mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa **1,280** kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na Mikataba **1,171** iliyofanyiwa upekuzi katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 sawa ongezeko la asilimia **9**. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya Miradi ya Serikali na miradi inayofadhiliwa na Wadau wa Maendeleo. Aidha, Hati za Makubaliano **341** zilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na idadi ya Hati za Makubaliano **295** zilizofanyiwa upekuzi katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023. Ongezeko hili linaakisi jitihada za Serikali kuhamasisha uwekezaji na diplomasia ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

89. ***Mheshimiwa Spika****,* kati ya Mikataba **1,280** iliyofanyiwa upekuzi, Mikataba **458** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali katika mchanganuo ufuatao: Mikataba **351** ilikuwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania **trilioni 10.52**; Mikataba **92** ilikuwa na thamani ya **Dola za Marekani bilioni 2.30** sawa na **Shilingi za Kitanzania trilioni 5.40**; na Mikataba **15** ilikuwa na thamani ya Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) **360,577,992.11** sawa na Shilingi za Kitanzania **trilioni 1.002**. Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali Kuu, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na kwa wananchi. Lengo ni kuhakikisha Serikali na Taasisi zake zinapata faida kutokana na utekelezaji wa majukumu yake na hivyo, kuikinga Serikali kuingia katika kesi mbalimbali kwa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya maombi ya ushauri wa kisheria **1,707** yalipokelewa na kufanyiwa kazi ikilinganishwa na maombi **812** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia **110.** Kati ya maombi **1,707**, maombi **390** yalihusu malalamiko ya watu binafsi na maombi **1,317** yanatoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

***(r) Kuendesha Mashtaka ya Jinai***

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai **27,205** ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ikilinganishwa na kesi **32,609,** zilizoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023. Aidha, jumla ya kesi **16,928** sawa na asilimia **62** zilihitimishwa ikilinganishwa na kesi **18,485** sawa na asilimia **57** ya kesi zilizohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023. Kati ya kesi zilizohitimishwa, **10,444** zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani ikilinganishwa na kesi **10,392** zilizohitimishwa kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi **680** katika Mahakama za watoto (*Juvenile Courts*) ambapo kesi **454** zilihitimishwa sawa na asilimia **67.**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi **6,649** katika Mahakama Kuu ya Tanzania ikilinganishwa na kesi **6,425** zilizoendeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, kesi **2,408** zilihitimishwa sawa na asilimia **36** ikilinganishwa na kesi **2,629** zilizohitimishwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na asilimia **41** ya kesi zilizoendeshwa.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya kesi **2,905** za jinai katika Mahakama ya Rufani ikilinganishwa na kesi **1,535** zilizoendeshwa kipindi kama hicho katika mwaka 2022/23. Kati ya kesi hizo, kesi **414** zilihitimishwa sawa na asilimia **14** ya kesi zilizokuwa zikiendeshwa ikilinganishwa na kesi **267** zilizohitimishwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na asilimia **17** ya kesi zilizokuwa zikiendeshwa.

95. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 hadi Aprili, 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi kubwa **64** katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ikilinganishwa na kesi **90** zilizoendeshwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, kesi **24** zilihitimishwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na kesi **40** zinaendelea katika hatua mbalimbali.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea kukagua magereza na vituo vya polisi nchini kwa lengo la kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki ya kutatua changamoto hizo kwa mujibu wa sheria. Katika mwaka 2023/2024, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya magereza **107** yalikaguliwa ikilinganishwa na magereza **63** yaliyokaguliwa kipindi kama hicho katika mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la magereza **44**. Pia, ukaguzi umefanyika katika vituo vya Polisi **251** ikilinganishwa na vituo **140** vilivyokaguliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la vituo **111**. Katika ukaguzi huo jumla ya mahabusi **1,250** waliachiwa ikilinganishwa na mahabusi **333** walioachiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la mahabusi **917** (**Kiambatisho Na.9).**

### *(s) Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Upelelezi wa Makosa ya Jinai*

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 hadi Aprili, 2024 OTM ilishughulikia jumla ya majalada **16,854** kutoka vyombo vya upelelezi ikilinganishwa na majalada **12,535** yaliyoshughulikiwa katika kipindi kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Kati ya majalada hayo, majalada **11,255** yaliandaliwa hati za mashtaka sawa na asilimia **67** ya majalada yaliyoshughulikiwa ikilinganishwa na majalada **6,349** yaliandaliwa hati za mashtaka katika mwaka 2022/2023 sawa na asilimia **51** ya majalada yaliyoshughulikiwa.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya majalada **16,854** yaliyopokelewa, majalada **1,138** yalifungwa ikilinganishwa na majalada **658** yaliyofungwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 na majalada **3,439** yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi ikilinganishwa na majalada **2,856** yaliyorejeshwa kwa upelelezi zaidi katika kipindi kama hicho katika mwaka 2022/2023. Hivyo, kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 kuwa **15,832** sawa na asilimia **94** ya majalada yaliyopokelewa ikilinganishwa na **9,863** sawa na asilimia **79** ya majalada yaliyofanyiwa kazi kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023. Vilevile, majalada **1,022** yalikuwa yanaendelea kufanyiwa kazi kote nchini, sawa na asilimia **6** ya majalada yote yaliyopokelewa ikilinganishwa na majalada **2,672** sawa na asilimia **21** yaliyokuwa yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kubuni mikakati ya kupunguza mlundikano wa mahabusi na wafungwa magerezani na kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi kwa kuhimiza matumizi ya adhabu mbadala. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara kupitia Mahakama imetoa Waraka wa Mhe. Jaji Kiongozi Na 4/2019 unaosisitiza maafisa wa Mahakama kutoa kipaumbele katika adhabu mbadala ya kifungo cha nje; Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.1 ya Mwaka 2022 (*The Written Laws- Miscellaneous Ammendments Act No. 1 of 2022*) imetungwa ambayo ilifanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20,

kwa kuweka Kifungu kipya cha 131A kinachoweka sharti la Mwendesha Mashtaka kufungua Kesi mahakamani mara tu baada ya kukamilisha shughuli za upelelezi ili kuepusha watuhumiwa kuwekwa vizuizini wakati kazi ya upelelezi ikiwa inaendelea.

***(t) Kushughulikia Urejeshwaji wa Wahalifu na Masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Makosa ya Jinai***

100. ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kusimamia kurejeshwa kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya makosa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imepitia mikataba ya urejeshwaji wa wahalifu watoro kutoka nchi mbalimbali na kujadili namna bora ya kuboresha mikataba husika. Katika kipindi hicho, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi nane (**8**) kutoka nchi zifuatazo Uturuki (**4**), India (**1**), Afrika Kusini (**2**) na Kenya (**1**). Aidha, Tanzania imetuma jumla ya maombi saba (**7**) ya kuomba wahalifu katika nchi ya Kenya (**2**), Afrika Kusini (**1**), Saudi Arabia (**1**), India (**1**), Uganda (**1**) na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (**1**).

***(u) Kuwaachilia Huru Wagonjwa wa Afya ya akili walio chini ya uangalizi wa Taasisi ya Afya ya Akili Isanga***

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuthibitika kuwa wagonjwa hao walitenda makosa wakiwa na ugonjwa wa afya ya akili, Mahakama haikuwatia hatiani na hivyo kuamuru wawe chini ya uangalizi wa Taasisi ya Afya ya Akili Isanga Dodoma kuendelea na matibabu wakisubiri amri ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 219 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Hivyo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya maombi **14** yaliwasilishwa Wizarani ambapo Amri ya kuwaachilia wagonjwa hao wa afya ya akili imetolewa.

### *(v) Kuimarisha Utekelezaji wa Programu ya Kutenganisha Shughuli za Mashtaka na Upelelezi*

102. ***Mheshimiwa Spika**,* OTM imeendelea kutekeleza mpango wa kutenganisha shughuli za mashtaka na upelelezi kwa kuendelea kuongeza idadi ya Mawakili wa Serikali na kuendelea kutoa vibali vya kuendesha mashtaka kwa Waendesha Mashtaka kutoka Ofisi na Taasisi mbalimbali. Lengo la mpango huu ni kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, OTM ilihuisha Kanzidata ya Waendesha Mashtaka waliopewa kibali cha kuendesha mashtaka na Mkurugenzi wa Mashtaka na Daftari la Mawakili wa Serikali. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina jumla ya Mawakili **663** pamoja na Waendesha Mashtaka waliopewa kibali na Mkurugenzi wa Mashtaka wapatao **1,095** nchi nzima. Pia, jumla ya wataalam **233** wanaohusika na upelelezi katika maeneo ya maandishi, picha, alama za vidole na milipuko wametangazwa katika Gazeti la Serikali.

103. ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Ofisi inaendelea kutoa huduma za kimashtaka katika mikoa **30** ya Kimashtaka na Ofisi **92** za Wilaya.

### *Kushughulikia Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi*

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kuiwakilisha Serikali katika kuendesha mashauri mbalimbali ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri ya **Madai 7,813** (mashauri ya ndani ya nchi **7,798** na mashauri ya nje ya nchi **15**), kati ya hayo, mashauri **6,113** ni mwendelezo wa mashauri ya Mwaka wa Fedha **2022/2023** na mashauri **1,700** ni mashauri yaliyofunguliwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024. Katika kipindi hicho, mashauri **762** yalimalizika, yakijumuisha, mashauri ya ndani ya nchi **750** na mashauri

ya nje ya nchi **12**. Aidha, kati ya mashauri ya madai yaliyomalizika, mashauri **719** yalihitimishwa Mahakamani na mashauri **43** yalihitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya mahakama.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishinda jumla ya mashauri **705** yenye madai ya fedha na kufanikiwa kuokoa fedha za Serikali jumla ya Shilingi **396,202,611,667.70.** Vilevile Ofisi imeokoa jumla ya **Shilingi 10,205,263,509.43** zilizotokana na mashauri **43** yaliyohitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama. Hivyo, kufanya kiasi kilichookolewa kwa kushinda kesi za Madai na kufanya majadiliano nje ya Mahakama kuwa jumla ya Shilingi **406,407,875,177.13**.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, hadi kufikia Aprili, 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imehitimisha mashauri ya madai yasiyohusisha fedha yakiwemo mashauri ya katiba, haki za binadamu, uwekezaji na biashara. Kwa mfano, Serikali imeshinda Shauri la kupinga kujengwa kwa mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki, shauri la kupinga Mkataba wa Uwekezaji katika Bandari ya Dar es salaam na Shauri la kupinga uwekezaji katika kiwanda cha Saruji cha Tanga.

108. ***Mheshimiwa Spika****,* kwa upande wa mashauri ya Usuluhishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi **179** kati ya mashauri hayo mashauri **148** ni ya ndani ya nchi na mashauri **31** ni ya nje ya nchi. Katika kipindi hiki, jumla ya mashauri **19** yalimalizika**,** ambapo mashauri **8** yalimalizika katika mabaraza/mahakama ya ndani ya nchi na mashauri **2** yalimalizika katika mabaraza nje ya nchi. Aidha mashauri **6** ya kitaifa na mashauri **3** ya kimataifa yalimalizika kwa njia ya majadiliano.

109. ***Mheshimiwa Spika****,* Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imewezesha Serikali kushinda katika mashauri matano (**5**) yaliyoendeshwa ndani ya nchi (Kitaifa) na kuokoa Shilingi **7,297,302,818.21** na shauri moja (**1**) la kimataifa na kuokoa Shilingi **818,285,700.00 (Milioni 818.28)** na Dola za Marekani **11,732,699.45** sawa na Shilingi 30,153,037,586.50 (Bilioni 30.15). Hivyo, Serikali imeokoa jumla ya Shilingi

**38,268,626,104.71 (Bilioni 38.26)** kutokana na kushinda mashauri hayo ya usuluhishi.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imehitimisha mashauri tisa **(9)** ya usuluhishi kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama, kati ya hayo mashauri sita **(6)** ni ya ndani ya nchi na mashauri matatu **(3)** ya nje ya nchi. Kupitia majadiliano haya, Serikali imeokoa Shilingi **47,510,903,758.35;** Dola za Marekani **60,322,799.82** (sawa na Shilingi 141,456,965,577.90) na Euro 487,982,230.66 (sawa na Shilingi 1,317,552,022,700.00 (Trilioni **1.3),** hivyo, Serikali imeokoa jumla ya Shilingi **1,506,519,892,036.25 (Trilioni 1.5).**

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kuendesha mashauri ya usuluhishi **160** katika vyombo na mabaraza mbalimbali ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

### *(w) Kuratibu Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Usimamizi wa Ufilisi na Udhamini*

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) imeendelea kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini kwa ajili ya mipango na maendeleo ya Taifa. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Aprili, 2024 RITA imesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa **1,520,899** pamoja na vyeti vya vifo **25,783**. Aidha, uhakiki umefanyika kwa vyeti vya kuzaliwa vya wanafunzi **130,493** na vyeti vya vifo **20,175** vya wazazi wa wanafunzi wanaoomba mkopo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

113. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini ilisajili jumla ya watoto **678,371** wenye umri chini ya miaka mitano katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Dar es Salaam. Aidha, Mradi huu umeendelea kutekelezwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, Halmashauri **184**, Kata **3,957** na Vituo vya Afya **7,304** na kufanya idadi ya watoto wa umri chini ya miaka mitano waliosajiliwa kupitia mpango huu kufikia **9,609,664** na kuweza kuongeza kiwango cha usajili katika kundi hili kutoka asilimia **13** mwaka 2012 hadi asilimia **68** mwaka 2024.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha usajili na utoaji wa vyeti kwa wakati kwa watoto wanaozaliwa, RITA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendela kutoa maelekezo kwa Mamlaka **184** za Serikali za Mitaa kuhakikisha watoto wanapozaliwa wanasajiliwa ikiwa ni sehemu ya haki ya mtoto. Pamoja na kuingiza taarifa hizo kwenye kanzidata ya RITA ili Serikali ipate takwimu za watoto waliozaliwa kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kulinda Maadili, Haki na Ukatili Dhidi ya Watoto, katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Aprili, 2024, RITA imesajili jumla ya hati **28** za kuasili watoto baada ya kupokea amri za Mahakama.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia RITA inaendelea na usajili wa matukio ya ndoa na talaka ambapo katika kipindi husika jumla ya marejesho **35,777** ya ndoa zilizofungwa na nakala za hukumu za talaka **798** zimesajiliwa.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia RITA imeendelea na jukumu la usimamizi na usajili wa bodi za wadhamini ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 RITA ilipokea jumla ya maombi ya huduma za bodi za wadhamini **1,112.** Kati ya maombi hayo **1,039** yalihitimishwa na **83** yanaendelea kufanyiwa kazi kama yalivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.10**. Vilevile, katika kuboresha utendaji wa bodi hizo, RITA imeandaa mwongozo wa Katiba ambayo inatakiwa kufuatwa na bodi zote za wadhamini zilizosajiliwa na zinazotarajiwa kusajiliwa RITA. Kupitia mwongozo huo migogoro ya bodi za wadhamini inayowasilishwa RITA itapungua kutokana na kuwepo kwa ibara inayohusu namna ya kusuluhisha migogoro hiyo pindi itakapojitokeza katika taasisi hizo.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara kupitia RITA imehudhuria mashauri **47** yaliyopo katika mahakama mbalimbali pamoja na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yanayohusu masuala ya mirathi na Bodi za Wadhamini zinazosimamiwa na Wakala. Jumla ya mashauri **25** yamemalizika hivyo

kuendelea na taratibu nyingine za ugawaji wa mali kwa wanufaika na mashauri **22** yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, RITA inasimamia jumla ya mirathi **90** ambapo mirathi saba **(7)** imefungwa baada ya kugawa mali kwa wanufaika na **83** zinaendelea kufanyiwa kazi.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala imeendelea kuimarisha upatikanaji haki kwa wakati kwa wananchi hususan katika masuala ya mirathi. Katika Mwaka wa Fedha, 2023/2024 hadi kufikia Aprili, 2024 RITA imeandika na kutunza wosia **118** na kuendelea kutoa elimu zaidi wa wanachi kuhusiana na faida za kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya mirathi inayojitokeza katika jamii. Aidha, Wizara kupitia RITA imetoa elimu kuhusu uandishi wa wosia na masuala ya mirathi kwa wananchi **29,826** kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia **14,156** (Wanawake **8,494** na Wanaume **5,662**); na makongamano na maonyesho ya Kitaifa ikiwemo ya Wiki ya Sheria, Nane Nane na Saba Saba **15,670** (wanawake **8,305** na wanaume **7,365**).

### *(x) Utekelezaji wa Masuala ya Kisheria katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa*

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria kikanda na kimataifa, Wizara imeshiriki mikutano miwili ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa kikao cha 46 cha nchi wanachama wa ESAAMLG kilichofanyika Kasane- Botswana Septemba, 2023 na Mkutano wa Bodi ya Uongozi ya (*United Nations African Institute for Prevention of Crime and the Treatment of Offenders - UNAFRI*), Addis Ababa, Ethiopia na Septemba 2023 Wizara ilishiriki katika warsha iliyoandaliwa na Sekretarieti ya Umoja wa Afrika iliyofanyika Cape Town Afrika Kusini Septemba, 2023 kujadili Itifaki ya Hali za Binadamu na Watu Kuhusiana Mtazamo Mahususi wa Haki ya Utaifa na Kuondoa Hali ya Kutokuwa na Utaifa Afrika (*Protocal to the Frican Charter on Human and Peoples' Rights Relating to the Specific Aspect of the Rights to a Nationality and Eradication of Statelessness in Africa*). Aidha, Desemba, 2023 Wizara ya Katiba na Sheria imesaini Hati ya Makubaliano na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Shirikisho la Urusi ili kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Sheria.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki katika mkutano wa Kamati Ndogo ya Umoja wa Kudhiti Fedha Haramu Duniani na Afrika na Mashariki ya Kati (FATF (ICRG-AMEJG) uliofanyika nchini Jordan. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano Maalum wa Nane wa Kamati ya Mawaziri wa Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 11 hadi 13 Desemba, 2023. Pia, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kawaida wa Tisa wa Kamati ya Mawaziri wa Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 14 hadi 16 Desemba, 2023. Vilevile, Wizara ilishiriki katika Mkutano Maalum wa Tisa wa Kamati ya Mawaziri wa Sheria na Haki ya Umoja wa Afrika uliofanyika Darban, Afrika ya Kusini tarehe 07 hadi 12 Februari, 2024. Ushiri wa Wizara katika mikutano hiyo umewezesha lugha ya Kiswahili kutumika rasmi katika vikao vya Kamati ya Mawaziri wa Umoja wa Afrika kuanzia tarehe 07 Februari, 2024.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki katika Mkutano wa 10 wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa (UNCAC) uliofanyika Atlanta, Marekani. Lengo la Mkutano lilikuwa ni kubadilishana uzoefu wa namna ya kupambana na uhalifu kwa nchi wanachama.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa nchi mwenyeji wa Kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika kikao hicho jumla ya wadau **1,860** wameshiriki. Baadhi ya manufaa kwa Tanzania kuwa nchi mwenyeji wa Kikao hiki ni pamoja na kuingiza fedha za kigeni takribani Dola za Marekani **7,000,000**. Katika kikao hiki, Serikali iliwasilisha taarifa kuhusu; upatikanaji wa haki ya elimu; uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa; kupinga ukali na ubaguzi dhidi ya wanawake; haki za watoto, wazee na watu wenye ulemavu; kuinua wanawake kiuchumi; kulinda mazingira; haki ya upatikanaji wa maji safi na salama; kupinga utesaji; kulinda wakimbizi; maendeleo ya vijana; na kuzingatia haki za binadamu wakati wa kutekeleza zoezi la

kuwahamisha wafugaji kutoka eneo la Ngorongoro kuhamia Kijiji cha Msomera, Handeni katika Mkoa wa Tanga.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola. Mkutano huo ulifanyika kuanzia tarehe 04 hadi 08 Machi, 2024 Unguja, Zanzibar. Aidha, Mkutano huo ulifunguliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jumla ya wageni **188** kutoka katika nchi **34** Wanachama wa Jumuiya ya Madola walishiriki. Yapo manufaa ambayo Tanzania imenufaika kwa kuwa nchi mwenyeji wa Kikao hiki ikiwemo kuingiza fedha za kigeni takribani Dola za Marekani **540,000**. Manufaa mengine ya Tanzania kuwa nchi mwenyeji wa mikutano ya kikanda na kimataifa katika Sekta ya Sheria ni pamoja na: -

(i) Kuongezeka sifa na heshima kwa Tanzania kidiplomasia na kuimarisha uhusiano wa kimataifa;

(ii) Tanzania kuendelea kuaminika na kuheshimika kimataifa katika kutambua na kuheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu; na

(iii) Kufahamika kwa vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania na hivyo kuongezeka kwa idadi ya watalii siku zijazo.

125. ***Mheshimiwa Spika**,* katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria katika ngazi za kikanda na kimataifa, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, ilishiriki katika Kongamano la *East African Legislative Summit on the Budapest Convention*. Kongamano hili lilifanyika Jijini Arusha ambapo washiriki walitokea katika nchi za Kenya, Malawi, Msumbiji na Tanzania. Kongamano hilo lilijadili Muundo wa Sheria za Makosa ya Kimtandao za Nchi za Afrika Mashariki na namna gani nchi hizo zinaweza kujiunga katika Mkataba wa Kimataifa wa Makosa ya Kimtandao (*Budapest Convention*).

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki kikao Kazi cha Ushirikiano wa Kimataifa kati ya "*Interpol*" na Maafisa wa Polisi kutoka nchini Thailand na Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai. Kikao hicho kilijadili ubadilishanaji wa taarifa kuhusu tuhuma za kusafirisha Kobe **116** kutoka Tanzania.

127. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeshiriki katika Mkutano wa 17 wa Wataalam wa Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa (UNCAC). Mkutano huu ulifanyika Vienna nchini Austria na kuwakutanisha pamoja maafisa viunganishi (focal persons) kutoka Nchi Wanachama. Lengo kuu la kikao hiki lilikuwa kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Urejeshwaji wa Mali zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu.

128. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipata fursa ya kushiriki Mkutano wa *Geiger Working Group* uliohusisha nchi kumi (**10**) ikiwemo Tanzania. Washiriki kutoka nchi Wanachama walijadili na kubadilishana uzoefu kuhusiana na namna ya kuzuia matumizi mabaya ya Mionzi na Nyuklia (Radiological and Nuclear Materials). Mkutano huo ulifanyikia tarehe 17 - 19 Oktoba, 2023, Zanzibar.

### *(y) Ujenzi wa Majengo ya Ofisi*

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekamilisha ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa ya Shinyanga, Manyara, Katavi na Rukwa. Vilevile, OTM inaendelea na ujenzi wa Ofisi katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Njombe na Geita. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Mwanza (68%) na Arusha (12%).

### *(z) Kuimarisha Mfumo wa Kisheria na Kiutendaji ili kuchangia Mapambano Dhidi ya Rushwa*

130. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi zake, inatekeleza afua zenye lengo la kuchangia mapambano dhidi ya rushwa. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo Uendelevu wa kupambana na Rushwa Tanzania (*Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania – BSAAT*), kazi zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Uzinduzi wa Miongozo mitatu (**3**) ambayo ni Mwongozo wa Kuwajali na Kuwalinda Mashahidi (*Witness Care and Protection Guidelines*), Utaifishaji na Urejeshaji Mali (*Asset Forfeiture and Recovery*) pamoja na Usaidizi wa Kisheria wa Pande zote katika Masuala ya Jinai (*Mutual Legal Assistance in Criminal Matters*) kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi. Lengo la Miongozo hii ni kuwawezesha waendesha Mashtaka na Wapelelezi kuwa na uelewa wa kutosha wa Sheria ya Ulinzi wa Mashahidi, Urejeshaji na Utaifishaji Mali pamoja na ushughulikiaji wa maombi ya usaidizi wa kisheria wa pande zote katika masuala ya jinai.

(ii) Majalada makubwa ya rushwa yapatayo **15** yamepitiwa katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Katika mapitio hayo majalada manne (**4**) upelelezi wake umekamilika, Majalada Saba (**7**) upelelezi haujakamilika na hivyo yalirudishwa TAKUKURU kwa ajili ya kuyafanyiwa kazi maeneo ambayo yalikuwa na upungufu na kukamilisha upelelezi kabla ya kuyasajili mahakamani, Majalada matatu (**3**) ushahidi wake ulionekana umetokana na mlolongo mmoja katika utendaji wa makosa hayo na hivyo chombo chunguzi kilielekezwa kuyaunganisha majalada hayo na kuwa jalada moja na jalada moja (**1**) lilifungwa. Aidha, katika zoezi hili, Mkurugenzi wa Mashtaka aliweka notisi mbili za zuio la mali "*Prohibitory Notice*".

(iii) Majalada **14** yamepitiwa kuhusu maombi ya msaada wa kukusanya ushahidi kutoka nje. Lengo la mapitio hayo ni kuratibu ukusanyaji wa ushahidi, kuchambua nyaraka zilizowasilishwa na kuangalia kama zimekidhi vigezo na masharti ya ushahidi kutoka nchi zilizoomba.

(iv) Maombi saba (**7**) ya kuzuia mali (*restrained application*) yameandaliwa na kusajiliwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya. Katika mkoa wa Dar es Salaam maombi matatu (**3**) yalisajiliwa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, maombi mengine matatu (**3**) yalisajiliwa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza na ombi moja (**1**) lilisajiliwa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya. Aidha katika zoezi hili, Mkurugenzi wa Mashtaka ameweka notisi mbili (**2**) za zuio (*prohibitory notice*).

(v) Mwongozo wa Kubadilishana Taarifa za Kutambua Magenge ya Uhalifu umeandaliwa. Mwangozo huo, utatumiwa na wachunguzi na waendesha mashtaka katika kutambua na kubaini magenge ya uhalifu ili kujenga mfumo bora ya kukabiliana nayo kwa mbinu za kisasa.

***(aa) Kuboresha Utendaji na Maendeleo ya Rasilimaliwatu iliyo chini ya Wizara***

**I. Wizara ya Katiba na Sheria**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushughulikia na kuratibu upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji, ambapo katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 watumishi **18** wamepokelewa kutoka kwenye Taasisi mbalimbali, wakiwemo Maafisa Sheria **12,** Wachumi wanne (**4**) na kada nyinginezo (**2**). Hivyo, kufikia mwezi Aprili, 2024 Wizara ina jumla watumishi **138** wa kada mbalimbali kati ya watumishi **182** wanaohitajika kwa mujibu wa tathmini ya kazi (Job List). Upungufu mkubwa wa watumishi bado upo kwenye kada ya Wanasheria (**20**), Wachumi (**13**) na Wakaguzi wa Ndani (**3**). Jitihada za kufuatilia upatikanaji wa watumishi

wanaohitajika zinaendelea kufanyika. Pia, watumishi watatu (**3**) waliteuliwa kwenye nafasi za uongozi. Vilevile, watumishi **24** wameshiriki mafunzo wakiwemo **5** mafunzo ya muda mrefu na **19** mafunzo ya muda mfupi. Pia, watumishi **45** wameshiriki mafunzo ya ndani.

### II. Mahakama ya Tanzania

132. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Mahakama ya Tanzania ina jumla ya Watumishi 5,666. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mahakama ya Tanzania imewezesha watumishi **119** kushiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi **1,848** wameshiriki mafunzo ya muda mfupi.

### III. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

133. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jumla ya Watumishi **177**. Kati ya watumishi waliopo **177**, Watumishi **106** ni kada ya Mawakili ya Serikali na Watumishi **71** ni Watumishi wa kada nyingine. Katika kipindi kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Watumishi **38** walithibitishwa kazini, Mtumishi mmoja (**1**) aliajiriwa, Watumishi wawili (**2**) waliteuliwa kuwa Wakurugenzi Wasaidizi, Watumishi **13** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na Watumishi **112** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

### IV. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

134. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya rasilimaliwatu. Hadi kufikia Aprili, 2024 Ofisi ilikuwa na jumla ya watumishi **943** kati ya hao, Mawakili wa Serikali ni **663,** Makatibu Sheria ni **123** na kada nyingine ni **157**. Kati ya watumishi hao, watumishi **37** ni ajira mpya ambao wameajiriwa katika kipindi hiki (Makatibu Sheria **36** na Mtakwimu **1**) waliohama **5** na kuhamia **4.** Aidha, Ofisi imethibitisha kazini watumishi **231**, na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi **40** Mafunzo ya muda mrefu na watumishi wanne (**4)** mafunzo ya muda mfupi.

## V. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jumla watumishi **238**. Kati ya watumishi waliopo Mawakili wa Serikali wapo **125**, Makatibu Sheria wapo **18** na watumishi wa kada nyingine wapo **95**. Aidha, watumishi watano **(5)** wameteuliwa katika nafasi za uongozi na watumishi nane **(8)** wameajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni. Vilevile, watumishi **11** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi **56** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi

## VI. Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

136. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024 Tume ilikuwa na jumla ya Watumishi **54** wa fani mbalimbali. Aidha, katika kipindi husika watumishi **11** walihamia, mtumishi mmoja (**1**) aliajiriwa kwa masharti ya kudumu na nafasi mbili (**2**) za uongozi zilijazwa.

## VII. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina jumla ya watumishi **144**. katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliajiri watumishi **10** na watumishi wawili (**2**) walithibitishwa kazini. Pia, watumishi **13** walithibitishwa katika vyeo, watumishi **144** walipata mafunzo ndani ya nchi, watumishi wawili (**2**) walihama na watatu (**3**) walistaafu utumishi.

## VIII. Tume ya Utumishi wa Mahakama

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 vifungu vya 14(1) na 29(1) vimeainisha majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama, ikiwa ni pamoja na uteuzi, ajira, masuala ya nidhamu na maadili kwa Maafisa wa Mahakama.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024; Tume ilimshauri Mheshimiwa Rais juu ya Uteuzi wa Majaji **21** wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Msajili Mkuu wa Mahakama na Msajili

wa Mahakama Kuu. Pia, katika kuimarisha utendaji wa Mahakama, Tume ilimteua Mtendaji wa Mahakama ya Rufani, Naibu Wasajili **30**, Katibu wa Jaji Mkuu na kuwathibitisha katika vyeo viongozi **43**. Aidha, iliwathibitisha kazini watumishi **204** wakiwemo Mahakimu Wakazi **19** na kupandishwa vyeo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo **211**. Tume imeratibu kibali cha ajira mbadala kwa watumishi wa Mahakama **112** za Kada mbalimbali.

## IX. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) una jumla ya watumishi **211** ikilinganishwa na Watumishi **342** wanaohitajika hivyo kuna upungufu wa watumishi **131.** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara kupitia RITA imepandisha vyeo watumishi wawili (**2**)**,** imewathibitisha watumishi **16** kwenye vyeo, watumishi **113** walipatiwa mafunzo ikiwemo watumishi **105** mafunzo ya muda mfupi na watumishi nane (**8**) mafunzo ya muda mrefu. Aidha, watumishi **11** walihamia katika Wakala, watumishi saba (**7**) walihamishwa kwenda kwenye Taasisi nyingine za Serikali na watumishi wawili (**2**) wamestaafu kwa mujibu wa sheria.

## X. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania

141. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilipata kibali cha kuajiri watumishi saba **(7)** wa kada mbalimbali na kuwasilishwa Sekretarieti ya Ajira kwa hatua zaidi. Wizara inaendelea kufuatilia suala hili. Aidha, Mtumishi Mmoja **(1)** amepata uteuzi, sita **(6)** walihamia na **14** walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

## XI. Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Chuo kina jumla ya watumishi **109,** watumishi **64** ni wanaume, sawa na asilimia **58.7** na watumishi **45** ni wanawake, sawa na asilimia **41.3.** Aidha; katika kipindi cha julai hadi Aprili, 2024, watumishi **6** ni ajira mpya, mtumishi **1** amethibitishwa kazini, watumishi **22** wamethibitishwa

kwenye vyeo, mtumishi mmoja (**1)** ameteuliwa, watumishi watano (**5**) wamehamia, watumishi saba (**7**) wamehama, mtumishi mmoja (**1**) amestaafu. Aidha, jumla ya watumishi **91** wamepata mafunzo, kati ya hao watumishi **84** wamepta mafunzo ya muda mfupi na watumishi saba (**7**) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu.

## G. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

143. ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu, Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:

(i) Uhaba na uchakavu wa ofisi na makazi hususan katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya;

(ii) Kuongezeka kwa uhitaji wa huduma za kisheria ikilinganishwa na uwezo rasilimali fedha na watumishi;

(iii) Kuongezeka kwa makosa yanayotokana na uhalifu kwa njia ya mtandao ikilinganishwa na uwezo wa kuyabaini.

(iv) Gharama kubwa za kuendesha mashauri ya nje ya nchi ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa jambo ambalo linasababisha kuomba kupatiwa fedha nje ya bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na

(v) Upungufu wa Mawakili wa Serikali wenye ubobezi katika maeneo ya gesi, mafuta, uwekezaji, anga, madini, uchumi wa buluu, na maeneo mengine ya kimkakati hali inayosababisha kupungua kwa ufanisi katika uendeshaji, usikilizwaji wa kesi na upekuzi wa mikataba.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto zilizotajwa, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zake imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kuboresha miundombinu ya Mahakama kulingana na Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama;

(ii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji haki;

(iii) Kuendelea kuwapatia mafunzo endelevu wataalamu wa Sekta ya Sheria ili kukabiliana na makosa yanayotendeka kwa kutumia teknolojia za kisasa hususan TEHAMA;

(iv) Kuimarisha matumizi ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala pamoja na kutumia TEHAMA ili kupunguza ushughulikiaji wa mashauri kwa kukutana ana kwa ana; na

(v) Kuwajengea uwezo Mawakili kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika maeneo maalum ya kimkakati.

## H. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### (a) Vipaumbele vya Wizara

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara na Taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria na utoaji haki kwa umma ili kuendana na Mipango ya Sekta ya Sheria nchini; na Mipango ya Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa kipindi husika. Katika kufikia azma hiyo maeneo mahsusi ya kipaumbele yameainishwa ambayo ni:-

(i) Kutunga Sera ya Taifa ya Haki Jinai;

(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma;

(iii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya Mahakama, kuharakisha mashauri ya kawaida na kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(iv) Uandishi wa sheria ikiwa ni pamoja na Kuandaa Toleo la Sheria Ndogo zilizofanyiwa urekebu mwaka 2025 na kuimarisha Marejeo na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa;

(v) Kuendesha mashtaka ya jinai Kuimarisha utenganishaji wa shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

(vi) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, sheria za kimataifa na mikataba;

(vii) Kuwezesha uanzishwaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro;

(viii) Kuwezesha Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kuanza kutekeleza majukumu yake;

(ix) Kuratibu masuala ya haki za binadamu, utawala bora na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;

(x) Kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu pamoja na usajili na ufilisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara;

(xi) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria ikiwa ni pamoja na Kufanya Mapitio ya Mifumo wa Sheria inayosimamia Elimu, Michezo ya Kubahatisha, Adhabu ya kifo na Kifungo cha Maisha na Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kibenki na Taasisi za fedha;

(xii) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sheria za utajiri asili na maliasilia za nchi;

(xiii) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xiv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki na huduma za kisheria; na

(xv) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu ya Wizara na taasisi zake ikiwemo ajira, uteuzi, nidhamu na maadili.

**(b) Kazi Zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kutayarisha Sera ya Haki Jinai na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo;

(ii) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kulinda haki za binadamu na watu;

(iii) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mikataba miwili (**2**) ya Haki za Binadamu ambayo Serikali imeridhia;

(iv) Kuratibu Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu wa Mapitio Katika Kipindi Maalum (UPR);

(v) Kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;

(vi) Kuanzisha na kuratibu madawati ya Huduma za Msaada wa Kisheria ngazi ya kitaifa na kijamii;

(vii) Kushughulikia maombi ya kuongezewa muda wa kufungua mashauri ya madai nje ya muda wa ukomo mahakamani;

(viii) Kuandaa mikataba ya kuwarejesha wahalifu watoro kwenye nchi walikofanya uhalifu;

(ix) Kuratibu tafsiri ya Sheria **161** kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili;

(x) Kuwezesha uanzishwaji na uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Usuluhishi wa Migogoro kwa njia mbadala Tanzania;

(xi) Kuimarisha mifumo ya Sheria na Kanuni za Utatuzi wa Migogoro kwa njia mbadala;

(xii) Kuratibu na kuwezesha Mapitio ya Sheria **20** zinazohusu Haki jinai;

(xiii) Kusajili mikataba **30** ya Utajiri asili na maliasilia za nchi ambazo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimeingia na wawekezaji;

(xiv) Kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa utekelezaji wa Sheria za Utajiri asili na Maliasilia za Nchi Sura 449 na 450;

(xv) Kutoa uelewa kuhusu Sheria za Utajiri asili na maliasilia za Nchi Sura 449 na **450** kwa Mawaziri **10**, Makatibu Wakuu **10**, Wakurugenzi wa halmashauri **50**, Maafisa Viunganishi **15** na Wawakilishi wa Wananchi **100** katika mikoa mitano (5) ya Tanzania Bara;

(xvi) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria za Utajiri asili na Maliasilia za Nchini Sura 449 na 450 katika Mikoa mitano (**5**) yenye uwekezaji mkubwa wa utajiri asili na maliasilia za Nchi;

(xvii) Kutoa mafunzo kwa Halmashauri **50** za Wilaya kuhusu utawala bora kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

(xviii) Kufanya tathmini ya uelewa wa wanafunzi kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Taasisi 10 za elimu;

(xix) Kufanya ziara katika magereza **20** na vizuizi **20** katika vituo vya polisi ili kutathmini uzingatiwaji wa utoaji haki;

(xx) Kutoa Elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma Katika Halmashauri **184**;

(xxi) Kutoa mafunzo kwa Askari Polisi na Magereza kuhusu utoaji wa huduma za kisheria katika maeneo ya vizuizi;

(xxii) Kuendeleza, kuboresha na kufungamanisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji haki katika Sekta ya Sheria;

(xxiii) Kuanzisha na kuendesha Mfuko wa Kuwalinda Watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi;

(xxiv) Kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wanafunzi **1,500**;

(xxv) Kusajiri na kutoa vyeti kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano;

(xxvi) Kuratibu na kusimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu ikiwemo vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili; na

(xxvii) Kuratibu na kusimamia ufilisi na udhamani ikiwemo kutoa elimu ya wosia kwa umma.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kuendesha na kusimamia zoezi la usaili baada ya kupata kibali cha Ajira kutoka ORUTUMISHI;

(ii) Kusimamia zoezi la Uteuzi kwa Watumishi wa Mahakama;

(iii) Kutoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya;

(iv) Kuendesha vikao vya mashauri na nidhamu;

(v) Kufanya ziara kwa ajili ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya;

(vi) Kutoa elimu kwa umma kupitia Vyombo vya habari na matukio mbalimbali; na

(vii) Kuendelea kuimarisha Mifumo ya Ajira, Nidhamu na Maadili kwa watumishi wa Mahakama.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kufanya urekebu wa Sheria Ndogo;

(ii) Kutoa Toleo la Sheria Ndogo zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2025;

(iii) Kuanza na kukamilisha tafsiri ya sheria 188 za Awamu ya Pili.

(iv) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma kuhusu matumizi sahihi ya Sheria zinazowagusa moja kwa moja mfano: Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya), Sura ya 287; na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Sura ya 288

(v) Kufanya uchambuzi wa masuala ya Sheria yanayoleta changamoto kwa wananchi mara kwa mara mfano: migogoro ya matumizi na umiliki wa ardhi na mirathi n.k.;

(vi) Kufanya Marejeo ya Mikataba ya Nishati na Rasilimali za Nchi yakiwemo Madini kwa kuainisha athari zinazohusiana na Mikataba husika ili kusaidia kutengeneza mpango wa kushughulikia athari hizo;

(vii) Kufanya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa;

(viii) Kuunganisha Mfumo wa OAG-MIS na Mifumo mingine kama vile Mfumo wa Kesi wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA);

(ix) Kuwajengea uwezo Watumishi kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mikataba, Uandishi wa Sheria, Ushauri wa Kisheria, Uchumi, Fedha na Utawala;

(x) Kufanya Majadiliano ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa kushiriki majadiliano ya mikataba ya Kimataifa na Kushiriki Mikutano ya Kikanda na Kimataifa. (EAC; SADC; Joint Commission Meetings; AU; (UN); na Vikao vya *Bilateral* na *Multilateral*;

(xi) Kumaliza ujenzi wa jengo la Mkoa wa Mwanza na kuendelea na ujenzi wa jengo la Mkoa wa Arusha; na

(xii) Kukusanya takwimu na taarifa muhimu kuhusu aina za uhalifu zinazotendeka, maeneo yanayokumbwa na uhalifu, na mifumo ya uhalifu inayotumiwa.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (Fungu 19) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kuiwakilisha serikali kwenye mashauri ya kikatiba, haki za binadamu, uchaguzi na mashauri yote ya kimataifa;

(ii) Kuiwakilisha serikali kwenye mashauri ya usuluhishi ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuiwakilisha serikali kwenye kesi za madai na usuluhishi za kimataifa;

(iv) Kuendelea kuboresha mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa taarifa za mashauri;

(v) Kuendelea kiboresha ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali katika mikoa;

(vi) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro; na

(vii) Kusimamia, kufuatilia na kupitia taratibu za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (Fungu 35) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na uendeshaji wa kesi za jinai;

(ii) Kushughulikia malalamiko yanayohusu haki jinai kwa wakati;

(iii) Kufanya ukaguzi katika maeneo yanayohifadhi mahabusi na wafungwa;

(iv) Kufanya vikao mbalimbali na vyombo chunguzi;

(v) Kuhuisha miongozo mbalimbali kwa lengo la kuharakisha upelelezi;

(vi) Kuendelea kufungua Ofisi za Wilaya kwenye Wilaya ambazo hazina Ofisi;

(vii) Kuendesha mashauri ya utaifishaji wa mali zinazotokana na uhalifu;

(viii) Kutayarisha programu mbalimbali za utoaji elimu kwa jamii juu ya utaifishaji na urejeshwaji wa mali zinazotokana na uhalifu;

(ix) Kutoa ushirikiano katika kukusanya ushahidi na kusafirisha mashahidi na wahalifu;

(x) Kushiriki katika mikutano ya kamati mbalimbali za uanachama wa Mamlaka mbalimbali zinazohusika na uendeshaji wa mashauri ya jinai; na

(xi) Kuendelea na ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Mashtaka katika Mikoa na Wilaya.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kutatua mashauri ya kawaida na kumaliza mashauri ya muda mrefu (backlog);

(ii) Kuimarisha uwezo katika Ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(iii) Kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

(iv) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;

(v) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki; na

(vi) Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, na nidhamu kwa watumishi.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kufanya utafiti wa namna Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinavyoendesha shughuli zao katika kuzingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(iii) Kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara;

(iv) Kupokea na kushughulikia malalamiko kuhusu masuala ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(v) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali kuhusu Sheria, Miswada na Kanuni kuhusu uzingatiaji wa Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora.

(vi) Kufungua ofisi ya Tume katika Mkoa wa Tabora;

(vii) Kufanya ufuatiliaji na kutathmini hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi wa Mkuu 2025;

(viii) Kufanya ukaguzi wa magereza, vituo vya polisi na maeneo mengine ya vizuizi ili kutathimini hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(ix) Kuratibu mahusiano na wajibu wa Tume katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda za Haki za Binadamu na Utawala Bora.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Fungu 59) katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kufanya Mapitio ya Mfumo wa Sheria Unaosimamia Elimu;

(ii) Kufanya Tathmini ya Mfumo wa Sheria Unaosimamia Michezo ya Kubahatisha;

(iii) Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Adhabu ya kifo na Kifungo cha Maisha;

(iv) Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria Unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kibenki na Taasisi za fedha;

(v) Kujenga Mfumo wa kielektroniki wa utendaji kazi (LRMIS);

(vi) Kuwezesha Mawakili 18 kuhudhuria Mfunzo ya Utafiti, Tathmini na Uandishi wa Sheria; na

(vii) Kuendelea na Ujenzi wa Ofisi katika Mji wa Serikali-Mtumba.

**(c) Makusanyo ya Maduhuli**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara na Taasisi inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **12,676,199,000** ikiwa ni maduhuli kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na.11**.

**(d) Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mpango na Bejeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

155. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **441,260,152,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu nane **(8)** ya Wizara na taasisi zake ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi Zake kwa mwaka wa Fedha, 2024/2025**

| | **Fungu la Matumizi** | **Bajeti 2024/2025** |
|---|---|---|
| 1 | Mishahara ya watumishi | 112,423,492,000.00 |
| 2 | Matumizi Mengineyo | 223,164,341,000.00 |
| 3 | Miradi ya Maendeleo-Ndani | 45,619,111,000.00 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo- Nje | 60,053,208,000.00 |
| | **JUMLA** | **441,260,152,000.00** |

156. ***Mheshimiwa Spika,*** kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama inavyoonekana hapo chini: -

**(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 775,023,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 4,723,629,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 0.00 |

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 0.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **5,498,652,000** |

**(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 4,211,099,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 22,376,187,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 1,314,506,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 450,000,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **28,351,792,000.00** |

**(iii) Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 4,304,051,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 16,446,669,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 0.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **20,750,720,000** |

**(iv) Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 16,397,290,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 61,143,087,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 9,943,517,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 50,000,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **87,533,894,000.00** |

**(v) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 74,538,577,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 78,620,476,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 31,002,000,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 57,438,500,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **241,599,553,000.00** |

**(vi) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria (RITA na LST)**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 7,820,523,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 30,567,829,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 3,359,088,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 1,592,650,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **43,340,090,000** |

**(vii) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 3,523,274,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 5,162,386,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 522,058,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **9,207,718,000.00** |

**(viii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - Sh. | 927,712,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | - Sh. | 4,124,078,000.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - Sh. | 0.00 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - Sh. | 0.00 |
| **Jumla Ndogo** | **- Sh.** | **5,051,790,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **- Sh.** | **441,260,152,000.00** |

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **441,260,152,000.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **112,423,492,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, Shilingi **223,164,341,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi **105,672,319,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati, kuna wageni ambao tunao hapa. Wageni wa Mheshimiwa Katani Katani, Mbunge wa

Tandahimba. Hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Tandahimba wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wilaya. Karibuni sana Bungeni, ahsante. *(Makofi)*

Baada ya utambulisho huo sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Katiba, Utawala na Sheria, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, UTAWALA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba taarifa nzima iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi.

(b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na Maoni ya Kamati.

(c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(d) Sehemu ya nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati.

(e) Sehemu ya tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(e) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawanda ya uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba ambayo ni:-

(a) Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria;

(b) Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(d) Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(e) Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(f) Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; na

(g) Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka

msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Makusanyo ya Maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria;

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(e) Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli, Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 105,002,000. Kati ya fedha hizo Fungu Na. 41 – Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya shilingi 45,000,000. Fungu Na. 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya shilingi 60,000,000 na Fungu Na. 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ililenga kukusanya shilingi 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli unaonesha yafuatayo:-

(a) Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya chini ya lengo. Hadi kufikia Februari, 2024 imekusanya shilingi 16,232,503 sawa na asilimia 56.07 tu. Fungu hili lililenga kukusanya shilingi 45,000,000 kutoka kwenye Ada za Usajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria, Mashirika na Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala za Majadiliano, Maridhiano, Upatanishi na Usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na kuondolewa kwa ada ya wasaidizi wa kisheria pamoja na upungufu wa wataalam wenye ujuzi na sifa zinazotakiwa kimataifa katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi nje ya nchi. Aidha, mpango wa Serikali uliopo ni kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuwajengea uwezo wataalam kutoka ndani ya nchi yetu.

(b) Fungu 36 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hadi kufika Februari, 2024 imekusanya kiasi cha shilingi 56,000,000 sawa na asilimia 93.33 ya lengo la makusanyo.

(c) Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hiyo haijafanikiwa kukusanya kiasi chochote cha fedha ya shilingi 2,000 iliyoidhinishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwenye fungu hili unatokana na mauzo ya hati za zabuni na marejesho ya mishahara kwa watumishi watakaoacha kazi. Hadi kufikia Februari, 2024 hakuna mauzo yoyote ya zabuni yaliofanyika wala mtumishi kuacha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya Fungu Namba 41 na Fungu Namba 55 chini ya ofisi hii, yanaweza kutafsiriwa kwamba, malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi au vyanzo vya maduhuli vilivyoainishwa havikuwa vya uhakika na siyo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo ni vyema Wizara na Taasisi zake zote zikazingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Aidha, Kamati ilishauri Fungu Na. 55 lisiwekewe Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli mpaka pale Serikali itakapojiridhisha na uhalisia wa makusanyo ya maduhuli kwenye ofisi hiyo. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika jedwali Na.01 la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi katika Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba kwa ujumla Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa shilingi bilioni 171.09 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi kufikia Februari, 2024 ofisi hii imepokea jumla ya shilingi bilioni 88.4 sawa na 51.67% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Taasisi zote saba chini ya ofisi hii hazijafanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa 66.6% hadi kufikia Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla siyo wa kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya ofisi hii zinapatikana kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2 na jedwali Na. 3 ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; wakati Waziri wa Katiba na Sheria alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, aliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 24.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta zinazosimamiwa na Kamati. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika jedwali Na. 4 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako

Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, maduhuli katika Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 105,000,000 ikilinganishwa na shilingi milioni 105,002,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika jedwali Na. 5 katika taarifa hii. Hii ni sawa na upungufu wa 0.002% ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa maoni kwamba kukosekana kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Fungu 55 ni uzingatiaji wa maoni ya Kamati kuwa Wizara iweke malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 182,502,834,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 37,958,969,000 ni mishahara na shilingi 144,543,865,000 ni matumizi mengineyo kama ambavyo yamechanganuliwa katika jedwali Na. 6 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 25% ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoishia ambao bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti ilikuwa shilingi 146,108,546,037. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 17,231,819,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 14,617,111,000 ni fedha za ndani na shilingi 2,614,708,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa shilingi 7,644,681,000 sawa na 30.73% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Sababu ya upungufu huo ni ukomo wa bajeti ya Serikali. Mchanganuo wa miradi ya maendeleo ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 7 katika taarifa hii. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha maoni ya Kamati yanayolenga mtazamo ambao ni msingi wa ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahususi fungu kwa fungu; Fungu Namba 41, Wizara ya Katiba na Sheria: -

(a) Serikali ihakikishe inaratibu Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign)* kwa mikoa 20 ambayo bado haijafikiwa;

(b) Wizara kwa kushirikiana na sekta husika ikamilishe mchakato wa tafsiri ya Sheria 258 kutoka kwenye lugha ya Kingereza kwenda kwenye lugha ya Kiswahili;

(c) Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;

(d) Serikali iimarishe mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ikiwa ni pamoja na kuwaandaa wataalamu wenye ujuzi na sifa zinazotakiwa kimataifa katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi ndani na nje ya nchi;

(e) Serikali iandae sera mahsusi itakayosimamia Mifumo ya Utoaji Haki Jinai na Haki Madai; na

(f) Serikali iendelee na kampeni yake ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:-

(a) Serikali iendelee kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili kuwawezesha kuandaa na kupitia kwa ufanisi mikataba na makubaliano mbalimbali ya Serikali; na

(b) Serikali iweke mfumo wa utoaji wa motisha kwa mawakili wa Serikali watakaowezesha ushindi wa mashauri mbalimbali ya madai ya Serikali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ihakikishe kuwa uendeshaji mashtaka na usimamizi wa masuala yote ya kesi unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ofisi hii iimarishe uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa vyombo vya uchunguzi kama vile Jeshi la Polisi, TAKUKURU nakadhalika, ili kuhakikisha kuwa upelelezi unafanyika kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama:-

(a) Tume iendelee kuratibu nidhamu na maadili kwa Watumishi wa Mahakama, ikiwa ni pamoja na kushughulikia kwa haraka mashauri ya kinidhamu dhidi ya Watumishi wa Mahakama; na

(b) Tume iimarishe utendaji kazi wa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya kwa kutoa miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa Kamati hizo na kufanya ukaguzi wa uendeshaji wa vikao kwenye Kamati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Serikali ihakikishe inaendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa tume ili kuiwezesha kuwa na watumishi wa kutosha na vitendea kazi kama vile magari ili tume iweze kufika maeneo mbalimbali yenye matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu 50 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Serikali iendelee kufanya tafiti na tathmini mbalimbali za utekelezaji wa sheria ili kubaini tija na kupendekeza maboresho katika sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano alioupatia Kamati, ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inamshukuru Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao ameendelea kuipa Kamati. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hii, Bibi Mary Gaspar Makondo; Dkt. Khatibu Kazungu, Naibu Katibu Mkuu; Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Ndugu Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Ndugu Patience Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ndugu George Mandepo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; na Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

### 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(e) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni: -

a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria;
b) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
c) **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
d) **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama;
e) **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
f) **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; na
g) **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria;
(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na
(e) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 105,002,000**, kati ya fedha hizo **Fungu Na. 41** - Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya **Sh. 45,000,000**, **Fungu Na. 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya **Sh. 60,000,000** na **Fungu Na. 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ililenga kukusanya **Sh. 2,000**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

(a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya chini ya lengo, hadi kufika Februari, 2024 makusanyo ni **Sh. 16,232,503** sawa na asilimia **36.07** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu hili lililenga kukusanya **Sh. 45,000,000** kutoka kwenye ada ya usajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria (Mashirika) na Watatuzi wa Migogoro kwa njia Mbadala za majadiliano, maridhiano, upatanishi na usuluhishi. Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na kuondolewa kwa ada ya wasaidizi wa kisheria pamoja na Upungufu wa wataalam wenye ujuzi na sifa zinazotakiwa kimataifa katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi nje ya nchi. Aidha, Mpango uliopo wa Serikali ni kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuwajengea uwezo wataalam kutoka ndani ya nchi.

(b) **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka hadi kufika Februari, 2024 imekusanya kiasi cha **Sh. 56,000,000** sawa na **asilimia 93.33** ya lengo la Makusanyo.

(c) **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufika Februari 2024 Ofisi hiyo haijafanikiwa kukusanya kiasi chochote cha fedha ya **Sh. 2,000** ilioidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unatokana na mauzo ya hati za zabuni na marejesho ya mishahara kwa watumishi watakaoacha kazi, hadi kufikia Februari, 2024 hakuna mauzo yoyote ya zabuni yaliofanyika wala Mtumishi kuahc kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya **Fungu Na. 41** na **Fungu Na. 55** chini ya Ofisi hii, yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli.

Aidha, Kamati ilishauri **Fungu Na. 55** lisiwekewe makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli mpaka pale Serikali itakapo jiridhisha na uhalisia wa makusanyo ya maduhuli kwenye Ofisi hiyo.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: MAKUSANYO YA MADHUHULI 2023/2024**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 16,232,503 | 36.07 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 56,000,000 | 93.33 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **105,002,000** | **72,232,503** | **68.79** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 2.3 *Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti*

#### 2.3.1 Fungu Na. 41 - Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu hili iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 47,394,011,037**, kati ya fedha hizo **Sh. 31,787,511,037** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 7,234,664,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 24,552,847,037** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 15,561,500,000** ilitengwa kwa ajili

ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 5,110,800,000** ni fedha za ndani kwa ajili ya Mradi Na. 5507: Upatikanaji Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike, Mradi Na. 5508: Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu na Mradi Na. 6201: Haki Mtandao (*e-Justice*) na **Sh. 10,450,700,000** ni fedha za nje kwa ajili ya uratibu wa Miradi sita (6) ya uwezeshaji wa upatikanaji Haki za Kisheria na Haki za Binadamu Tanzania ikiwemo ujenzi wa Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania *(BSAAT)*.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 24,661,913,368.67** sawa na asilimia **52.03** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 21,981,324,729.57** sawa na asilimia **69.15** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 4,406,052,866.56** sawa na asilimia **70** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 17,575,271,863.01** sawa na asilimia **71.58** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 2,664,356,136** sawa na asilimia **17.12** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.2 Fungu Na. 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 18,817,867,000** kati ya fedha hizo **Sh. 16,362,867,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 4,072,737,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 12,290,130,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 2,455,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 2,000,000,000** ni fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria Mkoani Mwanza na Arusha na **Sh. 455,000,000** ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (*Building Sustainable Anti- Corruption Action Tanzania (BSAAT)*.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 10,918,921,653.3** sawa na **asilimia 58.02** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh.**

**9,667,660,672.37** sawa na asilimia **59.08** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 2,545,750,450** sawa na asilimia **62.50** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 7,121,910,222.37** sawa na asilimia **58** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 1,251,260,980.93** sawa na asilimia **51** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 68,858,929,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 61,938,929,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 14,766,538,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 47,172,391,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 6,860,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 6,000,000,0000** ni fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Ofisi na **Sh. 860,000,000** ni fedha za nje ambapo **Sh. 260,000,000** ni kwa ajili ya Mradi wa *UNICEF Support Mult-sectoral Project* na **Sh. 600,000,000** ni kwa ajili ya Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (*Building Sustainable Anti- Corruption Action Tanzania (BSAAT)*.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea jumla ya **Sh. 32,012,791,336.68** sawa na asilima **46.49** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 29,008,752,390.16** sawa na **asilimia 46.83** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 7,167,224,015.20** sawa na asilimia **48.53** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 21,841,528,374.96** sawa na asilimia **46.30** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 2,948,038,947.48** sawa na **asilimia 43** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.4 Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama;

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 5,595,906,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 734,606,000** ni

Mishahara (PE) na **Sh. 4,861,300,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 3,138,981,133** sawa na asilima **56.09** ya bajeti iliyoidhinishwa. kati ya fedha hizo, **Sh. 457,743,560** sawa na asilimia **62.31** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 2,681,237,573** sawa na asilimia **55.15** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.5 Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 8,151,540,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 8,151,538,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 2,847,924,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 5,303,614,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora jumla ya **Sh. 5,391,702,967** sawa na asilima **66.14** ya bajeti iliyoidhinishwa. kati ya fedha hizo, **Sh. 1,813,315,000** sawa na asilimia **63.67** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 3,578,387,967** sawa na asilimia **67.47** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.6 Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 5,195,945,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 950,736,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 4,245,209,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilipokea jumla ya **Sh. 2,775,323,533.30** sawa na asilima **53.41** ya bajeti iliyoidhinishwa. kati ya fedha hizo, **Sh. 543,596,000** sawa

na asilimia **57.17** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 2,231,727,533.30** sawa na asilimia **52.57** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.7 Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 17,075,850,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 3,629,161,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 13,446,669,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya **Sh. 9,505,049,229.44** sawa na asilima **55.66** ya bajeti iliyoidhinishwa. kati ya fedha hizo, **Sh. 2,413,018,000** sawa na asilimia **66.48** zilipokelewa kwa ajilii ya Mishahara (PE) na **Sh. 7,092,031,299.44** sawa na asilimia **52.74** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) kwa ujumla, Wizara ya Katiba na Sheri iliidhinishiwa **Sh. 171,090,048,037/=** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 88,404,683,221.39/=** sawa na **asilimia 51.67** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

(b) Taasisi zote saba chini ya Ofisi hii hazijafanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla si wa kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa

na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Jedwali Na. 3.**

**JEDWALI NA. 2: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 31,787,511,037 | 21,981,324,729.57 | 69.15 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 16,362,867,000 | 9,667,660,672.37 | 59.08 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 61,938,929,000 | 29,008,752,390.16 | 46.83 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 5,595,906,000 | 3,138,981,133 | 56.09 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 8,151,538,000 | 5,391,702,967 | 66.14 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 5,195,945,000 | 2,775,323,533.30 | 53.41 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 17,075,850,000 | 9,505,049,229.44 | 55.66 |
| **JUMLA KUU** | **146,108,546,037** | **81,468,794,654.84** | **55.75** |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 15,561,500,000 | 2,664,356,136 | 17.12 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 2,455,000,000 | 1,251,260,980.93 | 51 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 6,860,000,000 | 2,948,038,947.48 | 43 |
| **JUMLA KUU** | **24,876,500,000** | **6,863,656,064.41** | **27.6** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri wa Katiba na Sheria alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 aliidhinishiwa jumla ya **Sh. 24,876,500,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4: MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA YA MRADI | JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | |
|---|---|---|---|---|
| | | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 5501 | Awamu ya Pili ya Uimarishaji wa Upatikanaji Haki za Kisheria na Haki za Binadamu | - | 234,510,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Tanzania | | |
| | 5502 | Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania (*BSAAT*) | - | 650,000,000 |
| | 5507 | Upatikanaji Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike | 442,668,000 | 3,912,627,880 |
| | 5508 | Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu | 2,057,002,500 | - |
| | 6201 | Haki Mtandao (*e-Justice*) | 2,611,129,500 | - |
| | 6207 | Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji Haki (*IMPACT*) | **-** | 2,041,132,658 |
| | 6517 | Kuimarisha Haki za Mtoto (*UNICEF Multisectoral*) | **-** | 3,378,219,462 |
| | 4632 | Program ya Usimamizi wa Utajiriasili na Maliasilia za Kijamii na Kiuchumi Tanzania (*Natural Wealth and Resources Socio economic Governance*) | **-** | 234,510,000 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasher | 6389 | Construction of Office Building | 2,000,000,000 | **-** |
| | 6210 | Mradi Endelevu wa | **-** | 455,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ia Mkuu wa Serikali | | Kupambana na Rushwa Tanzania (Building Sustainable Anti-Corruption Action Tanzania (BSAAT) | | |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 6389 | Ujenzi wa Majengo ya Ofisi | 6,000,000,000 | - |
| | 6517 | UNICEF Multisectoral Project | - | 260,000,000 |
| | 5502 | BSAAT Support Project | - | 600,000,000 |
| | **JUMLA** | | **13,110,800,000** | **11,766,000,000** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 105,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 105,002,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika **Jedwali Na. 5**. Hii ni na sawa na upungufu wa asilimia **0.002** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: MADUHULI KWA MWAKA 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 |
|---|---:|---:|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 45,000,000 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 60,000,000 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **105,002,000** | **105,000,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba, kukosekana kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Fungu Na. 55 ni uzingatiaji wa maoni ya Kamati kuwa Wizara iweke malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 182,502,834,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 37,958,969,000** ni Mishahara (PE) na **Sh. 144,543,865,000** ni Matumizi Mengineyo (OC), kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**

**JEDWALI NA. 6: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025**

| FUNGU | MISHAH ARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 7,820,520,000 | 30,567,829,000 | 38,388,349,000 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,211,099,000 | 22,376,187,000 | 26,587,286,000 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 16,397,290,000 | 61,143,087,000 | 77,540,377,000 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 775,023,000 | 4,723,629,000 | 5,498,652,000 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 3,523,274,000 | 5,162,386,000 | 8,685,660,000 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 927,712,000 | 4,124,078,000 | 5,051,790,000 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 4,304,051,000 | 16,446,669,000 | 20,750,720,000 |
| **JUMLA KUU** | **37,958,969,000** | **144,543,865,000** | **182,502,834,000** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa asilimia **25** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 146,108,546,037**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu

mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 17,231,819,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 14,617,111,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 2,614,708,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa **Sh. 7,644,681,000** sawa na asilimia **30.73** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya upungufu huo ni ukomo wa bajeti ya Serikali, Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7.**

**JEDWALI NA. 7: MCHANGAUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | **Mradi Na. 5501:** Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji Haki na Ulinzi wa Haki za Binadamu Tanzania (*Strengthening Access to Justice and Human Rights Protection in* | - | 262,734,400 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | *Tanzania*) | | |
| | **Mradi Na. 5508:** Mradi wa Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu (*Access to Justice for Sustainable Development*) | 1,659,088,000 | |
| | **Mradi Na. 6201:** Mradi wa Upatikanaji Haki Kielektroniki (*e-Justice*) | 1,700,000,000 | - |
| | **Mradi Na. 5502:** Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania – BSAAT) | - | 650,000,000 |
| | **Mradi Na. 6517:** *UNICEF Support to Multi sectoral* | | 679,915,600 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | **Mradi Na. 6389:** Construction of Office Building | 1,314,506,000 | - |
| | **Mradi Na. 6210**: Strengthening Anti Corruption Program | - | 450,000,000 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | **Mradi Na. 6389**: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi | 9,943,517,000 | - |
| | **Mradi Na. 6517:** *UNICEF Support to* | - | 50,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | *Multi sectoral* | | |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | **Mradi Na. 6550**: Mradi wa Upatikanaji wa Haki na Utawala wa Sheria (*Acces to Justice and Rule of Law II Project – UNDP SUPPORT PROGRAMME*) | - | 522,058,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **14,617,111,000** | **2,614,708,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **17,231,819,000** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato

## 4.2 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu

### 4.2.1 Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria

a) Serikali ihakikishe inaratibu Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (*Mama Samia Legal Aid* Campaign) uwandani kwa Mikoa Ishirini (20) ambayo bado haijafikiwa;

b) Wizara kwa kushirikiana na Sekta husika ikamilishe mchakato wa tafsiri wa Sheria 258 kutoka kwenye lugha ya Kingereza kwenda kwenye lugha ya Kiswahili;

c) Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya utoaji haki, ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati;

d) Serikali iimarishe mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ikiwa ni pamoja na kuwaanda wataalamu wenye ujuzi na sifa zinazotakiwa Kimataifa katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi ndani na nje ya nchi;

e) Serikali iandaee sera mahususi itakayosimamia Mifumo ya utoaji haki jinai na haki madai; na

f) Serikali iendelee na Kampeni yake ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano.

### 4.2.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

a) Serikali iendelee kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili kuwawezesha kuandaa na kupitia kwa ufanisi mikataba na makubaliano mbalimbali ya Serikali; na

b) Serikali iweke mfumo wa utoaji wa motisha kwa Mawakili Serikali watakao wezesha ushindi wa mashauri mbalimbali ya madai ya Serikali ndani na nje ya nchi.

### 4.2.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ihakikishe kuwa uendeshaji mashtaka na usimamizi wa masuala yote ya kesi unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wakati. Aidha, Ofisi hii iimarishe uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa vyombo chunguzi kama vile Jeshi la Polisi, TAKUKURU, n.k ili kuhakikisha kuwa upelelezi unafanyika kwa wakati na kwa kuzingati sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

### 4.2.4 Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

a) Tume iendelee kuratibu nidhamu na maadili kwa Watumishi wa Mahakama, ikiwa ni pamoja na kushughulikia kwa haraka mashauri ya kinidhamu dhidi ya Watumishi wa Mahakama; na

b) Tume iimarishe utendaji kazi wa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya kwa kutoa miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa Kamati hizo na kufanya ukaguzi wa uendeshaji wa vikao kwenye Kamati hizo.

#### 4.2.5 Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Serikali ihakikishe inaendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ili kuiwezesha kuwa na Watumishi wa kutosha na vitendea kazi kama vile magari, ili Tume iweze kufika maeneo mbalimbali yenye matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

#### 4.2.6 Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

Serikali iendelee kufanya tafiti na tathmini mbalimbali za utekelezaji wa Sheria ili kubaini tija na kupendekeza maboresho katika Sheria hizo.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.- Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb. - Mjumbe

13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb. - Mjumbe
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb. - Mjumbe
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano alioupatia Kamati, ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati pia inamshukuru Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao ameendelea kuipa Kamati. Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na Mhe. Rais na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Bi. Mary Gaspar Makondo, Ndg. Dkt Khatibu Kazungu Naibu Katibu Mkuu, Prof. Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ndg. Sylvester A. Mwakitalu Mkurugenzi wa Mashtaka, Ndg. Patience Ntwina Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ndg. George Mandepo Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Dkt. Boniphace Luhende Wakili Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
29 Aprili, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Zedi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye hatua ya uchangiaji. Hapa nina majina ya wachangiaji ambao tutakuwa nao kwa leo. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Shally.

*(Hapa Katibu Mezani alizungumza na Mwenyekiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashauriwa kwamba bado kuna Mwenyekiti wa Bajeti hajasoma. Basi namwita Mwenyekiti wa Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa kwako, iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa

Mfuko wa Mahakama Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha, Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 217.98. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 61.23 ni mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 2.34 ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto *(IJA)* na shilingi bilioni 69.62 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni shilingi bilioni 84.78, ambapo shilingi bilioni 31 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 53.78 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 155.24 sawa na asilimia 71.22 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 50.13 zilitumika kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 72.27 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa ni jumla ya shilingi bilioni 32.84 sawa na asilimia 38.74 ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.65 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 29.19 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya matumizi mengineyo umetokana na nyongeza ya shilingi bilioni 20 ambazo zilitumika kwa ajili ya kugharamia majaji wapya walioteuliwa pamoja na kugharamia programu ya kuondoa mlundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 12.57. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 7.54 zilikusanywa sawa na 60% ya lengo. Mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2023 umeainishwa katika jedwali Na.1. la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kugharamia programu ya kuondoa mlundikano wa mashauri, ambapo ina lengo la kusaidia utolewaji haki kwa wakati na hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kama ifuatavyo: -

(a) Kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu, ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Mahakama imeweza kusikiliza mashauri 133,823 kati ya mashauri 196,592 sawa na 68.07% ya mashauri yaliyokuwepo;

(b) Kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa mashauri (*e-case management*), mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning platform*) katika Chuo cha *IJA*, na mfumo wa usimamizi wa takwimu na mitandao ya Mahakama. Mifumo hii imesaidia kuongeza tija katika shughuli za Mahakama kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za haki kwa wakati na kwa gharama nafuu;

(c) Kukamilika na kuanza kutumika kwa Mfumo wa Unukuzi na Tafsiri *(Transcription and Translation System - TTS)* ambao umeshafungwa katika Mahakama 11. Mfumo huu umesaidia kupunguza muda wa uandishi wa mwenendo wa mashtaka na uandishi wa hukumu;

(d) Kuanzishwa kwa mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri na kuendelea kufanya udhibiti na ufuatiliaji wa mifumo ya miradi, maktaba na mawakili wa Mahakama ambayo imerahisisha

upatikanaji wa huduma za Mahakama kwa wananchi na kupunguza muda wa kusikilizwa kwa watumiaji; na

(e) Kuimarisha uwezo wa ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama katika ngazi zote, ambapo hadi kufikia Februari, 2024 ukaguzi umefanyika katika vituo 958 kati ya vituo 962 vya Mahakama za chini sawa na asilimia 99.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliana na changamoto zifuatazo: -

(i) Ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida unaosababisha Mahakama kushindwa kuboresha baadhi ya huduma na mazingira ya kazi kwa watumishi;

(ii) Ufinyu wa bajeti ya fedha za maendeleo hususan fedha za ndani, hali inayosababisha baadhi ya miradi kutotekelezwa kwa wakati na baadhi kushindwa kuanza kutekelezwa;

(iii) Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi hususan katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya;

(iv) Upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali ambapo, Ofisi ya Mahakama ina upungufu wa watumishi 1,562; na

(v) Upungufu wa vitendea kazi hususan magari ambapo, Ofisi ya Mahakama ina upungufu wa magari 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/2022 hadi 2025/2026). Mpango Mkakati wa Mahakama ya Tanzania wa miaka mitano (2020/2021-2024/2025) na pia maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025. Maeneo ya kipaumbele

katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa Mfuko wa Mahakama ni yafuatayo:-

(i) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(ii) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(iii) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

(iv) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;

(v) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha utoaji haki; na pia

(vi) Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu kwa kutoa mafunzo na kusimamia nidhamu ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya bajeti kwa mwaka 2024/2025, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya shilingi bilioni 241.6 sawa na ongezeko la 10.87% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita ya shilingi bilioni 217.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 71.92 ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, shilingi bilioni 2.62 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto na shilingi bilioni 78.62 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 88.44. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 31 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 53.78 ni fedha za nje. Mchanganuo wa ongezeko la bajeti umeainishwa kwenye jedwali Na. 2 la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Mahakama unatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 12.57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu uhaba wa Mahakama za Mwanzo, zinazohitajika ni 3,959, zilizopo ni 960 sawa na 28.24% ya mahitaji. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba 70% ya mashauri yanatoka katika Mahakama za Mwanzo. Kukosekana kwa Mahakama za Mwanzo kumesababisha ongezeko la mashauri ikiwemo mashauri ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo hususan fedha za ndani ili kuongeza idadi za Mahakama za Mwanzo. Hatua hii itasaidia kufikia lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri kufikia asilimia moja au chini ya hapo kutoka asilimia tano ya mashauri ya muda mrefu yaliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa watumishi na magari kwa Mahakama, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ili Mahakama iweze kufanya kazi kikamilifu na kwa ufanisi inahitaji watumishi 6,247. Hata hivyo, watumishi waliopo ni 4,685 sawa na upungufu wa watumishi 1,562. Kamati ilitaarifiwa kwamba katika mwaka 2024/2025 Mahakama imeomba kibali cha kuajiri watumishi hao 1,562. Kati ya hao Mahakimu Wakazi ni 181.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa magari yaliyopo sasa ni 586 na yanayohitajika ni 646, hivyo kuna upungufu wa magari 60 kwa ajili ya Majaji na kuondoa magari 30 yaliyochakaa ili kuongeza kasi ya ukaguzi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza watumishi na magari katika Mahakama zote nchini ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji haki na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa utolewaji fedha za maendeleo za ndani umekuwa siyo wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 fedha za maendeleo za ndani zimetolewa kwa asilimia 11 tu ya bajeti iliyoidhinishwa. Utolewaji huu wa fedha umeathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa nyumba za majaji, hatua iliyopelekea kuongezeka kwa gharama za kukodi nyumba za majaji pamoja na kumbi za mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo za ndani kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa kuliko kutegemea fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuhakikisha inafanya maboresho makubwa ya matumizi ya TEHAMA nchini, ikiwemo kusimikwa kwa mfumo wa *Transcription and Translation System - TTS* kwa vituo 11. Mifumo hii imepunguza gharama na kuokoa fedha na kupunguza muda wa uandishi wa mwenendo wa mashtaka na hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mifumo ya Mahakama inasomana na kubadilishana taarifa. Mfano, mifumo mipya ya usimamizi wa miradi, maktaba na mawakili. Vilevile Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha usimikaji wa mfumo wa *TTS* kwa vituo jumuishi vya Mahakama vilivyobakia nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa *IPU;* na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuongoza vema Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha mashauriano na Kamati wakati wa kujadili bajeti ya Fungu 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inamshukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na Wataalam wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa

kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya bajeti ya Mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majina ya Wajumbe wa Kamati yaingie katika *Hansard* kama yalivyo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama - Fungu 40, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya shilingi 241,599,553,000 ambapo kiasi cha shilingi 71,922,320,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama; shilingi 2,616,257,000 ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; shilingi 78,620,476,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na shilingi 88,440,500,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa

Mahakama (Fungu 40) kwa mwaka wa fedha 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha, Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi bilioni 217.98.** Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 61.23** ni mishahara ya Mahakama, **shilingi bilioni 2.34** ni mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **shilingi bilioni 69.62** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni **shilingi bilioni 84.78** ambapo **shilingi bilioni 31.00** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 53.78** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya **shilingi bilioni 155.24** sawa na **asilimia 71.22** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi bilioni 50.13** zilitumika kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 72.27** zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya matumizi mengineyo kwa **asilimia 104** umetokana na mahitaji maalumu ya kugharamia majaji wapya walioteuliwa pamoja na kugharamia programu ya kuondoa mlundikano wa mashauri. Kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa ni jumla ya **shilingi bilioni 32.84 sawa** na **asilimia 38.74** ya Bajeti. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 3.65** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 29.19** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Mahakama ulipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **shilingi bilioni 12.57**. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **shilingi bilioni 7.54** zilikusanywa sawa na **asilimia 60** ya lengo. Mwenendo wa utekelezaji Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2023/24 umeainishwa katika **jedwali Na.1.**

**Jedwali Na.1. Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa Fedha 2023/24**

| Matumizi | Bajeti | Fedha zilizotolewa hadi Machi | Asilimia ya Bajeti |
|---|---|---|---|
| Mishahara ya Mahakama | 63,579,252,000 | 50,131,175,423.55 | 78.84 |
| Matumizi Mengineyo | 69,620,476,000 | 72,266,842,950.30 | 104 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 31,002,000,000 | 3,651,668,814.25 | 11.78 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 53,777,027,000 | 29,194,640,252.75 | 54.29 |
| **Jumla Kuu** | **217,978,755,000** | **155,244,327,440.27** | **71.22** |

**Chanzo**: *Mfuko wa Mahakama*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kugharamia programu ya kuondoa mlundikano wa mashauri, ambayo ina lengo la kusaidia utolewaji wa haki kwa wakati na hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Mahakama.

## 3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24.

### 3.1. Mafanikio

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Mfuko wa Mahakama umefanikiwa kutekeleza masuala yafuatayo:

a) Kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu, ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Mahakama imeweza kusikiliza **mashauri 133,823** kati ya **mashauri 196,592** sawa na **asilimia 68.07** ya mashauri yaliyokuwepo;

b) Kukamilisha ujenzi wa mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (*e-case management*), Mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning platform*) katika Chuo cha IJA, na mfumo wa usimamizi wa takwimu na mitandao ya Mahakama. Mifumo hii imesaidia kuongeza tija katika shughuli za Mahakama kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za haki kwa wakati na kwa gharama nafuu;

c) Kukamilika na kuanza kutumika kwa Mfumo wa Unukuzi na Tafsiri (Transcription and Translation appplication systemTTS) ambao umeshafungwa katika Mahakama 11. Mfumo huu umesaidia kupunguza muda wa uandishi wa mwenendo wa mashtaka na uandishi wa hukumu;

d) Kuanzishwa kwa Mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri na kuendelea kufanya udhibiti na ufuatiliaji wa mifumo ya miradi, maktaba na Mawakili wa Mahakama ambayo imerahisisha upatikanaji wa huduma za Mahakama kwa wananchi na kupunguza muda wa kusikilizwa kwa watumiaji; na

e) Kuimarisha uwezo wa Ukaguzi na Usimamizi wa shughuli za mahakama katika ngazi zote, ambapo hadi kufikia Februari,

2024 ukaguzi umefanyika katika vituo 958 kati ya vituo 962 vya Mahakama za chini sawa na **asilimia 99.1**.

### 3.2. Changamoto

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2023/24, Mfuko wa Mahakama unaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida unaosababisha Mahakama kushindwa kuboresha baadhi ya huduma na mazingira ya kazi kwa watumishi;

ii. Ufinyu wa bajeti ya fedha za maendeleo hususan fedha za ndani, hali inayosababisha baadhi ya miradi kutotekelezwa kwa wakati na baadhi kushindwa kuanza kutekelezwa;

iii. Uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi na makazi hususan katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya;

iv. Upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali ambapo, Ofisi ya Mahakama ina upungufu wa watumishi 1,562; na

v. Upungufu wa vitendea kazi hususan magari ambapo, Ofisi ya Mahakama ina upungufu wa magari 60.

## 4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 hadi 2025/26), Mpango Mkakati wa Mahakama ya Tanzania wa miaka mitano (2020/21-2024/25) na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/25. Maeneo ya kipaumbele katika Bajeti ya 2024/25 kwa Mfuko wa Mahakama ni yafuatayo:-

i. Kuraharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;

ii. Kuimarisha uwezo katika Ukaguzi na Usimamizi wa shughuli za Mahakama;

iii. Kuendelea kutekeleza Mapango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

iv. Kuboresha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;

v. Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha utoaji haki; na

vi. Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu kwa kutoa mafunzo na kusimamia nidhamu ya watumishi.

**4.1. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2024/25.**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya **shilingi bilioni 241.6** sawa na ongezeko la **asilimia 10.87** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24 ya **shilingi bilioni 217.9**. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 71.92** ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **shilingi bilioni 2.62** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **shilingi bilioni 78.62** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za matumizi ya maendeleo zilizotengwa ni **shilingi bilioni 88.44**, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 31** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 53.78** ni fedha za nje.

Mchanganuo wa ongezeko la bajeti umeainishwa kwenye **jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na.2. Ulinganisho wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama ya mwaka 2023/24 na Makadirio ya mwaka 2024/25.**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI 2023/24 | MAPENDEKEZO YA BAJETI 2024/25 | ONGEZEKO (%) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 62,234,024,081 | 71,922,320,000 | 17.4 |
| Mishahara ya IJA | 2,345,228,000 | 2,616,257,000 | 11.5 |
| Matumizi Mengineyo | 69,620,476,000 | 78,620,476,000 | 12.9 |
| **Maendeleo** | **84,779,000,000** | **88,440,500,000** | **4.3** |
| Fedha za ndani | 31,002,000,000 | 31,002,000,000 | 0 |
| Fedha za nje | 53,777,000,000 | 57,438,500,000 | 6.8 |
| **JUMLA** | **217,978,252,081** | **241,599,553,000** | **10.8** |

**Chanzo**: *Mfuko wa Mahakama*

### 4.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/25 Mfuko wa Mahakama unatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **shilingi bilioni 12.57**.

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.

### 5.1. Uhaba wa Mahakama za Mwanzo.

**Mheshimiwa Spika**, Mahakama za Mwanzo zinazohitajika ni **3,959** zilizopo ni **960** sawa na **asilimia 24.24** ya mahitaji. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba **asilimia 70** ya mashauri yanatoka katika Mahakama za mwanzo. Kukosekana kwa Mahakama za Mwanzo kumesababisha ongezeko la Mashauri ikiwemo Mashauri ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo hususan fedha za ndani ili kuongeza idadi za Mahakama za mwanzo. Hatua hii itasaidia kufikia lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri kufikia **asilimia 1** au chini ya hapo kutoka **asilimia 5** ya mashauri ya muda mrefu yaliyopo hivi sasa.

**5.2. Uhaba wa Watumishi na Magari kwa Mahakama.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Mahakama ili iweze kufanya kazi kikamilifu na kwa ufanisi inahitaji watumishi **6,247**, hata hivyo watumishi waliopo ni **4,685** sawa na upungufu wa watumishi **1,562.** Kamati ilitaarifiwa kwamba katika mwaka 2024/25 Mahakama imeomba kibali cha kuajiri watumishi **1,562** kati ya hao Mahakimu Wakazi ni **181**. Kwa upande wa magari, magari yaliyopo sasa ni **586** na yanayohitajika ni **646** hivyo kuna upungufu wa magari **60** kwa ajili ya majaji na kuondoa magari 30 yaliyochakaa ili kuongeza kasi ya ukaguzi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuongeza watumishi na magari katika Mahakama zote nchini ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa haki na kwa wakati.

**5.3. Fedha za Maendeleo za Ndani.**

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa utoleaji wa fedha za maendeleo za ndani umekuwa si wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 fedha za maendeleo za ndani zimetolewa kwa **asilimia 11** ya bajeti iliyoidhinishwa. Utolewaji huu wa fedha umeathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa nyumba za Majaji hatua iliyopelekea kuongezeka kwa gharama za kukodi nyumba za Majaji pamoja na kumbi za mikutano. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo za ndani kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa kuliko kutegemea fedha za nje.

### 5.4. Mifumo ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuhakikisha inafanya maboresho makubwa ya matumizi ya TEHAMA nchini ikiwemo kusimikwa kwa mfumo wa *Transcription and Translation Software* - TTS kwa vituo 11. Mifumo hii imepunguza gharama na kuokoa fedha kwa kupunguza muda wa uandishi wa mwenendo wa Mashtaka na Hukumu. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mifumo ya Mahakama inasomana na kubadilishana Taarifa. Mfano, Mifumo mipya ya usimamizi wa miradi, maktaba, na mawakili. Vilevile, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha usimikaji wa mfumo wa TTS kwa vituo jumuishi vya Mahakama vilivyobaki nchi nzima.

### 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa IPU na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuongoza vema Bunge letu. Vilevile, niwashukuru Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha mashauriano na Kamati wakati wa kujadili Bajeti ya Fungu 40. Aidha, Kamati inamshukuru Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama pamoja na wataalamu wote wa Ofisi ya Mahakama na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umakini na weledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu Bajeti ya Fungu 40, Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
5. Mhe. Dkt. Charles Kimei, Mb
6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
10. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb
11. Mhe. Stella Ikupa, Mb
12. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb
13. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
14. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb
15. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
16. Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb
17. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb
18. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb
19. Mhe. Omar Ali Omar, Mb
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria yenye jumla ya **shilingi 241,599,553,000** ambapo kiasi cha **shilingi 71,922,320,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **shilingi 2,616,257,000** ni Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **shilingi 78,620,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 88,440,500,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Oran Manase Njeza, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
29 Aprili, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza kwa wasilisho.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni zaidi ambao wapo katika ukumbi wetu wa Bunge ambao wamealikwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana. Tunaye Ndugu Alicia Mbuya ambaye ni Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama. Naona ametoka. *(Makofi)*

Tunaye Profesa Fatihia Massawe, Naibu Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Mahakama, nadhani wanaonekana upande ule wa chini. Tunatambua uwepo wao, lakini kwa ujumla wake Mheshimiwa Waziri amealika Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara yake ambao wako kazini sehemu mbalimbali ndani ya ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Pia Waziri wa Katiba na Sheria amealika mashirika yasiyo ya kiserikali na wajasiriamali kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Pia amealika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wajasiriamali kutoka Mkoa wa Njombe. Karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine ambao ni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 86 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge na Waziri wa Madini, hawa ni wanafunzi wa *Tanzania Medical Laboratory Students' Association (TAMELASA)* kutoka Dar es Salaam, karibuni sana kwa ziara ya mafunzo. *(Makofi)*

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Butiama na Mkoa wa Mara wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Mkoa Ndugu Ibrahim Mjanakheri, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Maryam Omar Said ambao ni wadau wa Afya ya Akili, Mazingira na Haki za Binadamu wa Shirika la *Akili Platform Tanzania* kutoka Mikoa ya Tabora, Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Kigoma. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, hawa ni marafiki zake kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hatua ya pili ambayo ni uchangiaji. Nitawaita sasa wachangiaji ambapo tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naanza kwa kukupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti Deo Mwanyika kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana kwa wasilisho lake zuri la bajeti. Nazipongeza Kamati zetu zote mbili; kwanza, Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa mawasilisho waliyoyafanya kwa niaba yetu yetu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona nchi yeyote ina amani na utulivu, basi ujue kuwa mifumo yake ya utoaji haki ni bora na imeimarika. Uniruhusu maneno haya niyanukuu tena kutoka kwa Nabii Isaya 32:17. Nabii Isaya aliishi karne ya nane Kabla ya Kristo, alisema, “Amani ni tunda la haki.” Pale ambapo haki inatendeka, amani itapatikana na itadumu.  Maneno haya yalizungumzwa miaka mingi sana, nimesema hapa, ni karne ya Nane Kabla ya Kristo. Ninavyosema

Kabla ya Kristo, maana yake, kabla ya mwaka sifuri. Karne ya nane, kabla ya mwaka sifuri, maneno haya yalizungumzwa kwamba amani ni tunda la haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii na maneno haya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayaishi kwa vitendo. Mimi nimekuwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria huko nyuma na sasa Utawala, Katiba na Sheria, sasa ni miaka nane. Mambo niliyoyaona ni mapinduzi makubwa sana ya mfumo wa utoaji na upatikanaji haki nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka hadi mwaka tumeona *commitment* kubwa ya Mheshimiwa Rais kupitia Watendaji wake Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, kupitia watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Yote tumeyaona, taasisi hizi zote tumeziona zinakwenda na zinatekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa Watanzania kwa sehemu kubwa wanaona umuhimu na wanaona *relevance* ya Wizara hii ya Katiba na Sheria ambayo ni Wizara mama ambayo ndiyo mhimili na ndiyo nguzo ya amani na utulivu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasherehekea miaka 60 ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar. Pia ni miaka 63 tangu tupate uhuru Taifa letu limebaki kuwa na amani na utulivu muda wote. *Credit* kubwa iende kwenye mifumo yetu ya utoaji haki nchini. Mahakama zetu zimekuwa na ubunifu wa hali ya juu ili kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa kila Mtanzania. Tumefuatilia taarifa za Wizara hapa, lakini pia tumefuatilia taarifa za Kamati zetu zote mbili ambazo zimewasilishwa hapa kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika vitu ambavyo tumeona, kwanza ongezeko la miundombinu ya kutolea huduma za haki kwenye ngazi za Mahakama ya Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Rufani na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kote kumekuwa na ujenzi wa miundombinu kwa maana ya ujenzi wa Mahakama. Sasa hizi Mahakama kwa namna moja au nyingine nami naweka msingi zaidi, msingi wa haki tunauona pale ambapo tunaenda kujenga Mahakama nyingi za Mwanzo ambako Watanzania wengi wanaohitaji haki wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona *commitment* kubwa sana ya Serikali. Hapa natamani sana kuipongeza Serikali katika ujumla wake, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuongoza utendaji mzuri wa Wizara hizi na kuhakikisha haki inawafikia Watanzania katika namna rahisi na namna ya ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yalikuwa ya jumla, lakini kimahususi kabisa kumefanyika mapinduzi makubwa sana ya kimifumo ndani ya Mahakama ya Tanzania. Hapa naomba kurejea kwenye Mfumo wa Unukuzi na Tafsiri ambao unafahamika kama *TTS* au kwa Lugha ya Kiingereza ni *Transcription and Translation System*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ni mashahidi na hapa wananisikiliza, tumekuwa na changamoto kubwa sana ya utoaji haki kwa wakati kwa Watanzania walio wengi. Mahakama zetu zimekuwa zinatumia muda mrefu sana kunukuu mwenendo wa mashtaka na kunukuu hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale ambapo wateja wetu ambao ni Watanzania wanahitaji tafsiri kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kwa haraka, imechukua muda mrefu sana. Jambo hilo limechangia sana kwenye kuchelewesha mwenendo na hukumu za mashtaka mengi. Mashauri mengi yamechukua muda kutolewa

maamuzi kwa sababu ya mifumo. Leo Mahakama yetu ya Tanzania ime-*adopt* Mfumo huu wa Unukuzi na Tafsiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza sana Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, ambaye amefanya jitihada za kipekee sana kuhakikisha mfumo huu unafungwa kwenye Mahakama zetu. Juu yake yuko Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania. Mapinduzi haya yanakwenda kuwawezesha Watanzania kufikiwa kwa karibu sana na kutendewa haki kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo faida nyingi ambazo kama muda ungeniruhusu, ningezisema lakini natoa tu ushauri kwa Serikali au msisitizo kwa Serikali kwa sababu Kamati zimeshasema mfumo huu umefungwa kwenye Mahakama 11 tu mpaka sasa. Mnajua kabisa mahitaji ni makubwa, Mahakama zetu zote zinahitaji hiyo huduma kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Mheshimiwa Waziri kwa sababu muda hauniruhusu sana, ahakikishe kwamba mifumo hii inakwenda kufungwa kwenye Mahakama zetu zote kuanzia Mahakama za Mwanzo mpaka Mahakama zetu za Rufani na hivyo kuwawezesha Watanzania kupata haki kwa wakati. Kwa kufanya hivyo, maana yake tutakuwa tumeliweka Taifa letu katika mazingira salama zaidi ya amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama. Namwita sasa Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa siku hii njema ambayo leo tumepokea bajeti ya mhimili mwingine katika mihimili mitatu iliyo katika nchi yetu

ikiwepo *Executive, Parliamen*t na hii ni *Judiciary*. Kwa hiyo, leo tuna bajeti nzito sana na ina mafungu takribani saba na hili ninalokwenda kulizungumzia mimi, ni lile la nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mhimili una baraka sana kwa sababu una tafsiri zile sheria tunazozitunga hapa ndani, lakini haitafsiri tu, pia inazifanyia kazi sheria hizo na inasimamia kwamba kila mtu anapata haki. Mhimili huu umefanikiwa kutumia bajeti yake ya mwaka wa awali kabla ya huu ambao unaenda kumalizika vizuri na ilipata Hati safi. Kwa hiyo, matumizi yake ni mazuri. Ile minong'ono ya rushwa, rushwa imepungua. Nakiri wazi kwamba huu mhimili unafanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuchangia kama Mjumbe wa Bajeti na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuwape walichoomba ili wakatekeleze kazi zao vizuri kwa sababu nyongeza ya bajeti ya mwaka uliopita na hapa ni 10% tu, wala hawaombi vitu vingi sana vya ajabu. Mwaka huu wanaomba takribani shilingi bilioni 241.6, ni bajeti ambayo inatamkika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuzungumzia yale machache ambayo tuliona kama ni changamoto. Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Oran Njeza ameyasema, lakini nina msisitizo kwenye mambo kadhaa ikiwemo kumaliza mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitaenda moja kwa moja kwenye kesi za mauaji. Kesi hizi zimekuweko muda mrefu na zinawaweka wale washtakiwa kuwa kwenye hali ya *suspense*, hali isiyojulikana, hali ya sintofahamu. Mshtakiwa anaumia, familia inaumia na wale waliomshtaki pia wanaumia sana kwa sababu kama ni mtu wao ameuawa, sasa kama ameuawa hukumu ni auawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua atakapokuja mtoa hoja, ni hukumu ngapi za kifo zimetekelezeka kwa kipindi cha muda wa siku za usoni? Tanzania hakuna au sisi tuna huruma sana! Huko Mahakamani hakujaenda shahidi za kutosha! Tayari mtu

amehukumiwa, hajahukumiwa, mtu ameshtakiwa kwa kuua, inachukua miaka zaidi ya 10 au 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa kawaida ambao ni *layman,* mimi ni mmojawapo, nashangaa na ninajiuliza, kama hii hukumu ya kifo haitekelezeki, kwa nini ipo? Muswada uletwe hapa na Serkali tubadili, tuseme Tanzania haitekelezi au haipo tayari kutoa hukumu ya kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nalisema kwa uchungu, lakini kwa vile jambo liko Mahakamani, siruhusiwi kutamka ila nina mtu wa karibu na nitasema mtu wa karibu kwa sababu ni mtoto wa kaka yangu. Aliuawa na akalimwa mgongoni kwa rato na ikaonekana na yule mtu akakamatwa akapelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukifika hapo huu mhimili au tunaambiwa usiseme zaidi, ni miaka imepita sasa takribani miaka 10, familia inaumia na familia ya mshtakiwa inaumia, lakini haitekelezeki. Nimeona niliseme wazi, huenda pia tuna huruma sana Tanzania, hata mimi sitaki kuua, lakini tujue ni nini kinachoenda tunapomweka mtu anakaa mahabusu kwa muda mrefu miaka nenda rudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnatuambia hapa *justice delayed is justice denied*. Iko wapi hiyo *justice* hapa? Nataka mnapokuja kutueleza tuelezwe kinagaubaga, ni nini kifanyike, kwa sababu hiyo pia ni kati ya kesi ambazo ni za mlundikano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi nyingine ni hizi kesi za kubakwa. Watoto wadogo wanafanyiwa vitu vibaya, kesi inakwenda inaulizwa, haitekelezeki, au hukumu haitoki. Inafika mwisho, mtu anawekewa dhamana. Sikatai, dhamana ni haki ya mtu, lakini kwa nini usiletwe Muswada hapa kwamba watu wanaobaka (mwanzoni tulipendekeza hapa mmoja mmoja katika kuchangia), labda wapunguziwe hizo kasi kwa kufanyiwa kile kitendo kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vipi, lakini wachomwe labda sindano ya kuwafanya wasiweze tena lile tendo. Imekuwa ngumu

kutekelezeka, lakini watoto wanatendewa vitu vibaya (watoto wa *gender* ya Ke na watoto wa *gender* ya Me). Lile jambo tulililoliomba hapa liletwe sasa. Hao wenye tabia mbaya mbaya sana, hata nashindwa kutamka hayo maneno, washughulikiwe. Hayo maneno hayatamkiki, ulimi unakuwa mzito. Washughulikiwe na tujue kabisa kwamba wamekomeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utekelezaji wa maombi ya bejeti, kwenye randama, kwenye ile kasma ya 21,112 ambayo ni *Basic Salary Non-Pensionable*, mwaka 2023 waliomba shilingi 66,000,000 tu, mwaka huu wameomba shilingi 382,320,000, nasema ni kama zaidi ya mara tano, karibu mara sita ya walichoomba. Sababu ni nini? Wanasema ongezeko la bajeti kwa kasma hii limetokana na ongezeko la watumishi wa mikataba wakiwemo madereva na mafundi sanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kila siku tunasema tumepata wahitimu wa vyuo vya *VETA*, tumepata wahitimu labda wa vyuo vingine, lakini ajira hazitoki. Mimi naiomba sana Serikali kutoka kwenye hiyo Wizara ya Utumishi, mwafungulie Mahakama waajiri wenyewe, kwa sababu unapotaka kupeleka bajeti mara 500 kwa ajili ya mkataba, kisa tu mmewazuia wasiajiri; kwa nini, wakati wana mlundikano hivyo wa *graduates* wa *level* mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawape uhuru, waupe huu mhimili uhuru wa kuajiri, la sivyo zitatumika hela nyingi sana na tayari tumeona. Leo nimekwishawaomba kwamba tuwaruhusu wapewe hili fungu waliloomba, lakini sasa kwenye ajira wanapopeleka watumishi wa mkataba ilhali ma-*graduate* tunao wengi na wahitimu wa *level* nyingine wapo wengi barabarani, siyo sahihi kabisa. Hili nalisema kwa uchungu, naomba Utumishi waangalie jinsi gani watu hawa watasaidika. Kwa bahati nzuri sana hawa ni watu ambao wanaweza kutafuta, kama ni Mahakimu wakafungua ofisi zao wakaanza kutoa huduma, lakini siyo wote. Naomba jambo hili liangaliwe kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Jaji Mkuu Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma kwa jinsi ambavyo

anaulea huu mhimili na niwapongeze pia wote wanaohusika kwenye mhimili huu. Kwa kweli ni watu ambao wanapendeza na tunawa-*admire* sana. Huku ndani tuko na Mheshimiwa Jaji, Dkt. Eliezer Feleshi na tunamwona anavyotekeleza kazi, lakini wajue pia na Spika wetu ni mmoja wa upande huo huo na wanauona huu mhimili ulivyokaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Profesa Ole Gabriel. Niseme kwa kweli amekuwa ni mtu ambaye anapenda kuelimisha watu tukiwemo sisi. Kila akiona kwamba kuna jambo tunalotaka kufahamu anatuelimisha, ndiyo maana tunaweza tukasimama tukausemea mhimili huu. Nimpongeze zaidi pia huyu huyu Profesa Ole Gabriel kwa kusimamia ujenzi wa majengo ya Mahakama katika Jiji hili la Dodoma. Tumeona majengo yote yanayojengwa na Mahakama ni majengo ambayo yana mvuto; ukiambiwa hapa ni kiasi gani unaweza ukakubali, ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili moja ambalo usiku na mchana linapeperusha bendera kidijitali, lakini linaandika pia Mahakama zilizomo, linaandika vitu vyote. Ni jengo zuri na niseme kwamba huu mhimili umeipendezesha Dodoma. Sasa pamoja na kuipendezesha Dodoma tusiishie kwenye majengo. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti vitu vyote twende navyo kwa kasi ikiwemo kuajiri na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama umewasha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite sasa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na leo tuko hapa salama, lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nyingi alizofanya na ameonyesha nia njema sana kwa kuunda ile Tume ya Haki Jinai. Vilevile Mheshimiwa Dkt. Samia ameleta sheria nyingi hapa tuzibadilishe ili ziweze kuwa na manufaa kwa Watanzania walio wengi. Vilevile nimpongeze Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Dkt. Balozi Pindi Chana kwa kazi nzuri ambayo anafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Waziri kwa kuteuliwa, yeye ni mtu *humble* sana. Kuna siku nimepiga simu saa nane ya usiku nikiwa *airport* na akapokea. Aendelee hivyo hivyo. Nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Dkt. Feleshi, *very humble* na Mheshimiwa Jaji *I still enjoy* ile *time I appeared before you.* Kwa kweli wewe ni mtu mwema sana sana na *I still think* nchi yetu imempata *Attorney General* mzuri sana, *very humble*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii. Hii Wizara ina watu wema sana, nadhani kwa Makatibu Wakuu ninaowafahamu *I think* Dkt. Mary Makondo ni *very humble*. Sijui dini yake, lakini nikimwangalia ni kama ameokoka hivi, ni mpole sana. Vilevile *DPP, DPP* ni mpole sana, *very nice, very nice team.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama walivyosema Kamati, tunaomba Serikali iendelee kutenga fedha nyingi sana ili iiwezeshe Wizara ya Katiba na Sheria kuendelea kuwahudumia Watanzania. Tumesema kila wakati kwamba utawala bora na sheria ndiyo nguzo yake, ndio msingi wa mambo yote. Kwa hivyo tukiwawezesha wataweza kutimiza jukumu lao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Ole Gabriel na Jaji Mkuu kwa kusimamia miradi ya Mahakama vizuri sana. Nchi yetu na nasema kama Wakili kwa mara ya kwanza na *I feel very jealousy* nikiona Mahakama zetu zilivyo nzuri sana; ina misingi mizuri

sana na miundombinu ni mizuri sana. Ukitembelea hizi Mahakama ambazo ni *integrated justice system* utafikiri ni hoteli fulani hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachowaomba tu sasa ni kwamba Watanzania walio wengi wanahitaji huduma hizi za Mahakama. Kwa hivyo kama walivyokuja kwenye Kamati na kuleta *plan* ya kwenda kila wilaya na tarafa, *plan* hiyo iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti mwaka jana na mwaka juzi walizungumza hapa na walisema Kiteto watajenga mahakama ya wilaya kwa bajeti ya 2024/2025. Kwa hivyo nimekuja kusema kwamba hii ndiyo 2024/2025, Kiteto na maeneo mengine ambayo hayana Mahakama tunataka Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwamba utawala wa sheria ndio msingi wa kila kitu nchini. Ripoti ya Kamati ya mwezi Februari tulizungumza na nanukuu ukurasa wa 51: "Kuhakikisha kwamba inatekeleza maamuzi yote ya Mahakama ili kulinda haki za raia ikiwemo kurejesha mali zilizotaifishwa iwapo mtuhumiwa ameshinda kesi na hatua zote za rufaa zimekamilika". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema pia kuhusu Ofisi ya *DPP* kushirikiana na taasisi zingine za upelelezi, ukamataji na utaifishwaji ili mali za watuhumiwa waweze kurudishiwa baada ya kushinda kesi zao. Mimi hapa nimezungumza mara kadhaa kuhusu kesi ya wananchi wangu wa Kiteto. Kesi yao ya mwisho ilikuwa ni kesi ya Mahakama ya Rufani Na. 356 ya mwaka 2018 ambayo hukumu yake ilitolewa Juni, 2020. Mfugaji mmoja, ng'ombe wake walikamatwa halafu alishinda kesi zote mpaka Mahakama ya Rufaa lakini mpaka leo bado hajapata haki yake na hili Mheshimiwa Waziri analifahamu kidogo kwa sababu alivyokuwa maliasili nadhani nililisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini kwa mwananchi wa kawaida? Unapopelekwa Mahakamani na ukashinda kesi? Kwa mwananchi wa kawaida kabisa wa kijijini kule Orkesumet kule, anatamani akae nyumbani Serikali imletee ng'ombe wake ama fidia;

kwa sababu ameshashinda. Hii ya kukaza hukumu sijui na kufanya nini, hizi ni kazi za mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Mheshimiwa Rais ni kwamba Watanzania wapate haki zao. Sasa nilikuwa naangalia kesi hii utashangaa sana, ng'ombe wamekamatwa walikuwa mia mbili takriban na sitini na tano, wamekaa miaka mitatu wakati wa kesi, wako Mahakamani. Siku wanashinda Mahakama ya Rufani wale Waswahili wamekwenda wamepiga hesabu wakakutwa na ng'ombe 96. Sasa wao wakachukua wale 265 toa 96 waliobaki halafu wakatengeneza fomu za ng'ombe wote wengine waliopotea, yaani 169. Mheshimiwa *Attorney General* na Mheshimiwa Waziri wa Sheria wawaambie hawa watu, *law is not mathematics, it is about principles, it is about conformity, it is about justices. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu mmoja tu anaiingizia hasara Serikali. Ng'ombe wamepotea, mwananchi hana na hivyo Serikali itashtakiwa, halafu kuna mtu mmoja tu amefanya haya. Sasa Mheshimiwa *Attorney General* utashangaa sana; nilikuwa naangalia wametengeneza kitu kinaitwa *livestock deaths certificates* ya wale ng'ombe 169. Sasa hii fomu hii kwa mara ya kwanza na mimi ni mfugaji, napata magonjwa ya ng'ombe hapa ambayo sijawahi kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *history of sickness* anasema *high fever*. Sasa sijui ni malaria? *I don't know*. Halafu *treatment given* anaandika *given,* hapo kaishiwa. Kwa sababu *if you produce documents* 169 sasa itafika mahali utakuwa una-*reproduce* hata maswali yaliyoandikwa hapo. *Treatment given* anasema *given*, fomu nyingine unachukua *treatment given local.* Halafu hawa ni watu wa Serikali, halafu wapo na wameandika majina yao hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Attorney *General* na Wizara ya Katiba na Sheria, *I think it should be fair* tusimamie utawala wa sheria na wale wanaotuchezeachezea *we must take them to task*. Haiwezekani, yaani Serikali nzima ama Wizara nzima, hawa wote, *all of us,* hata sisi tunaotunga Sheria hapa tuonekane hatusimamii eti kwa

sababu kuna mtu mmoja tu ambaye ni mvivu, anafikiri sheria ni *balance sheet,* kwamba unachukua ng'ombe 265 unatoa 69 halafu unasema wengine wamekufa, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu. Tume ya Haki za Binadamu ni Tume ya kikatiba na ni muhimu sana kwa nchi yetu. Tuiwezeshe, ipate fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi zake. Kama ilivyokuwa *envisaged* na Katiba *article* 129 na 130, walete ripoti hizi tuwe tunaziangalia na ku-*debate* hapa, nadhani itakuwa ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *DPP* nia yao ni kwenda kila wilaya ili haki isimamiwe. Sasa, hatuwezi kuwataka waende huko kama tusipoweka *resources* za kutosha ili waajiri watu wa kutosha na sheria zisimamiwe vizuri sana. Sasa tunazungumza habari ya sijui ni *16%* ya watumishi wanaotakiwa ndio walionao. Tume-*progress* kwa sababu miaka miwili, mitatu iliyopita ilikuwa ni 10%. Ina upungufu mkubwa sana na hakuna namna nyingine yoyote, ni kuwezesha *resources* hizi zipatikane ili waweze kusimamia sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na *Program ya Mama Samia Legal Aid.* Sisi tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu Manyara ilikuwa kati ya Mikoa na Kiteto ilikuwa *beneficiary* wa programu ya *Mama Samia Legal Aid.* Wamekwenda vijiji vingi sana na tuliona manufaa ya *Mama Samia Legal Aid.* Watanzania wanahitaji na ndiyo maana hata tukiwaona kwenye mikutano ya wanasiasa ama ya siasa huko Watanzania wamejaa na wanalalamika sana. Kwa hiyo hii programu ya *Mama Samia Legal Aid* pengine ingesaidia kupunguza matatizo ambayo Watanzania walio wengi wanayo huko majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati nilizungumza hapa kuhusu ng'ombe kutozwa laki moja kwa kichwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hii Wizara Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro alikuwa ni wakili, Mheshimiwa Mchengerwa wakili, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ni wakili na sasa Mheshimiwa Angellah Kairuki ni wakili. Halafu kuna watu tu wanakaa kaa tu huko, wanafikiri ni *mathematics* tu, halafu

wanatoza shilingi 100,000 kwa kichwa cha ng'ombe ilhali hakuna hata sheria moja inayo-*support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza sana hapa na Mheshimiwa *Attorney General* na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alitoa ripoti hapa, akasema nendeni huko. *By the way,* Tume ya Haki za Binadamu nao wameandika ripoti yao na wamesema *this is illegal*. Sasa huyu ni nani anayefanya *mathematics* tu? Tulizungumza hapa na Bunge lilisema kuhusu mwisho wa faini *minimum* na *maximum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siku hizi wamekuja na njia nyingine, Desemba mwaka jana wananchi wangu waliwakamata. Sasa kwa sababu wanajua *maximum* ni *ten million* wanawalazimisha watu kugawa ng'ombe kwa makundi mawili ili wa-*impose fine* ili hata kama ni mtu mmoja ndiye analipa, analipa milioni kumi kwa milioni kumi. *Law is not about mathematics*, Mheshimiwa *Attorney General we need your authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Mwenyezi Mungu awabariki na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambao wameongozana na Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Arri. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji, nimwite sasa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, niombe Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kukupongeza kwa kukaa kwenye kiti hicho; umependeza na naamini utatutendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo

yake na nia yake njema juu ya nchi yetu juu ya masuala ya utawala bora, mambo ya sheria pamoja na Katiba. Nimpongeze sana pia Mheshimiwa Waziri Pindi Chana, Naibu wake pamoja na timu yao kule chini kwa usimamizi mzuri juu ya Wizara hii, wanafanya kazi nzuri sana. Sisi kama Kamati tumepata ushirikiano mzuri kutoka kwao kwenye mambo mengi tuliyokutana, kuanzia kwenye kutembelea miradi mpaka kwenye kujadili bajeti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mheshimiwa Jaji Mkuu na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ambaye yuko humu ndani, pia Mtendaji Mkuu wa Mahakama Mheshimiwa Ole Gabriel, mtumishi wa Mungu. Pia niwapongeze sana timu zote zinazoongoza Mafungu ya Katiba na Sheria. Kwa sababu kwa kweli kazi yao ni nzuri sana, wamehusika sana katika kutuelimisha kama Kamati ili tujue kila fungu linahusika na nini na majukumu na kazi zao. Wamekuwa na bidii sana ya kukutana na Kamati ili kutuelimisha na sisi kwa sehemu kubwa tumeelewa na ndiyo maana nimegeuka kuwa mwanasheria mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa kuanzisha Vituo Jumuishi vya Mahakama *(ICJ)*. Vituo hivi kwa kweli vinatufaa sana sisi wananchi kwa sababu vina mambo mengi. Ukikuta kituo kinaitwa kituo maana yake hapo kuna Mahakama ya Mwanzo, kuna Mahakama ya Wilaya, kuna Mahakama ya Mkoa, kuna Mahakama Kuu na wakati mwingine Mahakama ya Rufaa inaweza ikatumia vituo hivi jumuishi kufanya *sessions* za Mahakama ya Rufaa. Niipongeze sana Serikali kwa *approach* hii. Naamini wananchi wataendelea kupata haki zao kwa karibu na gharama nafuu kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea vituo hivi Mwanza, Njombe, hapa Dodoma na mahali pengine, vituo hivi vimejengwa vimekamilika kabisa na ni vituo ambavyo vinajitosheleza. Niiombe tu Serikali iongeze watumishi kwenye vituo hivyo, mahakimu wa Mahakama za ngazi zote hizo wawepo kwenye vituo hivyo ili kwamba wananchi wetu wakienda pale waweze kuhudumiwa na mambo yao yaweze kuishia hapo badala ya kusafiri kuelekea mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa ajili ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuokoa fedha nyingi za Serikali, hasa kwenye mashauri haya ya nje na hata haya ya ndani. Niipongeze sana Serikali kwa sababu kupitia Wakili Mkuu wa Serikali, Serikali imeokoa fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anasoma hotuba yake, tumesikia alivyotaja mabilioni na matrilioni ya fedha yaliyookolewa, lakini sisi pia kwenye Kamati na hata taarifa yetu imetaja kwamba, Wakili Mkuu wa Serikali ameokoa fedha nyingi sana za Serikali ambazo zingepotea kama isingekuwa weledi na utaalam wa ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe ofisi hii iweze kuongezewa wafanyakazi ili wawepo wafanyakazi wa kutosha, pia mafunzo juu ya masuala ya upatanishi *(arbitration)*. Nadhani ni *field* mpya kwetu kama tunaweza kuanza kuwa na chuo cha kwetu hapa, tukafundisha wataalamu wa kutosha kuhusiana na jambo hili, litakuwa jambo jema. Kama hatuna, basi kama kuna vyuo kule nje, basi wataalam wetu wapelekwe wajifunze juu ya masuala haya ili watuwakilishe vizuri sisi Serikali. Dunia ya leo ya utandawazi na tunapokaribisha uwekezaji mwingi namna hii na unapofurika kuja Tanzania, tunahitaji ofisi hii ifanye kazi yake vizuri ikiwa na wataalamu walio na weledi kwenye mambo mbalimbali ili Taifa letu tusipate hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nizungumze mambo mawili na la tatu nitamalizia la Jimbo langu. La kwanza, ni mchakato wa kupata haki baada ya kushinda kesi, Mheshimiwa Olelekaita amezungumza kidogo. Mchakato huu kusema kweli baada ya mchakato wa kesi kuisha na mtu anatakiwa sasa apewe haki yake, mchakato ni mrefu sana. Inabidi afungue tena kesi kwa Msajili wa Mahakama kupata hiyo haki yake, aweke tena wakili kama ana uwezo wa kufanya hivyo au aanze kusafiri kupata haki yake aliyopata mahakamani kwenda mahakamani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mlolongo wote huu naambiwa uko kisheria, lakini hii sheria si inaweza ikabadilishwa? Kwa sababu

kusema ukweli mlolongo huu unawanyima haki wananchi wetu wengi mno. Kwanza, wananchi wetu akishashinda kesi hajui kama kuna mambo ya kukazia hukumu na hata huo utaratibu akielezwa wa kukazia hukumu, utaratibu wake na namna ambavyo upo kisheria ni mrefu mno, kiasi kwamba inaingiza gharama na inakatisha tamaa na wananchi wetu wengi wameshindwa kupata haki yao na wengine hata wameaga dunia hawapo, lakini haki yao walishinda mahakamani kwa sababu tu ya kipengele hiki cha kutokukazia hukumu ili kupata haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali ijaribu kuangalia sheria inayoongoza masuala haya ni sheria ya namna gani, iletwe hapa Bungeni tuweze kuirekebisha. Kama pengine labda tu ni *bureaucracy* za kimahakama, sasa utaratibu huo unaweza kufupishwa? Tukizungumzia masuala ya kidijiti ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu ameyazungumza vizuri. Masuala ya kidijiti yakienda vizuri huu utaratibu unaweza ukafupishwa ili mtu apate haki yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza, mimi nimeshinda kesi, ng'ombe wangu walikamatwa kwenye hifadhi, nikashinda kesi. Hivi Mahakama inashindwa nini sasa wakati huo huo kwa sababu imeniona nina haki, inashindwa nini kunipa haki wakati huo huo? Mpaka tena nianze utaratibu mwingine, nikasajili, nitafute mtu wa kunisaidia, kwa kweli utaratibu huu si mzuri sana na nadhani sisi kama Wabunge tunahitaji kuuangalia upya na kama ni sheria, iletwe hapa Bungeni tuibadilishe ili utaratibu huu uweze kutoa haki kwa watu wetu mara mtu anaposhinda kesi mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka kuzungumzia ni juu ya *documentation* za ushahidi. Ushahidi unapokwenda mahakamani, unatakiwa upeleke *documents* ambazo ni *original*. Kwa mfano, kama ni mkataba, nina kesi na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mpembenwe, labda za madai, nipeleke mkataba wangu ambao ni *original,* nipeleke malipo yangu ambayo nilifanya *original.* Sasa, kama nina kazi nazo zingine zinasimama kwa sababu hizi *documents* ziko kule mahakamani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki, muda wako umeisha, hitimisha.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh! Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite Dkt. Charles Stephen Kimei na muda ukiruhusu nitamwita Agnesta Lambert Kaiza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nikupongeze kwa namna unavyoendesha kikao chetu, nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kusimamia na kuimarisha mhimili huu ambao unasimamia utoaji wa haki kwa wananchi wa Tanzania na ambao kama mwenzangu alivyosema ndiyo chanzo cha amani na utulivu tulionao katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, nitoe pongezi kwa Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu, bila kumsahau Jaji Mkuu, pamoja na *AG*. Nimkumbuke rafiki yangu na mtendaji mzuri sana, Ndugu Elisante Ole Gabriel, Mtendaji wa Mahakama hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa pongezi kidogo za kijumla halafu nitazungumza mambo ambayo nafikiri wengine wanastahili kuiga kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara hii, ambayo tumezungumza sisi tukiwa kwenye Kamati ya Bajeti. Pia nitazungumza kidogo kuhusu Jimbo langu, Mahakama za Mwanzo zilivyokaa, zilivyo duni na zinastahili ukarabati. Mwishoni nitajielekeza kwenye kushauri kwamba ni vizuri *supporting institutions,* mamlaka zingine zinazo-*support* Mahakama kama vile *DPP*, TAKUKURU, Magereza, Polisi, wakachukua hatua za haraka na mikakati ya haraka ili kwenda sambamba na mabadiliko ambayo yamefanyika kwenye Mhimili wa Mahakama, *otherwise* itakuwa haisaidii sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za mwanzo na jumla ni kwamba na Watanzania wafahamu kwamba, Mahakama yetu ina jengo la *state of art* lililojengwa hapa Dodoma. Limejengwa kwa fedha siyo nyingi lakini ni jengo wanasema kwamba kimataifa pengine ni jengo la sita duniani la mahakama ambalo ni zuri zaidi. Jengo la sita *is the state of art building* watu wanaweza wakaja wakaliona, sisi tuliliona kwa kweli ni jengo lenye hadhi ya mahakama na ni jengo ambalo linatisha pia kwenda, utasema nisiende kule, nita-*avoid* kwenda kule kwa sababu unaweza ukapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia pongezi kwa Mahakama hii *especially* kwa ubunifu wa Mtendaji wetu kuhusiana na *mobile courts* (mahakama zinazotembea). Naamini zimeshaanza, zimeanza mijini ila naamini zitasaidia sana kama wataweza kuziteremsha kwenye ngazi ya majimbo yale ambayo yako vijijini, kwa sababu kule juu kunahitajika sana na ndio kwenye ukandamizaji mkubwa na watu hawana fedha za kutafuta haki. Kwa hiyo, naamini kwamba hizi *mobile courts* zitafanya kazi yake na zitashushwa kwenye ngazi za chini kwa sababu zinatoa haki kwa namna ambayo ni gharama nafuu zaidi kwa wale watu ambao wanastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hawa ambao wamezungumza kuhusu *TTS,* huu mfumo ambao sasa ni wa kwanza naamini kwa macho yangu mimi nimekuwa wa kwanza kuona kumbe *artificial intelligence* inaweza ikatumika *very effectively* na naamini kwamba ni ubunifu mzuri, waliweza kufanya jambo hili ambalo limerahisisha sana utoaji na uandikaji wa hukumu na tafsiri za hukumu ambazo zinatolewa baada ya kesi kusikilizwa. Pia inaweka kumbukumbu nzuri zaidi kuliko ambapo kama imefanyika na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni kwamba, kitu ambacho kimetufurahisha sana kwenye Kamati yetu ya Bajeti, ni namna ambavyo watendaji kwenye hiki kitengo utendaji wa Mahakama unafanya katika kutekeleza miradi. Wanaingia kwenye miradi na wakandarasi ambao wanapatikana kwa njia ya kawaida ambayo tunatumia *NeST*. Wakishafanya wanaandika mikataba ambayo inawaruhusu endapo

baada ya mradi kutekelezwa wanaenda kufanya tathmini kuona kwamba, kweli ule mradi umetekelezwa kwa gharama zile walizokubaliana nazo au siyo na mara nyingi unakuta kwamba mradi umetekelezwa kwa gharama ambayo ni *much less,* kwa sababu wametumia vifaa pengine siyo vile. Nashukuru kwamba wanaweza kupata bakaa, wamekuwa wanapata bakaa kubwa kwenye utekelezaji wa miradi yao, bakaa ambayo wanaipeleka kwenye maeneo mengine, kwenye miradi mingine ambayo ilikuwa hata kwenye bajeti pengine haijapata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashangaa na niliwauliza nikasema pengine ninyi kwa sababu ni Mahakama bado hawa jamaa wakandarasi wanaogopa kuwatapeli, kwa sababu sehemu nyingine wakandarasi hawa wanatapeli. Wewe unamwambia ajenge kitu cha gharama hii, *value for money* inashuka, wanatumia tu vitu wanavyotaka kutoka *anywhere.* Nashukuru na nasema kwamba, pengine tujifunze kwao mikataba ya utekelezaji miradi ya maendeleo nayo ifuate mkondo huo ili tuone kweli tunapata thamani ya fedha kwenye miradi yetu. Hilo ni jambo linalofurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi uliotekelezwa au miradi hii ya maboresho iliyotekelezwa kwenye Mahakama imewezesha kumkabidhisha miradi mingi na kesi nyingi zilizokuwa za muda mrefu, alisema 196,895 kesi za zamani. Wakaweza kuondoa 68% wakatekeleza, wakaondoa zile kesi ndani ya kipindi cha Julai kuja Februari, 2024. Ni jambo la kufurahisha sana na nawapongeza watendaji, ni jambo ambalo tunaona kwamba, kweli mwishoni tutaondokana na kesi za muda mrefu. Katika kesi hizi za muda mrefu, miezi sita tu wanasema ni ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya kutoa haki kwenye majimbo yetu imeharibika, wamesema wenzangu, inahitajika zaidi ya Mahakama za Mwanzo 3,000, lakini ziko kama 900, tofauti ni kubwa sana. Naangalia kule jimboni kwetu kwamba, kweli nashukuru kwamba nilipata ukarabati wa mahakama moja ya pale Kilema, lakini mahakama nilizonazo kwanza ni kama nne tu kwenye kata zaidi ya

16, lakini ukweli ni kwamba zimechakaa, ni za miaka, tena huwezi hata kukaa, ni mahali pachafu kabisa, hapafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mtendaji wa Mahakama, akatupatie Mahakama za Mwanzo kwenye Kata ile ya Kirua Vunjo Magharibi hatuna, Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, Kata ya Marangu Mashariki na Magharibi hatuna, Kilema Kusini na Kati hatuna, pamoja na kule Kahe hakuna hata Mahakama moja. Nitaomba Mungu akituwezesha bajeti ile naona amepata 100,005 bilioni ya maendeleo atuangalie huko, atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona changamoto kubwa ambayo imebaki kwa Watanzania sasa kupata *full enjoyment* ya maboresho yanayofanyika kwenye Mahakama zetu na utoaji wa haki. Suala hili la kwamba sasa Mifumo ya Jeshi la Polisi, Mifumo ya *DPP* iko vizuri lakini anatakiwa na yeye achukue hatua. Mifumo ya kule TAKUKURU na Magereza ambayo ndiyo inapeleka kesi kwa Mahakama, basi iboreshwe ipate bajeti za kutosha ili iweze kuendana na *speed* ya Mahakama inavyokwenda. Mandhari ya kutolea haki kwenye maeneo haya ya mahakama kwenye ngazi zote kuanzia Mahakama ya Mwanzo basi iweze kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuona kwamba hivi vituo jumuishi vinakuwa mpaka na sehemu za watoto kucheza. Kuna vitu ambavyo unaanza kuona kweli nchi yetu ni nchi ya kipato cha kati, japokuwa kwenye kiwango cha chini kidogo, lakini kweli tumepiga hatua sana kwenye mambo ya haki. Namshukuru Mungu na atuwezeshe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nawatakieni Wenyeviti wa Kamati zote na Wajumbe wa Kamati zote zinazohusika na masuala haya, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Utawala na wewe mwenyewe nawatakieni kila la kheri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Waheshimiwa Wabunge muda wetu hautatosha kwa mchangiaji wa mwisho kumaliza katika dakika kumi. Tutakaporejea mchana, tutaanza na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha kabisa, baada ya kusema haya, nasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa majina yameshatangazwa, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Zedi na Mheshimiwa Saputu.

Mheshimiwa Kakunda. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anafanya juhudi za

kuboresha Sekta hii ya Sheria nchini, hasa kwenye eneo hili la usimamizi wa vyombo vya utoaji haki. Katika zile 'R' nne za Mheshimiwa Rais, 'R' ya tatu ni *Reform* na hapo kwenye *Reform* ndipo tunapokuta kuna masuala ya kurekebisha sheria na mifumo na hii imefanyika vizuri sana. Tunahitaji mabadiliko mengi ya sheria ili Serikali iweze kujipambanua kufanya kazi vizuri zaidi, ku-*respond* katika mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuwa na sera, lakini kama una sera halafu huna Sheria maana yake ni kwamba, unakuwa huna nguvu ya kutekeleza hiyo sera. Kwa hiyo, kama una sera yoyote ile, lazima hiyo sera iwe *backed* na sheria ili sheria itoe nguvu kwa watekelezaji wa hiyo sera. Nikirejea kwenye maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa tarehe 15 Julai, 2023 siku alipopokea Taarifa ya Tume ya Haki Jinai iliyoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mohamed Chande, alitoa maagizo makuu matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo kuu la kwanza, Rais aliagiza Taasisi zote za Haki Jinai zifanye marekebisho ya mifumo yao ya kiutendaji ili kusimamia vizuri zaidi upatikanaji wa haki kwa wananchi, hilo lilikuwa agizo kuu la kwanza. Nilitegemea katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri angeainisha marekebisho ambayo yameanza kufanyika, kama Rais alivyoagiza, lakini sikusikia. Pengine labda wakati anahitimisha atakuja atueleze hapa kwamba, ni marekebisho gani ambayo yanaendelea kufanyika kupitia utekelezaji wa agizo hili kuu la Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, Mheshimiwa Rais aliagiza taasisi zinazohusika ziheshimu utu wa watuhumiwa wakati wa ukamataji, wakati wa upelelezi pamoja na wakati wa uendeshaji wa mashtaka ili haki ionekane inatendeka. Sasa, hapa kidogo nawasifu Polisi, kule kwenye Polisi kuna maboresho mengi katika utekelezaji wa suala hili. Polisi wamejielimisha sana, wanapokamata wanakamata kwa ustaarabu, wanaendesha upelelezi wao kistaarabu na wanampeleka mtuhumiwa Mahakamani kistaarabu. Kwenye kipengele hicho malalamiko ni machache kwa upande wa polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vyombo vyetu vingine, jinsi *TFS* wanavyokamata watuhumiwa kwenye hifadhi zetu, jinsi wanavyokamata *TAWA*, hata *TANAPA* na vyombo vingine inaleta malalamiko makubwa kwa wananchi na hili ni jambo ambalo ni la kuelimishana tu. Kwa nini Polisi wameweza halafu hawa *TFS* bado wawe na shida kwenye eneo hilo? Kwa hiyo, ni maeneo ambayo ni ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ambayo kwa kweli, inahitajika elimu kubwa iweze kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengine ambao wanahitaji kupata elimu ni Askari Mgambo. Nao wanakamata kule vijijini, wanatumwa na Maafisa Watendaji wa Vijiji, wanatumwa na Maafisa Watendaji wa Kata, wanakamata kwa vipigo, yaani kidogo kuna shida kwenye eneo la ukamataji. Kwa hiyo, elimu inahitajika kwa vyombo vingi vya Serikali ili waboreshe eneo hili la ukamataji, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la tatu ambalo alitoa Mheshimiwa Rais ni Vyombo vya Ulinzi na Usalama vitoe kipaumbele katika kuzuia uhalifu badala ya kutoa kipaumbele katika kukamata, yaani kuviziavizia. Toa kipaumbele katika kuzuia uhalifu badala ya kuvizia kukamata. Nalipongeza tena hapa Jeshi la Polisi, hasa upande wa Polisi Barabarani, wamejikita zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi. Anamwambia kufanya hivi ni kosa la usalama barabarani, kufanya hivi ni kosa, kufanya hivi ni kosa, labda wakirudia hilo gari wanalipiga faini zile za kwenye karatasi. Angalau kidogo upande wa Polisi, lakini vyombo vingine bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Rais alipotoa maagizo kama hayo alikuwa *serious* na Taifa lilimwangalia na lilimwelewa. Kwa hiyo, nategemea sana, watekelezaji sasa nao wamwelewe Mheshimiwa Rais ili waende kama anavyotaka. Mheshimiwa Rais anataka nchi iongozwe vizuri na kuiongoza nchi vizuri ni kupunguza malalamiko ya wananchi, wananchi wasiendelee kuvilalamikia vyombo vya Serikali. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri

aongoze katika utekelezaji wa maagizo hayo ili kweli tuwe na maboresho katika eneo hili la sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu sasa, ukiacha hayo maagizo makuu matatu ya Mheshimiwa Rais. Pendekezo la kwanza, Watanzania wengi wanaoishi vijijini asilimia kubwa ni wahanga wa haki. Mimi ni Mbunge wa vijijini, siyo Mbunge wa mjini kwa hiyo, nina uzoefu zaidi na vijijini. Kule vijijini mfumo wa haki ni kandamizi, yaani ukiitwa kwa Mtendaji wa Kijiji ni hatari, ukiitwa kwa Mtendaji wa Kata ni hatari. Sasa mambo kama haya sidhani kama huku juu wanayafahamu, lakini sisi tunayafahamu. Nafikiri Wabunge wanaotoka vijijini labda wangehusishwa katika mjadala ili kuboresha haki jinai kwenye maeneo ya vijijini kwani limekuwa ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hukumu nyingi kule vijijini zinatolewa na Afisa Mtendaji wa Kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata ndiyo Hakimu kule kijijini. Kule kijijini hakuna Mahakama, hata Baraza la Kata utendaji wake ni wa kusuasua kabisa, wale ndiyo Mahakimu, wale ndiyo wanatoza faini. Wewe umekamatwa ugoni? Lipa shilingi milioni tatu. Umempiga mwenzako? Tena Maafisa Watendaji wa Vijiji wengine wana, wewe umempiga mwenzako? Kosa la kupigana hadharani ni wote ndani na ili kutoka toa shilingi milioni na wewe toa shilingi milioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kengele ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshismiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Kata mengi yana shida katika kusimamia haki katika maeneo ya vijijini. Kwa bahati mbaya sana Mabaraza ya Kata hayakuingizwa kwenye Hadidu za Rejea za ile Tume ya Haki Jinai. Kwa hiyo, ile Ripoti ya Tume ya Haki Jinai haikutoa angalizo wala agizo lolote kuhusu uboreshaji kwenye hili eneo la Mabaraza ya Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mapendekezo mengi sana huko nyuma kwamba, Mabaraza ya Kata yawekwe chini ya Mahakama badala ya kuwa chini ya wanasiasa kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini angalizo na pendekezo hilo

halijafanyiwa kazi na Serikali. Naomba wakati Mheshimiwa Waziri anapokuja alieleze Bunge hili Tukufu ni lini Serikali itafanya uamuzi wa dharura na wa haraka wa kuhamishia Mabaraza ya Kata chini ya Idara ya Mahakama ili kuboresha weledi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama za Mwanzo; kwa mujibu wa Tovuti ya Serikali ya Mahakama, hapa nchini tunazo Mahakama za Mwanzo kama 1,105, kati ya tunazohitaji ambazo ni takribani zaidi ya 3,000. Mahakama ambazo zimekamilika kwa maana ya majengo, watumishi kwa maana ya Mahakimu na watumishi wengine ambao siyo Mahakimu ni Mahakama 84 tu ambazo zina-*qualify* kwamba, kweli hizo ni Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, tuna shida katika eneo hili na naiomba Serikali iweke kipaumbele cha juu katika kujenga Mahakama angalau 100 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi tu walizopanga sijui 76, sijui 60, kwa mwaka zinashindikana kujengwa. Naiomba Serikali iweke kipaumbele cha juu kujenga Mahakama. Sisi Sikonge tunahitaji Mahakama saba katika Wilaya ya Sikonge peke yake, kwa sasa tunayo moja tu ya pale Sikonge Mjini, lakini tunahitaji Mahakama ya Kipili, Kitunda, Kiloleli, Ipole, Igigwa na Nyahua. Hizi ni kata za mbali, wananchi wanapata shida kupata haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kuna namba za dharura ambazo zimetajwa kwenye tovuti ya Serikali, kama wananchi wana dharura yoyote wanaweza wakapiga. Katika orodha ya hizi namba za dharura namba ya Mahakama haipo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie dakika moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba ya dharura ya Mahakama haipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa unachukua muda wa mtu mwingine sasa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo kengele ya pili sasa. Mheshimiwa Zedi, samahani, Mheshimiwa Zedi kuna mtu alitajwa kabla ya mimi kujua, Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Katiba na Sheria. Hii ni mara yangu ya nne nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikichangia Fungu – 55 ambalo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimeingia katika Bunge hili, kama jinsi ambavyo nimesema, nimekuwa nachangia sana katika Tume hii ya Haki za Binadamu na michango yangu mikubwa imejikita kuhusu kuishauri Serikali iweke mkazo au ioneshe umuhimu wa hali ya juu kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Tume hii ya Haki za Binadamu. Niombe, wakati naendelea kuchangia, kila nitakaposema Tume basi ichukuliwe kwamba, namaanisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa ajili ya kukomboa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takribani zaidi ya miaka mitano tume hii haijawahi kutengewa fedha za miradi ya maendeleo kwa mapato ya ndani. Fedha ambazo zimekuwa zikiisaidia tume hii ni fedha za wahisani. Hatukatai kupewa hisani kutoka kwa wenzetu kwa sababu, hata kuaminiwa kama nchi kusaidiwa ni jambo la kushukuru, lakini nilitegemea kwamba, sisi kama nchi tuoneshe mfano kwanza kwa kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Tume hii kwa sababu, mwisho wa siku Tume hii ipo kikatiba kwa ajili ya kulinda na kutetea haki za Watanzania, kwa maana ya Tume ya Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haileti ladha nzuri kwamba, wahisani wawe na uchungu juu ya haki za Watanzania wenzetu. Ndiyo maana hata hii leo nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuikumbusha Serikali na hususan Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kuwa, utakapokuwa unakuja ku-*windup* leo, sina mpango na sijawahi kuwa na mpango wa kushika shilingi *unless otherwise* usinipe maelezo ya kutosha. Mheshimiwa Waziri, atwambie ni kwa nini Serikali haiwezi au inashindwa kutenga fedha hata kama ni kidogo, kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayohusiana na tume hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa dira ya wazi kabisa anaonesha ni namna gani ambavyo nia yake njema ni kuona kila Mtanzania haki yake inalindwa na siyo tu kulindwa, lakini inatetewa popote pale alipo. Kuonesha dira ya Mheshimiwa Rais, ni kuhakikisha Watanzania wanapata haki zao za msingi. Juzi tarehe 22 Aprili, 2024, ilikuwepo hafla pale Chamwino Ikulu ya kuvisha Nishani ya Miaka 60 ya Muungano. Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Taifa amekiri kupokea malalamiko yaliyotolewa na Wabunge ndani ya Bunge hili, lakini pia na wananchi na watumishi wakidai juu ya kikokotoo kwamba, hawaoni kama kinawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hafla hiyo Mheshimiwa Rais amesema waziwazi kwamba, amepokea malalamiko yale na anakwenda kuyafanyia kazi tokea wakati ule ambapo alikuwa anavisha nishani pale. Jambo hili linaonesha wazi kabisa kwamba, Mheshimiwa Rais ana nia njema. Mheshimiwa Rais hataki kusikia haki ya mwananchi yeyote Mtanzania inavunjwa na asiwepo wa kwenda kumsemea wakati Tume hii ipo Kikatiba kwa ajili ya kuwasemea Watanzania kuhakikisha haki zao za msingi zinaweza kulindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee kuchangia nikijikita katika changamoto zinazoikabili taasisi hii muhimu, ambayo ni nyeti na ambapo nimesema dira ya Mheshimiwa Rais juu ya tume hii kwa Watanzania iko wazi kabisa kwa matendo. Changamoto ya kwanza ni kukosekana kwa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume,

ni mambo ya ajabu kabisa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili shida ni nini? Ni nini changamoto inayozuia Tume hii nyeti isiweze kuwa na makao makuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili wanasema ni upungufu wa watumishi 154 ambapo kwa sasa tume hii ina watumishi 150 tu. Haiwezekani tume nyeti namna hii ikawa ina watumishi 154 tu, lakini uhitaji wao ni watumishi 150 wa nyongeza. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa naomba anieleze kinagaubaga shida ni nini? Ni nini tatizo? Waziri aajiri watumishi 150 waende kuungana na watumishi hawa 154 ili mwisho wa siku waende kusaidia nia njema ya Mheshimiwa Rais huko chini vijijini ambako, kama alivyosema Mheshimiwa aliyetangulia kuongea kwamba, haki imepotea. Watu hawapati haki zao za msingi kwa wakati, lakini hata zinapovunjwa waziwazi hakuna wa kuwasemea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tatu wanasema ni kushindwa kufika maeneo ya matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kutokana na ufinyu wa bajeti. Nimesema kwamba shida ni bajeti, pamoja na kupata hela kutoka kwa wahisani, bado nayo ni ndogo haikidhi matakwa ya Tume hii. Sasa tujiulize, ni uvunjwaji wa kiasi gani ambao upo huko chini ambao Tume hii inapaswa kufika maeneo hayo kusaidia na kutoa huduma za kisheria, lakini watumishi hawa hawana hata magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze ni nini mpango mkakati kuhusiana na changamoto hii? Kwa sababu, mwisho wa siku kama watumishi hawa hawawezi kupata hivi vitendea kazi kwenda huko chini kuhakikisha kwamba, wanatimiza wajibu wao, basi Tume hii inakuwa haina haja hata ya kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni kutokuwa na ofisi za matawi katika mikoa 23 ya Tanzania Bara na mikoa minne ya Zanzibar. Hebu tujiulize mbona huko chini tuna Ofisi za Serikali za

Mitaa? Tuna ofisi katika ngazi ya kata, tuna ofisi katika ngazi za wilaya, kuna ofisi katika halmashauri na hadi ngazi za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aeleze shida iko wapi? Tume yake hii kuwa na ofisi, kama wameshindwa ngazi ya vijiji, wameshindwa ngazi ya wilaya, *what about* ngazi ya mkoa? Kingine hii nchi ni moja, Serikali ni moja, wanashindwa nini hata kwenye halmashauri zetu wakatenga ofisi maalum wakawepo hawa watumishi ambao usiku na mchana wataweza kuwafikia wananchi hawa ambao wanahitaji msaada wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea na wewe Tume hii imeomba au niseme inaomba kuidhinishiwa shilingi milioni 522,058,000. Hii Tume siyo kwamba inaomba kwa mapato ya ndani, inategemea pesa hizi zitoke kwa wahisani. Tujaribu kujiuliza, ikitokea wahisani hawa wakasema kwamba kwa sasa hatuna uwezo wa kusaidia, hii tume itafanya kazi namna gani? Itaweza namna gani kutimiza majukumu yake ambayo kimsingi majukumu hayo ni ya kumsaidia Mheshimiwa Rais ambaye usiku na mchana anapopata nafasi ya kuongea na Watanzania anachokisema kwanza, anasema; "Watanzania haki zao zilindwe, haki zao zipatikane kwa haraka." Mwisho wa siku haki wanayoichelewesha ni kama haijapatikana kabisa, hata ikija kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa mbele ku-*wind up* atueleze kinagaubaga kama Wabunge tuelewe ni nini shida inayopelekea mambo yote haya yasiweze kutekelezeka. Wakati nachangia katika bajeti kama hii mwaka jana nilimwomba Mheshimiwa Waziri, nikasema ikiwa CAG analeta ripoti yake hapa Bungeni, ikiwa TAKUKURU wanawasilisha ripoti zao za kiutendaji kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, shida ipo wapi kwa Tume hii ya Haki za Binadamu kuwasilisha ripoti za mwenendo wa uchunguzi wa mambo ambayo wanakwenda kuyachunguza? Ni kwa nini wasituletee hapa Bungeni tukadadavua, tukaangalia nini shida ili mwisho wa siku kama Bunge tuweze kushauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa atueleze ni kwa nini, kwa sababu Tume hii imesema wazi ndani ya Kamati kwamba, wao ripoti zao wanazipeleka kwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ni kwa nini hajazileta humu Bungeni tukazichambua, kama tunavyochambua taarifa za *CAG*? Wakati mwingine Bunge linatoa msimamo wa moja kwa moja, linatoa mapendekezo, linaweka msimamo wa pamoja kwamba jambo hili lazima litekelezwe ndani ya muda fulani, shida ipo wapi, kigugumizi kipo wapi taarifa hizi za Tume hii nyeti kuletwa hapa Bungeni? Mheshimiwa Waziri asiponiambia kiukweli nitashika shilingi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kwenye taarifa ya Tume wameeleza kinagaubaga mafanikio ambayo wao wanayaona ni kama mafanikio. Ukisikiliza huu utekelezaji wa bajeti ambayo wanasema ni mafanikio kwao utaona ni kwa namna gani Tume hii haijaweza kutimiza wajibu wake wa Kikatiba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante...

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana hata vitu ambavyo ni vidogo vya kawaida...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa...

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanaviona... *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Agnesta L. Kaiza aliendelea kuongea bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Zedi, ajiandae Mheshimiwa Saputu. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ambayo inahusu Wizara nyeti kabisa ya Katiba na Sheria. Awali ya yote nitumie fursa hii kwa dhati kabisa ya moyo wangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa kwa kuhakikisha kwamba mifumo ya utoaji haki katika nchi hii inaendelea kuboreka siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria na Kamati yetu tunapokea taarifa za taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na haina shaka yoyote kwa vigezo vyovyote vile ambavyo utatumia, ni kwamba mifumo ya utoaji haki inaendelea kuboreka siku hadi siku. Nakiri kwamba changamoto zote hazijaisha lakini kwa kiwango kikubwa sana mifumo ya utoaji haki imeboreka sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Wazari wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana kwa namna ambavyo anajitoa kuhakikisha kwamba Wizara yake inakwenda vizuri. Pia, nimpongeze sana Naibu Waziri Mheshimiwa Jumanne Sagini, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, kukabidhiwa hii Wizara kama Naibu Waziri na sisi kama Kamati na Wabunge wote tuna matumaini makubwa kwamba atafanya kazi kama kawaida yake kwa weledi wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kama mambo mawili, matatu ya kuzungumzia. Jambo la kwanza ni kuhusu Mpango wa Msaada wa Kisheria wa Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign),* mpango huu haujajulikana sana, lakini ni mpango muhimu sana hasa kwetu sisi Wabunge ambao tunaongoza majimbo ambayo maeneo makubwa ni vijijini. Mpango huu kwetu sisi ni mkombozi mkubwa sana kwa sababu lengo lake kubwa ni kuhakikisha wananchi wetu katika maeneo yetu wanapopata kesi au mashauri ya kisheria basi waweze kupata msaada wa kisheria bure bila gharama yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wengi katika maeneo yetu hasa yale ya vijijini hawawezi kumudu gharama za mawakili.

Gharama za mawakili ni kubwa wanapokuwa na kesi hawawezi kuwalipa mawakili na mwisho wa siku wananchi wetu wengine wanaishia kupata vifungo na hukumu mbalimbali, lakini si kwa sababu ni wakosefu, ni kwa sababu hawana utaalam wa kisheria. Vilevile, hawana uwezo wa kifedha wa kumudu gharama za mawakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu Mpango wa *Mama Samia Legal Aid Campaign* lengo lake ni kuhakikisha kwamba maeneo yetu ya vijijini kunakuwa na watu ambao wanaishi maeneo yale yale, lakini wanapewa elimu ya sheria kwa kiwango fulani. Kazi yao kubwa ni kuwasaidia wananchi bure wale ambao wana uhitaji wa kupata msaada huu wa kisheria pale ambapo wanapata kesi au mashauri mbalimbali ya kimahakama. Kwa hiyo kwangu, jambo hili ni muhimu sana na kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, mwaka jana nilipata fursa ya kuhudhuria uzinduzi wa mojawapo wa hizi programu za *Mama Samia Legal Aid* pale Bariadi, tulikuwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nilikuwa *impressed* sana, namna ambavyo *set up* ilivyokuwa, wananchi wenye shida mbalimbali za kisheria ambao ni wananchi wa kawaida kabisa ambao hawana kabisa uwezo wa kumudu gharama za mawakili, namna ambavyo wanasaidiwa na wanaweza kutoka kwenye shida hiyo ya kuwa na mashauri na kesi mbalimbali. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana, kwamba tulivyokuwa pale na nilimwomba na yeye aliahidi kwamba katika bajeti ya mwaka huu ya fedha ambazo tunazipitisha kwa ajili ya *Mama Samia Legal Aid Campaign* ambayo kuna baadhi ya mikoa nadhani kama 20 ambayo haijafikiwa. Kwa bajeti hii tunayoipitisha ita-*cover* baadhi ya mikoa na nikaomba kwamba Mkoa wa Tabora uwe ni mmojawapo kati ya mikoa ambayo safari hii *Mama Samia Legal Aid Campaign* itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alikubali na tulikubaliana kwamba Mkoa wa Tabora utakuwa ni mmojawapo ambao utapata fedha hizi na *campaign* hiyo ifanyike na Tabora pale shughuli hii itafanyika Wilaya ya Nzega. Pia, tulikubaliana kwamba

itafanyika kwenye Jimbo langu la Bukene. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, tunapitisha hela za *Legal Aid Campaign* naomba ahadi yako kwamba Mkoa wa Tabora utakuwa ni mmojawapo, Wilaya ya Nzega na Jimbo la Bukene ili shughuli hii iende ikafanyike pale na wananchi wangu wa Bukene waweze kupata huduma hii nzuri kabisa ya ushauri wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa wito kwamba Wizara iendelee kusajili hawa watu wa maeneo yetu wanaitwa *Paralegal,* wale watoa msaada wa kisheria ambao wanakaa kwenye kata zetu, waweze kuwa *recruited*, wapewe elimu inayostahili na misaada kama ambavyo tulikuwa tumezungumza na kupewa maeneo ambayo watakuwa wanakaa, watakuwa wanapatikana ili wananchi waweze kufaidika na hii nia njema kabisa ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi hasa wa vijijini wasiokuwa na uwezo wanapata huduma ya kisheria bure, kwa sababu tunajua hawana uwezo wa kuwalipa mawakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni hoja ambayo Mheshimiwa Kakunda ameigusia na Mheshimiwa Agnesta pia ameigusia, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa mtazamo wangu inahitajika elimu kubwa sana kwa wananchi ili wajue hasa hii tunayoisema Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni nini? Inafanya kazi gani? Ipo wapi na inapatikana vipi? Inaonekana kabisa kwamba wananchi wengi hawajui hii ni Tume muhimu sana, sana, sana, kwa sababu ndiyo Tume ambayo inapokea malalamiko yote ya wananchi kuhusu pale ambapo haki za binadamu zimekiukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za binadamu zinaweza zikakiukwa kwa namna nyingi tu tofauti tofauti. Kwa mfano Mheshimiwa Kakunda, ametoa mfano hapa wa maeneo ambayo yanapakana na hifadhi, wakati fulani kwa mfano tu unaweza ukakuta labda Askari wale wa *TFS* wanaingia pale wanafanya mambo ambayo ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Labda kuchukua mazao ya watu, labda kuchukua mali za watu na chakula. Vitu kama hivyo mahali sahihi kwa kupeleka malalamiko hayo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi maeneo yetu ya vijijini hata hawajui hiyo Tume unaipataje, ukipata hilo tatizo unakwenda wapi ili ndiyo ufike Tume ya Haki za Binadamu. Mheshimiwa Agnesta, amezungumza hii Tume inakabiliwa na changamoto nyingi sana. Katika mikoa 31 tuliyonayo hii Tume inapatikana kwenye mikoa mitano tu, maeneo mengine yote haipo na hii Tume kwa takwimu zao wakati fulani wanapokea malalamiko mengi sana, lakini wakipokea malalamiko wanapaswa waende wakayafanyie uchunguzi lakini hawana uwezo kabisa wa kwenda kufanya uchunguzi. Hawana magari, hawana fedha, hawana chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wanapokea malalamiko halafu wanakaa nayo tu, wanayakusanya tu kwa sababu uwezo wa kuyafanyia uchunguzi hawana. Ni ushauri wangu moja kati ya maeneo ambayo yanatakiwa yatengewe fedha na fedha ziende, basi ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kama ambavyo waheshimiwa wengine wamesema, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ana dhamira ya dhati ambayo kila mmoja anaiona waziwazi ya kuhakikisha kwamba uonevu wa namna yoyote ule unakomeshwa kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na maeneo kama ambavyo hasa Mheshimiwa Kakunda, amezungumza maeneo ya vijijini kule wakati fulani kunakuwa na uonevu wa waziwazi wa wananchi kuchukuliwa vitu vyao, kupewa hukumu zingine hazistahiki. Unakuta ofisi za vijiji wakati mwingine zimegeuka kuwa kama Mahakama na mambo kama hayo. Sasa yote hayo yanaweza yakashughulikiwa kama tutakuwa na Tume ya Haki za Binadamu ambayo inafanya kazi ipasavyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, yeye aliyetupa uwezo kwa siku ya leo kuwepo katika Bunge hili kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge. La pili, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa jinsi ambavyo anafanya kazi yake vizuri ya kuliongoza Taifa letu ili kuhakikisha hatma na matumaini ya wananchi wa Tanzania yanafikiwa katika nyanja na sekta mbalimbali. Nisiache kupongeza Wizara nzima ikiongozwa na Waziri wetu na wataalamu wake wote wanaoshughulika na masuala ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu moja kwa moja na changamoto zinazokabili Wizara hii ikiwemo Mahakama. Kwanza suala la ufinyu wa bajeti katika Mahakama na Wizara kwa ujumla, hasa Mahakama. Pale ambapo chombo kama Mahakama kinakosa uwezo wa kufanya shughuli zake za kutoa huduma na utoaji wa haki katika nchi ina maana kwamba suala la utawala bora halipo sawa. Kwa hiyo kitendo chochote cha kujaribu kuinyong'onyeza Mahakama kwa kutoipa bajeti yake kihalisia na jinsi ilivyopitishwa na Bunge na jinsi walivyokusudia, hiyo inamaanisha kwamba ni kudhoofisha utoaji wa haki na kukiuka misingi ya haki za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka kuiasa Serikali katika kutoa fedha kwa ajili ya kuipa Mahakama itoe *OC* kikamilifu ili iwezeshe Mahakama kutekeleza majukumu yake. Itoe pia suala la kuiwezesha Mahakama katika kuhakikisha kwamba imefika katika maeneo ya huduma. Hata hiyo Tume ya Haki za Binadamu kama kweli ukiweza kuunda chombo ambacho hukiwezi kukihudumia au kukipa fedha, basi ina maana gani? Haina maana ya kuwepo, sasa kama Serikali inataka kutuambia hiko chombo hakina maana, basi Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie kwamba kwa nini hiyo Tume ya Haki za Binadamu haipewi fedha zake na kama ina uhalali wa kuwepo kwa mujibu wa Katiba kwa sababu ipo kwenye Katiba kwa

nini hamuipi fedha? Ni suala ambalo Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kama Serikali atujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *OC* lazima Mahakama ipewe, lakini siyo hilo tu pia suala la ukarabati wa Mahakama na ujenzi wa Mahakama. Tunashukuru kwa sababu Serikali imejitahidi kwa kiwango kikubwa sana katika suala la ukarabati wa Mahakama, lakini pia suala la ujenzi wa Mahakama mpya, tunaipongeza Serikali sana katika sehemu hiyo na tunampongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa ujumla ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba ili mtu aweze kuona kwamba haki inaweza ikapatikana na ikatendeka ni pale tu ambapo anafika katika eneo la utoaji wa haki akaona eneo hilo linafaa, anaburudika kwa sababu ni eneo safi, ni eneo ambalo linaonesha kabisa kwamba kuna tafsiri na taswira ya yeye kupata haki zake za msingi. Sasa anapofika katika eneo ambalo ni la utoaji haki na yakawa ni maeneo ambayo ni mabovu, ni machakavu, anaona hivi hapa kweli nitapata haki yangu au ndiyo nimekuja kuangamia. Kwa hiyo, hili nalo ni suala ambalo lazima Serikali ilione kwa mapana yake, kwamba lazima Mahakama zote zile za zamani zikarabatiwe na maeneo mengine ambayo yanahitaji Mahakama yaweze kupata hizo Mahakama, ikiwemo katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi katika Kata ya Bwawani ambayo nilikwishaitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la upungufu wa watumishi. Suala la upungufu wa watumishi kwa maana ya Majaji, naona Mheshimiwa Rais, anajitahidi sana kuteua Majaji mara kwa mara, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini katika kada hii ya Mahakimu naona kama bado kuna changamoto. Pia, Mahakama ipewe uhuru wa kuajiri yenyewe kwa sababu yenyewe ndiyo inajua inahitaji watu kiasi gani na watu ambao wana-*professional* kiasi gani katika uzoefu wa kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo pia cha kutoipa Mahakama uhuru ni kuikiuka ile Ibara ya 4(i) ya Katiba ambayo imezungumzia

kuhusu suala la *separation of power* ambayo ndiyo tunapata masuala ya *executive*, *legislative* na *Judiciary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Serikali yenyewe inashindwa kutoa uhuru kwa Mahakama kwamba iajiri ina maana bado inaingilia *(interference)* ya Mhimili mwingine, inaonesha kwamba hatuheshimu misingi ya haki za kibinadamu. Pale unapogusa sheria yoyote ambayo inataka kuzuia haki yoyote una maana unakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye marekebisho ya sheria mbalimbali, maana ya kuwepo kwa sheria ni kuweka sheria ili iweze kusaidia Taifa katika masuala ya kiuchumi, kijamii na kadhalika, sasa kama kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati lakini bado tunaendelea kuziangalia hatuzirekebishi ina maana kwamba, hapa ndipo ambapo pia tunaendelea kukiuka haki za binadamu na kurudisha uchumi wetu nyuma na kuwafanya wananchi wasiweze kuona Serikali kweli ina nia njema ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria kama Sheria ya Rushwa, *The Prevention and Combating Corruption Act, Cap 329* na marekebisho yake ya mwaka 2022. Sheria hii bado haiipi TAKUKURU uwezo wa kupambana na rushwa kikamilifu. Nikisema hivi waliosoma hiyo sheria na hata *AG* anaweza kukubaliana na mimi kwamba, tunahitajika kufanya marekebisho makubwa sana kwenye hiyo sheria ili kuiwezesha TAKUKURU kuwa na uwezo mkubwa na kuiimarisha ili kuwa na adhabu ambazo zinaendana na suala lenyewe la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo chochote cha kuhujumu mali ya umma si suala la kufumbia macho, ni suala la sisi wote kukazia macho ili tuweze kujenga uchumi ambao Serikali ikikusanya kodi yake pasiwepo na panya yeyote ambaye anaingiza mikono yake kwa sababu ya udhaifu wa sheria, pia kutokuwepo kwa maadili. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ije kuirekebisha sheria hii kwa sababu haipo sawa, imepungua nguvu zake kwa mujibu wa jinsi ambavyo tutaitazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la marekebisho ya sheria mbalimbali kama nilivyosema, sheria za kurekebisha ni nyingi, lakini najaribu kutaja haya ambayo nimeona yapo hapa. Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1979, kwanza nasikitika sana, Mahakama imetoa hukumu kwamba sheria hii irekebishwe na ikatoa na muda *specific,* lakini mpaka leo Serikali imekuwa na kigugumizi, ina maana Serikali haitaki kusikia Mahakama imesema kama Mhimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya wananchi kule nje wanaona kwamba, kumbe Serikali yenyewe kwa sababu ni Serikali inaweza kukataa kutekeleza sheria au kutekeleza hukumu ya Mahakama, ni kwa nini? Nadhani Mheshimiwa Waziri akija hapa katika ku-*windup* atueleze ni kwa nini Serikali haitaki kuhitimisha jambo la kutekeleza hukumu ya Mahakama ya kurekebisha Sheria ya Ndoa kuhusiana na umri wa kuolewa watoto wa kike? Kwa nini na matatizo hayo bado yanaendelea mpaka leo? *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa mzungumzaji kwamba, kuna sheria zinazohusu wanadamu, pia zina maadili ya kidini na maadili mengine ya kibinadamu na utamaduni wao katika nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mollel.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo siipokei, mtoa taarifa labda angesoma sheria na kuunganisha pia Sheria za Dini ya Kikristo, Sheria ya Kiislamu, hakuna sheria inayosema kwamba mtoto wa umri wa miaka 16 au 13 aolewe. Kwa hiyo, naomba mzungumzaji asipotoshe Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hiyo ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria hiyo naomba irekebishwe na Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini Serikali haitaki kurekebisha sheria hii au inakataa uamuzi wa Mahakama ambapo Mahakama ambayo ndiyo chombo pekee kichopewa uwezo wa kutafsiri sheria na kutoa haki katika Taifa hili, *otherwise* tuambiwe kuna namna nyingine ambayo tunaweza tukapata haki kwa kupitia chombo kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kusema Sheria ya Wanyamapori. Sheria ya Wanyamapori imekuwa na yenyewe ni sheria kandamizi, wanyamapori wana thamani zaidi kuliko binadamu. Binadamu anapouawa fidia anayopewa sijui ni shilingi 500,000, sijui 1,000,000 lakini mnyama akiuawa au akikutwa mtu na ngozi ina maana atapigwa faini ya uhaini ya kuua mnyama ambayo atatozwa faini labda mamilioni ya shilingi au akafungwa hata maisha, hapa binadamu haangaliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sheria nayo ni ya kuitazama ili fidia ya raia nayo iongezeke kwa kiwango ambacho hakiwezi kumlipa binadamu, lakini kitoe matumaini kwamba, angalau binadamu nao wameonekana ni watu. Kwa hiyo, sheria hii nayo inatakiwa kurekebishwa kwa sababu haitendi haki kwa wananchi wa Tanzania, tunaona wanyama wana thamani zaidi ya binadamu au Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mabaraza ya Ardhi kwa maana ya *Land Disputes Act. Cap.* 216 na marekebisho ya 2019 na yenyewe inatakiwa irekebishwe. Mabaraza haya hayatoi haki kwa wananchi wa Tanzania. Mabaraza haya yenyewe katika mikoa, unaweza kukuta kwa mfano, Mkoa wa Arusha, Mabaraza ya Ardhi yapo mawili katika wilaya saba, sasa haki inapatikana wapi hapo na migogoro ya ardhi ni mingi? Naomba sheria hii irekebishe Mabaraza yote ya Ardhi yapitishwe kwenye mkondo wa Kimahakama, kwa sababu itatusaidia sana kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata haki na kuepukana na mambo ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya, kesi inapigwa kwa mara moja miezi sita. Mtu anakaa miezi sita ndiyo aende kwenye kesi au mwaka mzima ndiyo aende kwenye kesi. Sasa hiyo ni kesi au ni kitu gani? Hiyo ni kudhulumu na ni kwamba, sisi kwa upande wa Sheria tunasema *the right delayed is the right denied* kwamba, haki iliyochelewa kutolewa ni sawa na haki iliyonyimwa. Sasa sidhani kama Serikali inakusudia kufanya hivyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili hiyo…

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia dakika moja kidogo tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili, utachukua muda wa mwingine.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Chaya, ajiandae Mheshimiwa Kilumbe. *(Makofi)*

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii vilevile kukushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia leo kwenye hii Wizara ya Katiba na Sheria. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Balozi Dkt. Pindi Chana, Naibu Waziri kaka yangu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nachukua nafasi hii vilevile kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, mtani wangu Mary Makondo, Mtendaji Mkuu wa Mahakama Profesa Ole Gabriel, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, leo naomba nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika maeneo mawili yanayoendana na masuala ya Katiba na Sheria. Mwaka jana Mheshimiwa Rais aliunda

Tume ya Rais ya Haki Jinai, ambayo hiyo Tume imekuja na mapendekezo 18. Hayo mapendekezo yote yamejikita katika kuhakikisha kwamba, wananchi wetu hususani wananchi wa kawaida wanapata fursa ya kupata haki ya kusikilizwa kwenye masuala ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni eneo la muhimu sana ambalo kimsingi ni utekelezaji wa zile *4Rs* za Mheshimiwa Rais, kwa upande wa *(reform)* maboresho. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa sababu mapendekezo haya 18, yanaenda kuleta mabadiliko makubwa sana kwa wananchi wetu hususani katika utoaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ambalo ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais, ni ile Kampeni yake ya Mama Samia *Legal Aid Campaign,* Kampeni ya Kisheria ya Mama Samia. Wachangiaji wengi wameeleza huu ni ubunifu mkubwa ambao sasa tunaenda kuwafikia wananchi wa kawaida kule chini, ndugu zetu wa kawaida kule chini wanapata shida sana za wapi wanaweza kupata misaada ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia kampeni hii tumeona, hata Singida alikuja Waziri akazindua, sasa wananchi wetu wa kutoka vijijini, Vijiji vya Sanza, Makuru, Kintinku na kwingineko sasa watakuwa na usaidizi wa masuala ya kisheria. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, hii ni mojawapo ya utekelezaji wa zile *4Rs, (Reform)*. Namwomba Waziri sasa hii kampeni ya Rais iende ikafanye kazi. Tunataka kuona matokeo, tunataka kuona wananchi wetu wanatetewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hizo shukrani, nina maeneo makubwa mawili ningependa kuchangia leo. Eneo la kwanza, ni kuhusu ufaulu wa *Law School,* wote ni mashahidi kwenye mitandao ya kijamii tulishuhudia kelele nyingi sana za wanachuo na wanafunzi kuhusu matokeo *ya Law School.* Naomba nirejee taarifa za mwaka 2021/2022 kwa *batch* ya 33 ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliofanya mitihani walikuwa 633, kati ya wale wanafunzi 633, wanafunzi 26 tu waliofanya mtihani kwa mara moja *(first sitting)* ndiyo waliofaulu mtihani, hii ni sawa na asilimia nne. Kati ya wale wanafunzi 633, wanafunzi 342 walitakiwa kurudia masomo yao *(supplementary)* ambao ni sawa na 54%, lakini kati ya wale wanafunzi 633, wanafunzi 265 walifeli kabisa, walikuwa *(discontinued)* na hawa walitakiwa kurudia masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uwekezaji wa nchi kama tuna wanafunzi 633 waliolipa ada *then* asilimia nne tu ndiyo wanafaulu kuna tatizo sehemu. Sasa tatizo ni nini? *Analysis* yangu inanionesha kuna maeneo matatu ambayo inawezekana ikawa ni *challenge*. Kwanza ni vyuo vyetu havifanani, ukiacha kwamba *TCU* ina-*regulate*, ina-*standardize* vyuo vyetu, bado vyuo vyetu havifanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto anayetoka *UDSM*, anayetoka Mzumbe, anayetoka *SAUT* na kwingine amesoma sheria, kwingine wanasoma miaka mitatu, kwingine miaka minne hawafanani. Hawafanani *capacities* vilevile ufundishaji haufanani. Kwa hiyo, nimwombe Waziri wa Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda, wakafanye utafiti wajue kwa nini wanafunzi wanafeli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine utafiti wangu umenionesha kwamba, wanafunzi wanafanya masomo 11 ndani ya mwaka mmoja na wana miezi sita ya kuingia darasani na miezi sita ya kwenda kwa ajili ya mafunzo. Kitu nilichojifunza kuna wanafunzi wengine wanakutana na yale masomo 11 kwa sababu ya utofauti wa vyuo anakutana nalo hilo somo mara ya kwanza *Law School,* hilo ni tatizo. Kwa hiyo, ndiyo maana tunajikuta ni asilimia nne tu ya wale ambao wamejiunga kwa ajili ya *Law School* ndiyo wanaofaulu, kwa hiyo, kuna tatizo sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tatu, taarifa nilizopata kutoka kwa hawa ambao waliwahi kufanya hii mitihani, ule utoaji wa zile *regular assessment, continuous assessment* matokeo yake unachelewa. Mtu anafanya *test one,* anaenda *test two* na anaenda

*test three* hajawahi kupewa matokeo, sasa mtu ataji-*assess* vipi kama amefaulu ili aweze ku-*make progress*, hilo nalo ni tatizo. Kwa hiyo, ni eneo ambalo ningeshauri waweze kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri nini? Jambo la kwanza, utafiti unaonesha kwamba ile asilimia nne inawezekana ikawa ni asilimia sahihi, kwa sababu wanafunzi wetu wanatoka kwenye vyuo tofauti tofauti, ambao wamefundishwa tofauti tofauti, vyuo vyenye uwekezaji tofauti tofauti na walimu wenye *capacity* tofauti tofauti. Tunahitaji kuwa na *entry exam,* tuwachuje kabla hawajaingia kwenye *Law School* ili tupate wale ambao wataenda kwenye *Law School,* kwa sababu haya malalamiko tunayoyapata kwamba tunafeli, tunaonewa nadhani tatizo ni *competency* ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutawezaje kuwachuja tuwapate wale watu wanaoenda kwenye *Law School,* lazima tuwe na kitu kinaitwa *screening test,* tuwa-*screen* ili tuwapate. Hivi ni lazima kila mwanafunzi aende *Law School?* Kuna *professional* nyingine, kuna kazi nyingine hazihitaji mtu awe na *Law School.* Kwa hiyo, tuwapate wale wenye sifa ili wakajiunge na *Law School. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Waziri, hebu tupitie mtaala wa *Law School,* tujiridhishe kile tunachoenda kuwapa wanafunzi wetu, je, wanastahili? Niliwahi kujiuliza kitu kimoja *Law School should be a non-academic program.* Walishasoma miaka minne huko walishawa-*pump* na *theory* na *principles,* tunahitaji waende kuwenye *practice.* Kwa hiyo, *it is a non-academic program*. Ndiyo maana inafundishwa na watu waliobobea walioko kwenye *field* kama Majaji na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie huu mtaala wetu tusije tukarudia yale yale tuliyomfundisha *year one* akiwa *UDSM, year two* akiwa Mzumbe, tunataka kuyarudisha tena kwenye *Law School*. Tutakuwa hatuwatendei haki, tuwafundishe vitu vitakavyowajenga *professional* yao. Kwa hiyo, hilo ni eneo la pili ambalo nashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nimelieleza, tutumie walimu ambao kwa kweli ni wabobezi, wamekaa *field*, kwa sababu lengo letu hatutaki kurudia *theories* tulizowafundisha. Tunataka kuwafundisha kazi na ili kumfundisha kazi, watumie mtu ambaye yupo kazini na hilo najua wanalifanya lakini nasisitiza waendelee kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni ombi, kule kwangu Manyoni, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametujengea Mahakama ya kisasa ya Wilaya pale Manyoni, haijawahi kutokea, pia ametujengea Mahakama ya Mwanzo ambayo imeungana na Jengo la Mahakama ya Wilaya ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama zetu za Mwanzo nyingi zina hali mbaya. Bahati mbaya zaidi wananchi wetu wanapata shida wanatoka umbali mrefu kutembea kwenda kutafuta huduma za kisheria. Kwa mfano, Sanza hawana Mahakama kule, kuna jengo ni chumba kimoja, Heka, Chikola, Nkonko, Kintinku, hawana Mahakama za Mwanzo. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo haya niliyoyataja eneo la Sanza, eneo la Nkonko, eneo la Chikola na eneo la Kitinku, tunaomba aje atuboreshee majengo ya Mahakama. Mheshimiwa Rais, anasisitiza *4Rs* katika ile *R* ya (*Reform)* mojawapo lazima tuweke maboresho kwenye Mahakama zetu. Tuwe na Mahakimu wa kutosha, vilevile majengo yetu yavutie. Mtu hata anapoenda kudai haki awe kwenye mazingira salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni suala la Watumishi wa Mahakama, tuna upungufu mkubwa sana wa Watumishi wa Mahakama hususani pale Manyoni. Lingine unamkuta Hakimu wa Wilaya amepanga mtaani, Hakimu wa Wilaya amepanga mtaani na kwenye ile nyumba aliyopanga *landlord* ana kijana ambaye ni kibaka, kila siku anapelekwa Polisi, Mahakamani, huyo Hakimu atatenda haki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri tuwajengee nyumba Mahakimu wa Wilaya hasa wale Viongozi wa Wilaya wawe kwenye mazingira salama, kuwaweka mitaani siyo

salama kwao, *it is very risk*. Kwa hiyo, ningeshauri Mahakimu wale Viongozi wa Wilaya tuwaangalie, tuwajengee nyumba kama tunavyojenga Nyumba za Wakurugenzi, tunavyojenga Nyumba za Viongozi wengine Wakuu wa Wilaya, Mahakimu wa Wilaya nao tuwajengee nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, wajiandae Mheshimiwa Condester Sichalwe na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Mheshimiwa Kilumbe hayupo? Mheshimiwa Sichalwe hayupo? Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Katiba na Sheria. Nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wanaishi kwa haki, demokrasia, umoja na wanaishi kulingana na sheria zinavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nitakuwa nipo sahihi nikisema kwamba, mwanahaki za binadamu namba moja Tanzania kwa sasa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hili kwa kweli amefanikiwa kwa ukubwa sana, ameanzisha Tume ya Haki Jinai ambapo maoni ya Watanzania yamechukuliwa na yanafanyiwa kazi. Bunge hili hili tumepitisha Sheria za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, tunaendelea kufanya mabadiliko mbalimbali ya sheria kuhakikisha kwamba, demokrasia na haki za binadamu Tanzania zinaendelea kulindwa. Naipongeza sana Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kufanya kuhakikisha kwamba Watanzania wote haki zao zinalindwa na kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchango wangu wa leo utajikita kwenye Fungu Namba 59 la Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Tume hii imeanzishwa chini ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria,

Sura Na. 171 ambayo tulianzisha tangu mwaka 1983. Kati ya majukumu makuu kabisa ya Tume hii, ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, inaziangalia na kuzitazama Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili ziendane na mazingira ya wakati huo na kuhakikisha kwamba, zinaendana na mabadiliko endelevu ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka uliopita taarifa zinatuonesha Tume hii ilitengewe shilingi bilioni 5.1, lakini mpaka tunavyozungumza Tume hii imepewa fedha kwa 53% tu ambayo ni sawa na shilingi bilioni 2.6. Changamoto ya ukosefu wa fedha katika Tume hii ya Kurekebisha Sheria ndiyo ambayo inatufanya mpaka sasa tunakuwa na sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria nyingi sana amezitaja Mheshimiwa Noah, akionesha kuna Sheria ya Ndoa ambayo mpaka sasa haijarekebishwa na Bunge hili, kuna Sheria za Ardhi ambazo zina migogoro, kuna Sheria za Wanyamapori ambazo zina migogoro kwa wananchi. Sheria hizo zingeweza kubadilishwa kwa wakati kama tungeipatia fedha za kutosha Tume hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba kushauri, tuipatie fedha za kutosha Tume hii ili mabadiliko yafanyike kwa wakati. Nitatoa mfano, leo hii kwenye Sheria zetu za Utumishi wa Umma, tuna mifumo ambayo ni *centralized.* Tumeianzisha mifumo hii kwa sheria za zamani na sera tunayoitumia sasa pia ni ya muda mrefu sana, sheria hii imeshakuwa na upungufu mkubwa sana kulingana na mazingira tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna mfumo *centralized* wa kupata waajiriwa wote Serikalini. Ajira zinatangazwa, watu wanaomba na tunakuwa na mfumo mmoja wa kuchakata nafasi hizi za ajira, lakini tumeona na tafiti mbalimbali zimefanyika zinazoonesha Tanzania ya sasa inahitaji mfumo *decentralized*. Inahitaji ajira zinapotangazwa zishushwe kwenye maeneo yetu, kama ni mikoa au wilaya ili watu wote Watanzania waweze kugawana nafasi hizi za ajira kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa Sera yake ya Elimu Bure na kwa kuendelea kuongeza mikopo kwenye elimu ya juu. Sasa hivi hakuna mkoa usio na wasomi, hakuna wilaya isiyo na wasomi, hakuna kata isiyo na wasomi. Wasomi wametapakaa kila sehemu. Tunahitaji mabadiliko ya sheria na sera zetu ili zinapotangazwa ajira zishushwe kwenye mikoa na wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano, kuna nafasi hapa zimetangazwa kama nafasi 46,000 tukigawana kwa mikoa 26 tunapata karibu kila mkoa nafasi 1,700. Kwa Mkoa wangu wa Mwanza ambao una wilaya saba tukigawana hizo nafasi 1,700 kila wilaya inaondoka na nafasi zaidi ya 250. Itakuwa ni ngumu sana kwa kijana yeyote au mtu yeyote aliyeomba ajira kulalamikia mfumo wa upatikanaji wa ajira ilihali hata kama hajapata yeye anajua katika wilaya yake au kata yake kuna watu kadhaa wamepata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatuondolea sana migogoro mingi kati yetu sisi na wale ambao tunawaongoza. Pia, katika hili hili la kurekebisha sheria, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona kwamba kuna haja ya kufanya mapitio katika ile mikopo ya 10%. Naipongeza sana Serikali katika bajeti ambayo imesomwa na TAMISEMI hapa wiki iliyopita, wametuambia kwamba tunarudisha ile mikopo ya 10% kwa halmashauri kadhaa kwa mfumo mpya na halmashauri nyingine kwa mfumo ule ambao utaangaliwa kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii tuliipitisha kwa Sheria ya Bunge. Tunahitaji Sheria iletwe hapa Bungeni ili tubadilishe kuruhusu mikopo hii kuanza kupitia benki. Leo hii tumetoa tamko hapa lakini tutakuwa *challenged* tunapitiaje benki bila kurekebisha sheria? Tutenge fedha kwa Tume hii ya Kurekebisha Sheria ili walete mabadiliko ya Sheria ya Fedha katika halmashauri zetu tuweze kuanzisha huu mfumo mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumekuwa tunapiga kelele sana kwamba, tunahitaji sheria iletwe kwa ajili ya kuwapa kipaumbele wale

wanaojitolea katika halmashauri zetu wapewe kipaumbele pale ambapo ajira zitatangazwa. Sheria hii imekuwa ya muda mrefu sana tunajua itakuja lakini haiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Wizara hii na chini ya Tume hii iangalie sheria tulizonazo izirekebishe ili mtu yeyote anayeomba kujitolea kupata *mentorship* kwenye ofisi zetu, kwanza waruhusiwe. Kwa sababu kwa mfumo uliopo sasa hivi, mtu anaomba kujitolea kama vile anaomba kulipwa mshahara. Anaomba kufanya kazi bure, anaomba kujitolea kwa muda wake, lakini ataongeza pia uzalishaji na utoaji wa huduma lakini wanapata usumbufu sana. Tuletewe sheria watu waruhusiwe kujitolea, lakini wale wanaojitolea wapewe kipaumbele kwenye ajira zinapotangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yatawezekana kama tukiiwezesha Tume hii ya Kurekebisha Sheria chini ya Fungu hili 59 kupata fedha zake kwa asilimia zote 100. Sheria zetu zianze kuendana na mazingira tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, misingi ya umoja, amani na uhuru tuliyonayo katika nchi yetu hii ilijengwa, haikutokea tu na ilijengwa kuanzia katika ngazi za familia. Tuna haja ya kuilinda sana taasisi ya familia. Kwa takwimu zilizopo sasa hivi inaonekana kwamba *divorce rate* kwenye nchi yetu inaongezeka kwa kasi na ni kwa kasi ambayo inatia mashaka ya ustahimilivu wa taasisi hii ya familia. Moja ya sababu ambazo zimeonekana zinaongeza rate ya *divorce* au talaka kwenye nchi yetu, ni umbali wa waajiriwa wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baba ameajiriwa Mwanza, mama kaajiriwa Mpanda, mama kaajiriwa Mara, baba kaajiriwa Rukwa. Hii ndiyo inaongeza wingi wa talaka. Kama tunataka kuhakikisha watoto wetu wanalelewa katika malezi bora tuhakikishe kwamba misingi ya mila na tamaduni zetu katika nchi hii zinalindwa, tuhakikishe kama Serikali inalinda taasisi hii ya familia. Tupitishe sheria hapa, tuzipitie sheria zetu za utumishi ili kuwepo na misingi inayobana utumishi wa umma katika kulinda familia. Kama baba ameajiriwa Mwanza hata kama ni wilaya tofauti, mama naye asogezwe karibu ili kulinda familia

na taasisi hii kuhakikisha kwamba tunakuwa na kesho ya watoto wetu iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza kuipongeza Wizara yetu ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuongea leo tukiwa tunajadili Wizara ya Katiba na Sheria, nimeona chama changu wameandamana hapa Dodoma Bungeni na moja kati ya kilio chao kikubwa kilikuwa ni Katiba mpya. Nimeingia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 16 nimeona mchakato unakwenda kwa kasi kweli kweli kuhakikisha kwamba tunapata katiba mpya. Pia, naona kuna *awareness* kubwa inafanyika kupitia makongamano, semina, warsha na kupitia hii huduma yetu ya msaada wa kisheria unaotokana na *Mama Samia Legal Aid. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watutambue na sisi kwamba na sisi tunawasaidia kutoa elimu kupitia maandamano haya ambayo wameyaruhusu na wanaona ni ya amani na tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza, nataka niseme jambo moja kubwa ambalo kiukweli Mheshimiwa Naibu Waziri anatoka Kanda ya Ziwa na wale Wabunge ambao wanatoka Kanda ya Ziwa tuna changamoto kubwa sana ya mimba na ndoa za utotoni. Wabunge wenzangu wengine wanasema ni za udogoni kwa sababu mtoto hawezi kubeba mimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye bajeti iliyopita, Wizara hapa tuliiomba kwa dhati na bahati nzuri aliyeshika shilingi sasa hivi ni

Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab. Wakaweka *commitment* kubwa kweli kweli kwamba wataleta mabadiliko ya sheria na wakatuita kwenye kongamano kubwa ambalo lilikuwa *live* Tanzania nzima wanaona. Tukawaleta wazee wetu kutoka maeneo mbalimbali; waganga wa jadi waliletwa, viongozi wa kimila waliletwa na viongozi wa dini zote waliletwa wakatoa maoni yao. Mkwamo upo wapi? Shida ni nini na kwa nini hawaleti mabadiliko ya sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema humu Bungeni, hata ule mchakato wenyewe wa kusema wanakwenda kukusanya maoni ya wadau ni kinyume na taratibu ya utungaji wa sheria. Mahakama ilishasema kwamba vifungu vile ni batili na watoto hawa wanaishi kwenye mazingira magumu. Walichotakiwa kufanya ni kuleta mabadiliko ya Sheria Bungeni na si kwenda kukusanya maoni ya wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge kwa sababu Mungu alitujalia busara na hekima tukamruhusu Waziri akajiridhishe. Alikuwepo Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro hapo, leo Mawaziri wamekuja wengine, lakini kiukweli niwaambie kwenye hili kidogo tutatofautiana. Tunataka sheria inayoruhusu mtoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake iletwe hapa tuifanyie mabadiliko na watoto hawa waendelee kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji mkubwa unafanyika kwa watoto hawa, tumerudisha *re-entry program,* Mheshimiwa Rais ameruhusu watoto warudi shuleni hata kama wamepata ujauzito. Tumetengeneza shule nyingi na madarasa mengi, watoto wa kike wanapewa hamasa kubwa ya kujiunga kwenye masomo hasa masomo ya sayansi. Kwa nini tunawawekea kikwazo hiki? Sisi kule kwetu Shinyanga tupo kwenye *top three*, sio sifa kuwa na watoto ambao wanaolewa katika umri mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa tukiwa tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu. Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu wake na *Attorney General* wanajua taratibu

za utunzi wa sheria. Wizara ya TAMISEMI imekasimiwa mamlaka ya kutunga kanuni za uchaguzi, lakini kasma hiyo waliyopewa wanatakiwa kuleta Bungeni pamoja na kwamba tumewakasimu, wanatakiwa walete hapa kwa ajili ya Bunge kufanya *scrutinization*. Hawajaleta kanuni zile tuweze kuona, *rules* za mchezo ule zinakwendaje? Wanaendeshaje uchaguzi wa Serikali za Mitaa? Hakuna Mbunge hata mmoja hapa anayefahamu uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaendeshwa kwa kanuni za aina gani na sasa hivi wameshaanza kufanya uhuishaji wa daftari la mpiga kura; hawatutendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, watuletee kanuni tuzione na nasema hivyo kwa uzoefu. Mwaka 2018, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilikuwa mbaya sana na zililalamikiwa sana. Wazilete Bungeni tuweze kuzichambua na turidhike nazo, tujue kile ambacho tumekasimisha Wizara ya TAMISEMI kuweza kusimamia uchaguzi kupitia Tume ya Uchaguzi kinafanyika kama ambavyo Bunge linatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha msaada wa kisheria kupitia *Mama Samia Legal Aid Campaign*. Nataka niseme labda kuna changamoto fulani, tafiti haikufanyika ya namna ya utekelezaji wa zoezi hili ndiyo maana tunaona hata utekelezaji wenyewe unasuasua. Kusema kwamba watumishi wa Serikali au hii Idara ya Serikali inahusika na mambo ya *legal aid* ndiyo iende ikafanye *legal aid,* ikaweke mahema kule chini kwenye mikoa, ni kujidanganya wenyewe. Mategemeo ya Watanzania yalikuwa makubwa sana hasa ya kada ya sheria, tuna mawakili wengi, tuna wanasheria wengi, ni kwa nini wanatoa watu Wizarani? Ni kwa nini wanatoa watu kwenye maofisi yao kwenda kufanya hiyo kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mpaka leo takribani mwaka mzima umepita wameenda kwenye mikoa sita tu kati ya mikoa 26 ambayo wametakiwa kuifikia. Hebu washirikishe wanasheria, wamesema wenzangu hapa vizuri, nilisema mimi nisiseme kuhusu *law school*, wamesema vizuri wenzangu. Kila mwaka tunatoa wanafunzi

*law school* maelfu na maelfu, wale wanafunzi wapo mitaani, hawana kazi, lakini uwezo wa kutoa ushauri wa kisheria wanaweza. Kwa nini wasifanye kazi hiyo badala yake watumishi wa Serikali wanakwenda kufanya wenyewe? Dhana ya *PPP* ipo wapi katika jambo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa nia ya dhati, wapo wanasheria wanaoweza kufanya kazi hii ya *legal aid,* zipo *NGOs.* Kazi ya Serikali ibaki kuwa ya uratibu, kuratibu kwamba kile kinachokwenda kuwasilishwa kwa wananchi hakipotoshi. Hata ukiangalia kwenye misingi tu ya dhana ya haki, yaani hizo kesi nyingi zilizopo kule ni kesi za ardhi, ni kesi zinazohusiana na mambo ya mirathi ambazo wakati mwingine Serikali ni sehemu ya watu wanaoshtakiwa au kulaumiwa kwenye kesi hizo. Wanakwenda kutoa msaada wa kisheria, wao ndiyo Serikali, wanatoa msaada wa kisheria, wakipelekwa mahakamani wao ndiyo washtakiwa. Hapo haki itatendekaje? Kwa hiyo naomba kwa nia ya dhati hii kazi Serikali ibaki kwenye dhana ya uratibu na wabaki wanasheria wengine na si lazima wawe mawakili, hata wanasheria wa kawaida waweze kufanya kazi hiyo ya *legal aid campaign. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana nimeona mwalimu wangu Sisti Mramba amekuwa ndiyo Mkuu wa Chuo hiki cha mafunzo kwa vitendo *(Law school)* cha sheria. Naomba, najua kuna utafiti ulifanyika kuhusiana na suala la *Law School* na tulitukanwa sana tukaitwa sisi vilaza. Niseme darasa langu mimi nililoingia mwaka wa kwanza sheria, mtu aliyefaulu kwa ufaulu wa chini alikuwa na *division* 1.9 na hakukuwa na kilaza pale, tukaambiwa sisi ni vilaza. Naomba utafiti ufanyike, kwa nini wanaingia 600 wanafaulu wanafunzi 14? Ufanyike utafiti na najua sina wasiwasi na mwalimu wangu huyu najua atakwenda kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kuna watu wanasoma pale *Law School*, mtu anatoka pale ana *supplementary* amefeli, lakini akiamua kuahirisha asiendelee na *Law School* aende *masters,* kule *Masters* masomo hayo anapata A, masomo hayo hayo kwenye *masters* anapata B+. Iweje leo uite huyu mtu ni kilaza? Umepewa *cream of the nation* uifundishe, wanafeli 90% ya wanafunzi halafu

unasema wewe ni mwalimu. Huu ni uongo, ningeomba suala hili tusifanye utafiti wa kisiasa. Ufanyike utafiti wa kitaalam kwa sababu hakuna kilaza anayesoma sheria kwenye nchi hii. Kila anayesoma sheria kwenye nchi hii ni mtu ambaye alipata wastani wa juu wa ufaulu *form four*, *form six* na mpaka ameweza kuingia chuo kikuu alifaulu vizuri. Huko ni kulionea eneo la sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la bajeti ya Mahakama na labda hili tunaweza kuwa tunalichukulia kwa wepesi. Mahakama ndiyo chombo cha juu cha utoaji wa haki nchini. Katika watumishi wa Mahakama hawawezi kwenda kuomba kwa mtu, hawawezi kufadhiliwa na mtu, hawawezi kupewa asante na mtu. Leo Bunge hili limekaa limepitisha bajeti tunasema wapelekewe fedha kwa ajili ya maendeleo, kweli tunapeleka 24% tu ya bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi haya majengo mazuri ambayo tunayajenga leo katika nchi hii ambayo ni kwa ajili ya Mahakama, bila watendaji wa Mahakama, bila vifaa vya utendaji wa Mahakama, haki itatolewaje? Hili jambo niseme na niombe kwa dhati tupeleke fedha, hawa watu tusiwaweke kwenye majaribu na ndiyo maana ni moja kati ya mhimili ambao umetengenezwa kikatiba; maana yake wanalindwa kikatiba. Sasa tusiwavunjie ile kinga yao ya kikatiba kuwaingiza kwenye vishawishi. Hawana makazi wana changamoto, hawapewi vipaumbele mbalimbali, hawapati hizi fursa ambazo tunazipata sisi kwenye mihimili mingine, lakini hata lile la kwao la msingi la kikatiba wanashindwa kupelekewa bajeti kweli ili wasimamie?

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Shinyanga tuna jengo zuri sana pale kwetu la Mahakama, limejengwa la kisasa lakini ukiangalia upungufu wa mahakimu na majaji, hata ripoti yao wenyewe wanasema hapa. Wanasema upungufu wa watumishi, katika watumishi 6,247 wanaotakiwa kuna upungufu wa watumishi 1,562 na kwa bahati mbaya suala la mtumishi wa Mahakama halina kusema atafanya msaidizi. Hakimu ni hakimu, lazima akae hakimu aamue kesi. Ukisema leo kuna upungufu wa mahakimu maana yake pale haki haitatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upungufu wanaousema kwenye mahakama za mwanzo, wanatakiwa wawepo watumishi 3,999, leo wana watumishi 960 sawa na 24% tu ya watumishi wanaotakiwa katika Mahakama hizi. Hivi unategemea kupata matokeo ya aina gani? Unategemea haki itatendeka vipi? Ndiyo maana leo mtu anaona kuliko niendelee kuzungushwa Mahakamani ni afadhali nisubiri mikutano ya wanasiasa niende nikashtaki pale, kwa sababu anaona huku Mahakamani kuna ukiritimba, anaona huku Mahakamani mambo hayaendi, ni afadhali niende kwenye mikutano ya wanasiasa. Matokeo yake yule mtu hatopata haki yake na unatengeneza mazingira ya rushwa katika kumhudumia mtu yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka haraka kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Kiukweli hii Tume ipo kikatiba na Tume hii hata kwenye mikataba ya kimataifa ambayo tumekubaliana ni Tume ya muhimu. Inatakiwa itoe ripoti ambayo ripoti hiyo itakuwa ni ya wazi, kila mtu anaweza kuiona. Leo hii ukiuliza Wabunge humu ndani ambao wanajua hata ripoti ya mwaka jana tu ya Tume ya Haki za Binadamu ni wachache sana. Sisi tunataka kufahamu hiyo ripoti na ni moja kati ya ripoti ambayo kiukweli ikitolewa hadharani itam-*brand* vizuri sana Mheshimiwa Rais. Kwa sababu katika kipindi ambacho Haki za Binadamu zimesimamiwa na kutekelezwa vyema ni wakati huu ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ripoti hii imebaki kukaa kwenye *draw* za Ofisi za Katiba na Sheria? Ni kwa nini? Nasisitiza na amesema vizuri sana Mheshimiwa Agnesta wakati anachangia. Wabunge tuletewe ripoti hii na ikibidi utengwe muda wa Bunge kwa ajili ya kujadili na kupitia ripoti hii. Kwa sababu wakati mwingine mambo mazuri yanafanyika hayajulikani kwa sababu hayasemwi na kwa sababu hayajulikani kwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize kwa nia ya dhati, tuletewe ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu lakini tuimarishe Kitengo cha Tume ya Haki za Binadamu. Malalamiko hayawezi kuwa mengi kama Kitengo hiki kitafanya kazi na *of course, as a matter of fact* hata

hiyo kazi inayofanywa na *Mama Samia Legal Aid Campaign,* hawa watu wa Tume ya Haki za Binadamu wanatakiwa kuwa sehemu ya hawa watu wanaokwenda huko chini kufanya kazi ya kutoa ushauri wa kisheria kwa sababu mwisho wa siku huko ndiko watakakoenda kukusanya taarifa za namna gani ambavyo haki za binadamu zinazingatiwa kwa mujibu wa Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri asiponijibu vizuri kuhusiana na suala la ndoa za utotoni, nitashika shilingi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani katika kipindi chake cha uongozi kumekuwa na mafanikio makubwa katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri Mheshimiwa Jumanne Sagini, bila kuwasahau viongozi wa Mahakama ya Tanzania na Viongozi Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na pia watendaji wote na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria tumefanya ziara mbalimbali za kukagua miradi na tumeweza kuona mafanikio na changamoto mbalimbali za taasisi zilizo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria; katika vipaumbele walivyokuwa wamepanga kuvitekeleza kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mojawapo ilikuwa ni kuimarisha huduma za kisheria kwa umma (Kipengele Na. 6) ambapo katika huduma za kisheria kwa wateja wameanzisha Kituo cha

Huduma kwa Wateja ambapo mwananchi anaweza kupiga simu na kueleza malalamiko ya masuala ya rushwa na ukiukwaji wa haki. Ni hatua kubwa sana imeleta wepesi wa huduma hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sasa ofisi hii imeendelea na mchakato wa kuanzisha Kituo cha Usuluhishi Tanzania. Katika changamoto mbalimbali ambazo wanakutana nazo ni uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA ikilinganishwa na miundombinu na mifumo iliyopo. Ushauri wangu ni kuwa Serikali iangalie maeneo ya pembezoni ya halmashauri zetu, hivyo Serikali ishirikiane na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ili kwa pamoja waweze kulitatua tatizo hili, pia Serikali iwekeze katika kutoa vitendea kazi kwa mfano vishikwambi na kompyuta ikiwa ni sambamba na upatikanaji wa mtandao wa uhakika ili kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Fungu Na. 16; ofisi hii majukumu na vipaumbele vyake wamevitekeleza ila bado pia wana changamoto ya uwepo wa miundombinu duni ya TEHAMA ambayo inapelekea ugumu wa upatikanaji wa taarifa mbalimbali za kiutendaji wa ofisi hiyo na hivyo wananchi kukosa haki ya kufahamu masuala yanayoendelea katika sekta ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na tatizo la kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara ya watumishi wa ofisi hii kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria, pia wana changamoto ya kukosekana kwa ofisi katika mikoa mbalimbali hivyo kupelekea kutokusogeza huduma hizo karibu na wananchi, hivyo naishauri Serikali kuhakikisha fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge za ofisi hii hususani za fungu la maendeleo zipelekwe kwa wakati ili kupunguza changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichangie kuhusu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka - Fungu Na. 35; ofisi hii ilianza kufanya kazi mwaka 2018 na mojawapo ya majukumu yake ni kukagua magereza na mahali popote wahalifu na mahabusu wanapohifadhiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wahalifu kwenye baadhi ya magereza wamekuwa wakipata magonjwa mbalimbali na katika kipindi hiki cha ugonjwa wamekuwa wakikosa chakula kinachofaa pamoja na matibabu hususan vipimo na dawa. Ushauri wangu ni kuwa baadhi ya magereza wanalima mbogamboga na matunda, tunashauri wagonjwa hawa japo wapatiwe mbogamboga hizo hasa wanapokuwa wagonjwa, tunashauri pia Serikali iwapatie dawa na vipimo bila kulipa gharama maana wengi wanakuwa hawana kipato wawapo magerezani au mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitembelea baadhi ya magereza haya na ukawatembelea wagonjwa hawa unaweza kutokwa na machozi, jambo hili liangaliwe kwa umakini mkubwa. Tunawapongeza kwa kwenda kukagua, tunawaomba wanapoondoka kwenye ukaguzi waweke mifumo mingine ya ufuatiliaji wa haki za wahalifu hawa, hata wakiwa hawapo eneo la tukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuiwezesha Ofisi hii ya Taifa ya Mashtaka kuendelea kujenga ofisi zao katika mikoa 10 ya Tanzania ambapo miradi hii ya ujenzi ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iiwezeshe ofisi hii katika suala la usalama wa watumishi, iwapatie vibali vya ajira kwa ajili ya kupunguza uchache wa watumishi na kuwaongezea vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia kuhusu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali - Fungu Na. 19; ofisi hii tumeona kupitia utendaji kazi uliotukuka na wa kizalendo wa watumishi mahiri wa ofisi hii nyeti kupitia kusimamia uendeshaji wa mashauri mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, pia kupitia usuluhishi wa mashauri, madai mahakamani na usuluhishi nje ya mahakama. Ofisi hii imeweza kukomboa kiasi cha shilingi trilioni 3.48 za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la usuluhishi wa kitaifa na kimataifa, ofisi hii imekomboa kiasi cha shilingi bilioni 223.69, kwa kazi

hii iliyotukuka kwa ofisi hii, lakini bado ina changamoto mbalimbali kama vile jengo la Makao Makuu ya ofisi yao Jijini Dodoma limefikia 47% ya utekelezaji ambayo ni nyuma ya muda. Kwa sababu hiyo, tunaiomba Serikali kwa kazi iliyotukuka iliyofanywa na watumishi wa ofisi hii, tunaomba fedha za ujenzi wa ofisi hii zikamilishwe kulipwa chini ya mkandarasi SUMA JKT. Aidha, tunashauri kwa jicho la tofauti watumishi wa ofisi hii wapewe vitendea kazi hususani magari. Pia nashauri watumishi wa ofisi hii wapelekwe kusomea zaidi kwenye ubobezi katika maeneo ya gesi, mafuta, uwekezaji, anga, madini, uchumi wa bluu na TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwatia moyo watumishi wa ofisi hii, tunaomba pia maombi haya ambayo wameomba kwa muda mrefu na ni ya msingi, Serikali iwatekelezee kwa jicho la udharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** *Sasa tunaanza na Mheshimiwa Nape na ajiandae* Mheshimiwa *AG*.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Mwanzo kabisa kabla sijasahau niseme naunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania kwa kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Miungano mingi imekufa, wamejaribu wenzetu katika Bara la Afrika, katika Mabara mengine, kuna watu wameungana miaka miwili, mitatu, miaka 10, miaka mitano imeshindikana. Sisi miaka 60 imewezekana, hongereni sana Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niwapongeze waasisi wetu Mwalimu Nyerere na Karume kwa kuasisi jambo ambalo kwa kweli limedumu kwa miaka hii 60. Niwapongeze Marais wote kuanzia

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa Awamu ya Pili, ya Tatu, ya Nne, ya Tano na sasa tupo na Mama Samia, Awamu ya Sita tunasonga naye mbele na amesema kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona vinaelea vimeundwa. Tumefikishwa hapa na misingi ambayo ndiyo imelifanya Taifa letu leo tunajivunia. Misingi hii mojawapo ni Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Toka imeasisiwa yamefanyika marekebisho kadhaa, lakini kubwa kuliko yote utamaduni tulioujenga wa kuiheshimu Katiba yetu. Hii Katiba imetuunganisha Watanzania bila kujali makabila yetu, bila kujali dini zetu, bila kujali tunapotoka na imetupa amani na utulivu tunaheshimiana, tunaenda salama kwa sababu hii Katiba imetufikisha hapo. Ukajengwa utamaduni wa kuiheshimu, kuifuata na ndiyo maana tukiapa tunashika Katiba na tumeapa kuilinda na kuitetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Watanzania 70% mpaka 80 tumezaliwa baada ya Muungano. Kwa hiyo hatujui kule nyuma, sisi tunajua Muungano wetu na ndiyo maana ni muhimu sana Watanzania tukahamasishana kuulinda na kuutetea kwa wivu na nguvu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya kumeanza kutokea wanasiasa wenzetu na nadhani kwa kufilisika kisiasa wameanza kutomasatomasa utamaduni wa kuheshimu Katiba yetu, utamaduni wa kuheshimu Muungano wetu na wanatumia maneno ya hovyo kidogo ambayo tukinyamaza na tukayavumilia kidogo kidogo huu utamaduni utaporomoka na hivyo tutaliangamiza Taifa letu, ni muhimu tuwakemee. Hapa nataka nitoe mfano, yuko mjomba wangu mmoja anaitwa Tundu Antipas Lissu, juzi akiwa Babati, Mkoani Manyara amesimama mchana kweupe akaanza kukosoa baadhi ya mambo yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosoa siyo tatizo, lakini alikuwa anakosoa akisema kwamba haya mambo yamefanywa kwa sababu Rais aliyepo ni Mzanzibari. Hili tukilinyamazia litaota mizizi na litabomoa

Taifa letu. Hatuwezi kukubali mtu mmoja amelewa na ameleweshwa na utu, ubinadamu, uzalendo na uungwana wa huyu anayemwita Mzanzibari. Lissu alikuwa amekimbia nchi yetu amerudishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, akalipwa fedha zake, akaruhusiwa kupanua mdomo hadharani kweupe na mikutano ya hadhara, lakini leo kakereka. Kukereka ni jambo la kawaida kwa sababu hatuwazi sawasawa wote. Leo tukiruhusu maamuzi ya Serikali zetu, maamuzi ya viongozi wetu yakakosolewa kwa namna ya anakotokea, kwa jinsia yake, kwa dini yake, kwa kabila lake au ukanda anakotoka, tutakuwa hatuitendei haki nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kuwaomba Watanzania. Hili jambo limesemwa siku mbili, tatu zilizopita. Nilitegemea chama chake na viongozi wake watamkemea. Kwa kuwa wameshindwa kumkemea nataka tutumie Bunge hili tuwaambie Watanzania wakikemee chama hiki na viongozi wao, na tukitenge, kwa sababu sisi tunaujua Utanzania wetu na makabila yetu yote. Mimi ni Mmakonde, mke wangu ni Mkurya na watoto wangu hata ukiwauliza hawajui ni kabila gani. Leo kila jambo wanasema huyu amefanya kwa sababu ni Mzanzibari angekuwa Mtanganyika asingefanya haya. Halafu bila aibu anakwenda kuwaomba Wazanzibari kura na kuwataka waunge mkono chama chake. Hili jambo lazima tulikatae, kama Watanzania tutumie nguvu zetu zote kulaani na kukemea upuuzi huu ambao unataka kuligawa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu amekuwa muungwana sana, ametumia Katiba hii ambayo, sawa, kama yapo mapungufu ya Katiba, hata ilipotungwa mwaka 1977 siyo hii tuliyonayo, tumekuwa tukirekebisha hapa na pale kulingana na mahitaji na mazingira, hakuna shida, lakini Watanzania tuna utamaduni wa kuheshimiana, hata tukikosoana basi tuheshimiane. Leo anatokea mwanasiasa kwa kutaka tu madaraka yuko tayari kuligawa Taifa letu na anasema kwa kusisitiza kwamba huyu ni Mzanzibari, huyu ni Mtanganyika. Leo tukiruhusu haya tunataka kuligawa Taifa letu. Nimesimama kusema Watanzania tusikubali upuuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kusema Watanzania tusikubali upuuzi huu. Nitawashangaa Watanzania waliozaliwa wakati wa Muungano na hata wanaokwenda kumsikiliza mpuuzi huyu. Tumkemee, tumtenge na tumlaani ili awe fundisho kwa wenzake na waache kutumia tamaa zao kuligawa Taifa letu, tusikubali, kwa sababu, kama ana hoja *platform* zipo. Ni Rais huyu Mzanzibari anayemsema ndiye aliyesema andamaneni, Polisi kawalindeni. Leo walikuwa wanaandamana hapa wamelindwa na Polisi, wamesindikizwa walipoenda. Wamesababisha foleni hapa Dodoma, magari yamesimamishwa ili wao waandamane kwa uungwana wa huyu Mama wanayemtukana. Wote kwa pamoja tumlaani, tumkemee na kwa sababu chama chake kimenyamaza na chenyewe tukizike, tuachane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vyama na watu ambao hawataki kuheshimu Katiba tuliyojiwekea na Mama anasema Katiba yetu siyo Msahafu, ameruhusu tujadiliane na akasema twendeni kwenye mchakato, akaunda timu na wao walikuwemo wengine wakazira. Sasa kama ameshindwa kutumia *platform* kujenga hoja yake nadhani tusiharibu Taifa letu, tusikubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria, napongeza misingi iliyojengwa ambayo imelifanya Taifa letu lifike hapa, *I am proud of my nation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizitembelea nchi za majirani zetu watu wanaulizana kwa ukabila wao, kwa udini wao, kwa ukanda wao na wanagawana madaraka kwa utaratibu huo. Mwenyezi Mungu amelibariki Taifa letu, makabila zaidi ya 126 hatugawani kwa makabila. Hawa wapuuzi wanaotaka kutugawanya kwa makabila lazima tuwakemee kwa sauti kubwa, lazima tuwalaani kwa sauti kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe, Muungano huu ni wetu siyo wa wanasiasa wachache. Ni kwa ajili yetu, kwa ajili ya watoto na wajukuu wetu na kwa hiyo tuutetee na tuulinde kwa wivu mkubwa. Kama yapo mapungufu ya kikatiba, kisheria na kiutaratibu tukosoane

na turekebishe kwa nidhamu, tukosoe turekebishe kwa kuheshimiana, wawe na adabu kidogo. Hili liwe fundisho kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge walipiga makofi mfululizo)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nape hayo ndiyo maua yako leo. Mheshimiwa *AG*. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukushukuru kwa fursa ambayo umenipatia. Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza nchi hii kwa misingi ya utawala wa sheria na utawala bora na halikadhalika, Mhimili wa Bunge kuendelea kusimamia hayo. Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wetu pamoja na Kamati zetu tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefika hapa kwa mchango mkubwa wa mhimili wa Mahakama, ambao kwa kazi kubwa inayofanywa na Bunge hili pamoja na Serikali, basi utekelezaji mwingine wa sheria zetu kutafsiriwa na migogoro inayotokea hupelekwa Mahakamani na kutolewa maamuzi ya kisheria. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkuu, Majaji wote pamoja na watendaji wanaokwenda Mahakamani wakiwemo *DPP* na mawakili kutoka katika ofisi yake, mawakili wa ofisi yangu, mawakili kutoka Ofisi ya *Solicitor General* na mawakili wote 3,479 waliopo kwenye sekta ya umma ninaowasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Naibu Waziri na niko hivi kwa sababu yao; kwa sababu ni viongozi wangu wanaonilinda, kuniongoza na kuhakikisha natimiza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya Bajeti kwa hotuba zao ambazo

waliziwasilisha asubuhi ya leo. Walitoa ushauri japo upo ushauri uliotolewa kuhusiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ofisi zingine za kioperesheni, hasa kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo Mawakili wetu. Ushauri huu tumeupokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze kwamba, kama Wabunge watakuwa wamepitia kitabu cha mapendekezo ya bajeti cha Mheshimiwa Waziri wataona kwamba kuna kiwango cha kiasi cha fedha bilioni tatu kimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo mawakili wetu kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika kushughulikia mikataba na makubaliano mbalimbali na kazi nyingine za kisheria zinazotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vivyo hivyo kuna fungu la fedha limetengwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa minajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilishauri kwamba uwekwe mfumo wa kutoa motisha kwa mawakili. Jambo hili ni jema na niahidi tu kwamba tutaendelea kulifanya. Yapo mengi yanayofanyika kwa wanaotenda kazi vizuri. Miongo mitatu ambayo nimekuwa kwenye utendaji kazi katika tasnia ya sheria naelewa watu wengi ambao wameajiriwa na Serikali katika tasnia yetu tumejitahidi kuhakikisha hawabaki hapo walipo. Wapo walioajiriwa kwa sasa ni majaji na wakurugenzi. Kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha na kutoa motisha zaidi kwa wote wanaotenda kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingi zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na tunawashukuru sana kwa sababu, yote yaliyowasilishwa yanalenga kutuwezesha kuboresha mifumo na kuhakikisha kwamba nchi yetu inaongozwa kwa utawala wa sheria na misingi ya utawala bora. Mheshimiwa Mashimba Ndaki pamoja na yote aligusia changamoto mbili, moja kwenye eneo la ukazaji wa hukumu *(exclusion)* na lingine ni kuhusiana na nyaraka hasa hati zinazowasilishwa Mahakamani na kusitisha shughuli nyingine za kiuchumi kwa wanaozipeleka Mahakamani kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumtoa hofu Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa sababu maboresho yanayoendelea sasa hivi yataendelea kuhakikisha kwamba hili eneo la ukazaji wa hukumu, kama ambavyo amegusia, ni eneo ambalo linaendelea kufanyiwa kazi. Eneo hili kwa kesi za madai linaangukia kwenye haki madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wote tulivyofuatilia, Mheshimiwa Rais baada ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Jaji Mkuu na hotuba nyingine zilizosomwa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria Duniani yaliyofanyika Februari Mosi aliielekeza Wizara ya Katiba na Sheria na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba baada ya kuwa ameunda tume ya kuangalia namna ya kuboresha mifumo ya utoaji wa haki jinai na ile ya mambo ya kuchunguza namna ya kuboresha huduma za Wizara ya Mambo ya Nje alielekeza sasa eneo hili la haki madai nalo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yapo mambo mengi ambayo najua tayari yanahusisha chunguzi na tafiti kupitia *Law Reform Commission*. Kwa hiyo, naamini kadri tunavyoendelea kufanya kazi kupitia Kamati za Kudumu za Bunge bila shaka tutaendelea kutoa taarifa ya mambo mbalimbali yatakavyokuwa yameendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi kwa sababu kama amefuatilia jedwali la sita bila shaka ataona sheria iliyotajwa pale, ile ya mabadiliko ya sheria mbalimbali kupitia mabadiliko ya sheria za sekta za kisheria. Kuna maeneo mengi ambayo Serikali imekwishaanza kuyafanyia kazi. Kwa mfano, mojawapo kwa sasa kwa mtu anayepeleka shauri kwenye Mahakama ya Rufani hahitaji kuomba kibali *(leave)*. Ilikuwa ni njia mojawapo, ni maeneo ambayo pia tujue kwamba mtu anapopata tuzo, tuzo hiyo ikakatiwa rufani basi hawezi akakaza hukumu mpaka uamuzi wa mwisho wa Mahakama ya Juu unapokuwa umetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hatua pia za kupunguza ile milolongo ya upatikanaji wa nyaraka za kimahakama *(record of appeal),* ni mambo ambayo Mahakama imepiga hatua kuhakikisha

kwamba yanapatikana kwa haraka zaidi. Kuhusiana na zile nyaraka ambazo nafikiri kwa dhana ile, kwamba zinakwama mahakamani kwa sababu tu zinahusiana na kesi na mtu akashindwa kuendelea na mambo yake mengine ya kiuchumi na kijamii, nimtoe tu wasiwasi kwamba sheria zetu, Sheria ya Mwenendo wa Madai, kupitia amri ya 7(14) zinaruhusu anayepeleka nyaraka hizo pamoja na hati yake ya madai baada ya kuwasilisha anaweza akaacha *certified true copies*. Lakini pia, kupitia Sheria yetu ya Ushahidi, Sura ya Sita, Kifungu cha 64 na 65 vinaeleza namna ya kutumia nyaraka mbadala na zile nakala halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Wakili Msomi Edward Olelekaita alipokuwa akichangia alielezea kero ambayo ilikuwa imewapata baadhi ya wapigakura wake ambao walikuwa na kesi ya mifugo yao kuhusishwa kwenye kesi na baadaye kukawa na maamuzi ya kwamba warejeshewe lakini hawajarejeshewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwatendea haki wapigakura wake na kuwasemea wengine wengi ambao wanakutana na kadhia ya namna hiyo. Nipende tu kueleza kwamba baada ya kuwepo kwa malalamiko haya Wizara ya Katiba na Sheria chini ya Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu waliwaketisha Wizara nyingine zinazohusika na jambo hilo ikiwemo Wizara ya Mifugo na wadau wengine kama vile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa sasa kinachoendelea ni kwamba kuna vikao ambavyo vinaendelea, vimefanyika tarehe 23 Aprili, 25 Aprili na kingine kitafanyika tarehe 2 Mei na hiki nafikiri ndicho kitakuwa cha kuhitimisha. Kwa hiyo Mheshimiwa Wakili Msomi endapo jambo hili litaendelea kutopata suluhisho, basi naamini Ofisi ya Waziri mwenye dhamana na Katiba na Sheria na ofisi nyingine tutaendelea kuhakikisha kwamba jambo hili linashughulikiwa na kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ambazo ziliwasilishwa na Mheshimiwa Mbunge Shally Raymond, dada yetu mkubwa. Mojawapo ilihusiana na kesi za mauaji kuchelewa au wanaohusishwa na kesi hizo baada ya kutiwa hatiani, basi hukaa muda mrefu bila

hatima zao kujulikana. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Shally kwamba, baada ya Mheshimiwa Rais kupokea ile Taarifa ya Haki Jinai tarehe 15 Julai, 2023, jambo hili lilikuwa ni moja ambalo lilikuwa likifanyiwa uchunguzi, kuhusiana na hatma ya watu wenye vifungo vya maisha pamoja na hatma ya watu ambao wanahukumu za kunyongwa (hukumu za kifo) na hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walifuatilia bila shaka taarifa ile ilikuwa na mapendekezo ambayo sasa yanafanyiwa kazi; kuangalia namna ya kubadilisha Kanuni ya Adhabu. Kwa upande wa adhabu ya maisha basi kuwe na vigezo vingine, isiwe kwamba maisha maana yake ni Maisha, lakini kwa maana ya adhabu ya kifo vilevile kuna mapendekezo ambayo yalitolewa, kwamba Mahakama isifungwe mkono, Jaji anayesikiliza au Mahakama inayosikiliza iweze kutoa adhabu nyingine kutegemeana na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na sababu kwamba taarifa ile na mapendekezo yake Mheshimiwa Rais aliyatolea maelekezo kwamba yafanyiwe kazi na Kamati ambayo inatengeneza mkakati wa utekelezaji wake. Kwa hiyo jambo hili litaendelea, yale mabadiliko ya sheria lazima yatakuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhia nyingine za kuhusiana na hayo nipende tu kueleza mimi kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ofisi nyingine na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka tunayo dhamana ya kushughulikia lalamiko moja moja ambalo linakuwa na mazingira ya kipekee. Kinachohitajika ni kupewa lalamiko ambalo inakuwa ni rahisi kulifuatilia. Tumekuwa tukifanya hivyo mara nyingi pamoja na kufanya kaguzi Magerezani na kufanya vikao na vyombo chunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joseph Kakunda, kaka yangu, nafikiri pamoja na mengine aliongelea ile Taarifa ya Tume ya Haki Jinai, kwamba ilipowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais ilikuwa na mapendekezo mengi na kwamba hakuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilipokuwa naangalia, nimejiridhisha kwamba Mheshimiwa Waziri amelitaja jambo hili kwenye *paragraph* ya 39 ambapo ameeleza baada ya kupokea taarifa ile Wizara iliketi na kuweka mpango wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa mpango wa utekelezaji huu tayari Wizara na kama zilivyo Wizara zingine zilizoguswa kwa sasa zimekwishakwenda mbele ya ile Kamati inayotengeneza mikakati. Kwa hiyo, mikakati ile maana yake itakuja kuzaa Sheria, itakuja kuzaa miongozo na Sera mbalimbali. Ukiangalia kwenye hiyo *paragraph* ya 39 kwa sasa Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji kadri unavyofanyika na ile Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nafikiri inatosha kukushawishi kwamba kilicho kwenye Taarifa hii ni sahihi na nisingetegemea Mheshimiwa Waziri atoe zaidi ya alichokitoa kwa sababu yeye amekwishapakua na kupeleka kwenye chombo kingine ambacho kimekwishapewa mamlaka ya kufanya hivyo na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile lilijitokeza suala la mabaraza nafikiri huyu alikuwa ni, lilijitokeza suala la kule ngazi ya kata, kwamba taarifa ile imeongelea maeneo ya kuboreshwa kwenye maeneo mbalimbali lakini haikueleza nini kifanyike katika ngazi ya kata. Sasa kwa taarifa hiyo hiyo pendekezo moja kubwa ni kuundwa kwa chombo kimoja chenye dhamana ya kufanya upelelezi ambacho kitakuwa na hadhi ya Taifa na ule mkakati sasa upo kwenye hatua ya kuandaliwa maana yake utakwenda mpaka ngazi ya kijiji yaani kule walipo wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unafuatilia nini kinafanyika na kinafanywa na polisi kwa sasa huwa wamekwishapeleka hao mapolisi kata. Kwa hiyo nafikiri ule mpango utakapokuwa umekamilika kwa sababu utazihusisha taasisi zote zinazofanya uchunguzi wa jinai wa kisheria, naamini hapatakuwa na ombwe lingine ambalo litajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Stephen Chaya aliongelea kuhusu Sheria ya TAKUKURU kufanyiwa marekebisho, ni

kweli hii Sheria ni zao la Mkataba wa Kimataifa *(United Nations Convention Against Corruption)* na baada ya Serikali yetu kuwa sehemu ya mkataba ule ndiyo tulitunga Ile Sheria ya Rushwa, Na. 11 ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama iliyo kawaida, sheria yoyote inayohusu maisha ya mtu, maisha ya nchi, shughuli za kijamii, shughuli za kiuchumi, mara kipindi kinavyoenda lazima ifanyiwe marejeo. Kwa hiyo, naelewa TAKUKURU wenyewe, lakini hata kwenye ile Tume ya Haki Jinai walielekeza kwamba hizi sheria zote pamoja na ile Sheria ya Uhujumu Uchumi zifanyiwe mapitio ili tuwe na vifungu vinavyoakisi uhalisia wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kwamba kama tumeendelea kuangalia lile jedwali la sita, tutaona jinsi ambavyo Serikali kwa kile inachokikamilisha kinaletwa hapa Bungeni na kitu kikubwa kabisa ambacho naipongeza Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ni jinsi ambavyo imekuwa ikifanya kazi kuhakikisha kwamba Miswada ya Sheria inayopelekwa kule basi haigandi, inawasilishwa kwenye Bunge hili. Ni faraja yangu kwa kipindi ambacho nimekuwemo humu, tayari kuna sheria nyingi na mfumo huo huo zimefanyiwa marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirudie kukushukuru wewe, lakini na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo wameitoa na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia fursa hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutualia afya iliyotuwezesha kusimama hapa tukiwa salama ili kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kwa mara nyingine na kunipangia majukumu mengine toka Wizara ya Mambo ya Ndani na sasa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria kumsaidia dada yangu Mheshimiwa Balozi Pindi Hazara Chana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru pia Viongozi Wakuu wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Wakuu wangu wote kwa miongozo na ushauri unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufasaha, lakini bila kumsahau kaka yangu Mheshimiwa *Engineer* Masauni aliyenilea miaka miwili na ushee nilivyokuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana Balozi kwa ushirikiano na mwongozo anaonipa katika kutimiza majukumu yetu ya Wizara. Niwashukuru pia watendaji wa Wizara wakiongozwa na Bi Marry Gasper Makondo, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hatibu Malimi Kazungu, Wakuu wote wa Taasisi za Wizara na Watendaji wote katika Wizara na Taasisi za Wizara hii kwa ushirikiano wao mkubwa katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, wote kabisa kwa ushirikiano, urafiki na udugu ambao tumekuwa nao wakati wote na wanaendelea kunipa moyo, tutashirikiana vizuri katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii. Shukrani zingine kwa umuhimu wa pekee kwa familia yangu kwa kuniruhusu na kunikosa mara nyingi ninapofanya kazi za Serikali na kazi zingine za Ubunge bila kuwasahau wananchi wa Butiama ambao wameridhia na kunivumilia ninapokuwa natekeleza majukumu mengi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda sitaweza kuzungumza hoja nyingi, nitamwachia nafasi Mheshimiwa Waziri wangu ili aweze kuzi-*cover*. Naomba uniruhusu nizungumzie chache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Kizito Mhagama kuhusu Mahakama iwe na mpango wa kuongeza matumizi ya mfumo wa tafsiri na unukuzi *TTS* katika Mahakama zote nchini. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepokelewa na Mahakama ina malengo ya kuweka mfumo huu katika Mahakama zote kwa awamu kwa kuzingatia uwepo wa fedha na miundombinu rafiki ikiwemo upatikanaji wa mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Edward Olelekaita amezungumzia juu ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kiteto na Mahakama nyingine za mwanzo zimetajwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kuhusu hili la Mheshimiwa Olelekaita nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kulingana na Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama, Mahakama ya Wilaya ya Kiteto itajengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwanza alipongeza uwepo wa *IJC* kwa maana ya *Integrated Justice Centre* na akashauri ziendelee kujengwa katika maeneo mengine. Tunamshukuru kwanza kwa pongezi, lakini tunapokea ushauri wake wa kuendelea kujenga vituo hivi kwani katika bajeti ijayo, vituo hivi vitajengwa katika mikoa tisa kwa maana ya vituo jumuishi katika Mikoa tisa ifuatayo: Geita, Katavi, Lindi, Njombe, Ruvuma, Simiyu, Singida, Songwe na Pemba. Kwa hiyo, ni dhamira ya Serikali kuona kwamba vituo hivi vinapekekwa katika maeneo mbalimbali ili Watanzania waweze kunufaika kama ilivyoelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lilizungumzwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei kuhusu uchakavu wa Mahakama za Mwanzo katika Jimbo la Vunjo, Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, Marangu, Kilema na kadhalika. Mapendekezo ya Mheshimiwa

Mbunge yamepokelewa na yatazingatiwa katika Mpango wa Ujenzi wa Mahakama kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ninayoomba kuichangia iliibuliwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye alizungumzia Serikali kuwa na kipaumbele katika kujenga Mahakama za Mwanzo na akasema Sikonge kuna Mahakama moja tu, zinahitajika nyingine katika kata saba zilizo mbali. Mahakama inayo mpango wa kujenga Mahakama za Mwanzo kwa kila Tarafa nchini kwa sasa. Kwa Mwaka 2024/2025, zitajengwa Mahakama za Mwanzo 72 katika wilaya mbalimbali nchini na Mahakama mojawapo itajengwa katika Kata ya Kipili, Wilayani Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia kwenye eneo la Mheshimiwa Joseph Kakunda kwa nini haijatajwa namba ya kupokea maoni ya malalamiko ya Mahakama? Naomba nimtajie namba hii na kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote, Mahakama ina kituo cha huduma kwa wateja, *call centre* kwa ajili ya kupokea na kushughulikia maoni, mapendekezo, malalamiko, pongezi na maulizo. Wananchi wanaweza kupiga simu hiyo bure kupitia namba 255800247 na namba nyingine ni 0752500400, pia kuna namba ya kutuma ujumbe mfupi ambao ni 0739502401.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu kwa mara nyingine. Nichukue nafasi hii kuendelea kukushukuru wewe binafsi, lakini pia nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Jumanne Sagini kwa kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu na nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia niwashukuru sana kwa ufafanuzi mzuri ambao wametoa mbele ya Bunge letu Tukufu. Napenda kuendelea kuishukuru sana Kamati yetu ya Katiba na Sheria, Kamati ambayo imetoa maoni muhimu, ushauri na mapendekezo na Waheshimiwa Wabunge wote tumepata wachangiaji takribani 13 michango yao ni muhimu na ni mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli nimepokea changamoto nyingi, *critics*, hali inayoonyeha dalili za dhati kabisa za mwamko mkubwa katika suala zima la masuala ya Katiba na Sheria na haki kwa ujumla. Aidha, katika michango hiyo imedhihirika wazi umuhimu wa kuimarisha Wizara kupitia Sera, Sheria, Kanuni, taratibu na Miongozo mbalimbali ambayo kimsingi inaongoza Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni dhahiri kuwa masuala ya huduma za msaada wa kisheria, masuala ya Mahakama, ujenzi na miundombinu ya Mahakama, ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara yetu na maeneo mengi sana yamechangiwa katika maeneo hayo. Hivyo kwa ruhusa yako naomba nianze kufafanua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala hapa tumeambiwa umuhimu wa makusanyo ya maduhuli kimsingi yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato. Sisi tunaungana kabisa na maoni haya muhimu kwamba maduhuli lazima yaakisi uwezo wa ukusanyaji lakini ukweli ni kwamba katika Mhimili wa Mahakama na Mhimili wa Katiba na Sheria, Wizara yetu na Mhimili wa Mahakama vyanzo vingi vinategemeana na zile sheria ambazo tumezitunga hapa sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatunga sheria tunasema atakayefanya makosa katika sheria hii atahukumiwa labda kifungo cha miezi sita ama faini. Tunaposema zile faini ndiyo maduhuli ya eneo letu sisi la Katiba na Sheria kwa sababu Wizara ya Katiba na Sheria jukumu lake hasa ni kutoa huduma, ukichukua upande wa *Law*

*Reform Commission* ni kutoa huduma siyo chanzo cha mapato, ukichukua Tume ya Utumishi wa Mahakama jukumu lake ni kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapokuwa tumeweka maduhuli ni kweli tunakuwa tumeweka, lakini kuna wakati tunafikia viwango na kuna wakati hatufikii kwa sababu tunakuwa labda kwa namna moja au nyingine hatujatoza zile faini kwa sababu watu wanatii sheria pasipo shuruti. Wanapotii Sheria pasipo shuruti maana yake ndiyo utawala bora wenyewe, maana yake nchi ina amani na utulivu, mambo yanaenda vizuri, lakini kwa wale wanaokosea ndipo tunaposema kuna faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwingine siyo rahisi sana kukidhi na kufikia maduhuli tuliyojiwekea, inategemeana kama sheria zimekiukwa ama hazijakiukwa, lakini hoja bado ni ya msingi kwamba tuone namna gani tunaweza tukafikia suala zima la maduhuli ambayo kimsingi tunakuwa tumejiwekea. Kuna suala zima la *Mama Samia Legal Aid,* hili ni jambo la msingi, tunamshukuru sana sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa kutupa maelekezo thabiti kabisa kwamba mwende kwa Watanzania muwasikilize kero zao, hoja zao na muone namna gani ya kuendelea kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane kabisa na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao kwanza na Kamati imesema, tufike katika mikoa ambayo bado. Kimsingi tunachokifanya sasa hivi tunapoenda katika mikoa tunazindua suala zima la *Mama Samia Legal Aid* na baada ya uzinduzi kunakuwa na mashirika ambayo yamesajiliwa kutoa huduma za msaada wa kisheria yakiwa katika mkoa husika au katika wilaya husika. Yale mashirika tunashirikiana nayo, lakini siyo tu mashirika pia kuna wasaidizi wa Sheria na hadi hivi sasa tuna wasaidizi wa sheria takribani 1,888 wamesajiliwa kutoa huduma za msaada wa kisheria na wanapopata taarifa wanawasaidia wananchi katika ngazi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mashirika tunayo mashirika tuliyosajili takribani 270 na nimeshaelekeza, lazima tuwe na *directory,*

unapoenda Kigoma mtu ana shida, ukatili umefanyika au jambo lolote mirathi au ardhi, anapohitaji huduma za kisheria ni wapi anaweza akapata na kuna wale ambao wanatoa huduma bure. Nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuzishukuru taasisi zote zinazotoa huduma za kisheria bure, miongoni mwao kuna Chama cha Wanasheria Wanawake wanatoa huduma bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanganyika Women Lawyers, Tanganyika Law Society,* Vyuo Vikuu, Kitivo cha Sheria ikiwemo Chuo Kikuu ch Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, *Law School of Tanzania* na maeneo mengine mengi wanatoa huduma *pro bono,* bila malipo yoyote, tunawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kuwasaidia Watanzania. Watanzania wana changamoto nyingi na ukitembelea huku nimeshuhudia baadhi ya watu wanapata changamoto kwa kuwa alikosa ushauri au kwa kuwa hakujua nini cha kufanya wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kushuhudia katika magereza unakutana na mama anakwambia, nimeingia kwa ajili ya *murder, murder* kutokana na nini anasema mume wangu hakuleta matumizi nyumbani na nilikuwa na Watoto, nikakaa nikaona bora niondoke, nikakoroga sumu kumbe ungempa huduma ya kisheria kwamba kuna ustawi unaweza kwenda kudai haki za kulea Watoto, ingeweza kuponya watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *Mama Samia Legal Aid* niwaambie Watanzania wote ni huduma ambazo ni haki za Watanzania. Katika mikoa yetu, katika wilaya zetu, vijiji, mitaa unapokuwa na changamoto za kisheria hapana kubaki nyumbani na manung'uniko na masikitiko, tutoke tuulizane, tutoke katika taasisi zetu, katika ofisi zetu za Serikali, tuombe msaada wa kisheria, tunazo ofisi zetu hata Ofisi za ma-*DC* wanasikiliza, Ofisi za Serikali za Mitaa, lakini Wanasheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunao kila halmashauri na taasisi zinazotoa huduma ambazo zimesajiliwa mashirika 270 wasaidizi wapo. Kwa hiyo tutatoa hiyo *directory* na tutazindua rasmi na tutaitangaza

na ku-*share* vizuri kabisa na mikoa yote na wilaya. Mtu anapokuwa na changamoto ni muhimu kujua aende wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, tumeona pia tutenge fedha, kwa hiyo tunachofanya ni kuzindua, baada ya kuzindua huduma ile tuhakikishe kila siku lazima inaendelea, siyo kwamba baada ya kuzindua tunaahirisha. Wito umetolewa hapa na Mheshimiwa Makamba kwamba, tuone namna gani ya kuwashirikisha wanasheria na mashirika mbalimbali, jambo hili tumelichukua alisema tutashirikiana vizuri kabisa na hivi karibuni kuna mkoa ambao tumepanga kwenda kuzindua. Basi wale ambao wako tayari ku-*volunteer*, iwe ni Wabunge au sio Wabunge, tutahakikisha tunashirikiana nao kwa ajili ya kutoa huduma, kupata uzoefu na kadhalika. Kwa hiyo, huduma hii ya *Mama Samia Legal Aid* imeendelea kusaidia sana. Wengine wamechukua mkopo, baba amechukua bila kumshirikisha mama, yamkini baba ametangulia mbele ya haki, mama anaambiwa nyumba inanadiwa. Ilikuwaje, anasema baba alikwenda kuweka nyumba dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiokoa hati za watu, tunalipia. Hivi karibuni tulipata kisa mkasa, mama mmoja alikwenda mpaka Ikulu, nyumba yangu inataka kuuzwa na benki, akaambiwa iliwekwa dhamana, mama akasema sikuwa na habari, naenda wapi na watoto? Kupitia Ofisi ya Rais mwenyewe ametoa maelekezo kwamba, wasikilizeni Watanzania muwasaidie. Kwa hiyo, *Mama Samia Legal Aid* imekuwa ni mkombozi sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisubiri viongozi wakubwa waje ndio tupange foleni kwenda kusema changamoto tulizonazo, tuzitatue kabla. Wapo viongozi wetu, ofisi zetu zipo na sisi Wanasheria tupo katika Mikoa na katika Wilaya, kwa hiyo, natoa wito kwa Watanzania wenye changamoto, karibuni tuzungumze tuyajenge tupate utatuzi na ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kama nilivyosema awali, pia Wizara imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Mteja *(Contact Centre)* ambacho namba ya Mahakama ipo, lakini pia *Mama Samia*

*Legal Aid* kwa kushirikiana na Wizara yetu kitengo cha TEHAMA tumeweka namba maalum ambayo niliitaja wakati nawasilisha taarifa yangu asubuhi, naomba nirudie kuitaja tena namba hiyo, ambayo ni 0262160360. Hii namba tutahakikisha Watanzania wanaijua ili wanapokuwa na changamoto waweze kupiga simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka ifanyike kama *Voda*, *Voda* wanakwambia ukituma hela kwenda mtandao tofauti, *tiGO/Airtel*, kuna namba unapiga unapokelewa na unaelekezwa ni namna gani ya kuweza kurekebisha changamoto yako. Kwa hiyo, hata huduma hizi tunataka zijulikane kwa Watanzania ili waweze kuzitumia kuuliza mambo yao, kuuliza mambo ya jirani yako, ya ndugu yako, ya jamaa yako, ya rafiki yako, kwamba, jambo hili tunaweza tukalitatuaje kwa pamoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasheria Mkuu na Naibu Waziri wamefafanua maeneo mengi, nawashukuru sana kwa ufafanuzi huo mkubwa, lakini kama nilivyosema awali yako mambo mengine tutaleta kwa maandishi. Tunachukua hoja zote ambazo zimetolewa na maoni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Serikali kwamba, iendelee kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wakati kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tu kwamba, suala la utoaji haki kwa wote na kwa wakati ni miongoni mwa vipaumbele vyetu. Ndio maana Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Haki Jinai ili ije na maoni ni namna gani haki inaweza kupatikana kwa watu wote na kwa wakati. Kwa hiyo, hii ni miongoni mwa vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais ameteua majaji wasiopungua takribani 21. Jana tu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesaidia kutupatia watendaji mahiri kabisa, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwenyekiti wa *Law Reform Commission,* Jaji Korosso, wameapishwa jana. Hii yote ni kuhakikisha kwamba, tunapewa nguvu kazi ya kutosha

tukachape kazi, tukawafanyie kazi Watanzania ambao wako takriban milioni 61. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *spirit* hiyo hiyo ya utoaji haki, ili haki ipatikane kwa watu wote na kwa wakati, Mhimili wa Mahakama umeendelea kupunguza mlundikano wa kesi. Hivi sasa mlundikano unaendelea kupungua, tunayo takribani asilimia tatu tu ya kesi zilizopo ambazo zinaendelea kutatuliwa. Kwa hiyo, naupongeza sana Mhimili wa Mahakama, chini ya Jaji Mkuu Profesa Juma na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, ambao wanafanya kazi vizuri sana na wameleta maboresho ya hali ya juu, ikiwa ni pamoja na miundombinu, Mahakama za Mwanzo na za Wilaya zinajengwa katika maeneo mbalimbali. Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wameuliza hili swali na Naibu Waziri amefafanua vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mkakati kabambe kabisa wa kuhakikisha miundombinu hii ya Mahakama inakuwepo katika maeneo yetu kwa sababu, ni chombo muhimu sana cha kutoa haki kwa wananchi. Kadri tunavyozidi kwenda imani kwa Mhimili wa Mahakama inaendelea kuongezeka. Hivi sasa watu wanajua kabisa kwamba, jambo lako linapokuwa halijakaa sawa unapoenda Mahakamani kwa kweli, unapata haki yako. Kwa hiyo, kupitia utafiti wa *REPOA* unaonesha imani kwa Mhimili wa Mahakama kila siku inazidi kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Tume ya Haki Jinai ambayo imekuja na maelekezo na maboresho. Sisi kama Wizara, tumeshawasilisha mpango wa utekelezaji na maboresho ya sheria mbalimbali. Kwa hiyo, sheria nyingi tunakwenda kuzirekebisha na nyingine hata sasa tumeshaanza kuzirekebisha. Kwenye kitabu, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, kwenye kiambatanisho namba tano na kiambatanisho namba sita tunaonesha ni miswada mingapi imekuja, sheria ndogo ngapi zimerekebishwa ambapo nyingi ni mapendekezo na maelekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea tu kusema kwamba, pia tumeshauriwa kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi.

Tulipokuwa katika Mkutano wa Mawaziri wa Katiba na Sheria wanaotoka Jumuiya ya Madola pale Zanzibar *(Commonwealth Ministers of Justice)* tumekubaliana kwamba, tunapoweza kutatua migogoro kwa njia mbadala, basi tutumie njia hiyo. Kuna wakati tunakwenda Mahakamani, ni sawa, lakini kama kuna njia mbadala, tunaita *alternative dispute resolution,* basi njia hiyo ni sahihi, inapunguza muda, inapunguza gharama na pia haki inapatikana. Kwa hiyo, miongoni mwa mikakati iliyopo hivi sasa ni pamoja na kuhakikisha kwamba, tunaanzisha Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi ambacho kinatarajiwa kushughulikia masuala mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hiki kitakuwa na wataalamu wenye ujuzi na ubobezi katika tasnia ya utatuzi wa migogoro. Hivi sasa nchi yetu ina wawekezaji wengi katika sekta mbalimbali, viwanda, maliasili, madini na kadhalika na hawa wote wakati mwingine kunakuwa na migogoro ya aina moja au nyingine. Hivyo, kama kuna mgogoro basi ni wakati sahihi kutumia njia mbadala ya usuluhishi na wakati mwingine inaandikwa kabisa kwenye mkataba kwamba, inapotokea sintofahamu au aina fulani ya mgogoro basi pia, iruhusiwe kutumia *alternative dispute resolution.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mahakama wao katika kesi za madai wana utaratibu wa kuanza na *mediation* kabla ya kwenda kwenye masuala ya *litigation*. Hivi sasa kupitia *Law School* wanatoa mafunzo kuhusiana na namna ya kutatua matatizo na migogoro kwa njia ya usuluhishi, lakini pia, tunazo taasisi mbalimbali nchini ambazo kimsingi zinafanya kazi hii ya kutatua changamoto kwa njia ya *alternative dispute resolution*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalihakikishia Bunge lako kwamba, tuko imara kuhakikisha, kama ushauri wa Kamati ulivyosema, Serikali iimarishe mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ikiwa ni pamoja na kuandaa wataalam wenye ujuzi wa sifa zinazotakiwa kimataifa katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano. Katika taarifa yetu tumesema baadhi ya kesi tulizoshinda kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni zile ambazo tumetumia njia mbadala ya

usuluhishi ambako na kwenyewe tumeokoa pesa nyingi sana katika kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kwamba, napenda kuzungumzia suala zima la sera. Hivi sasa Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Haki Jinai. Sera hiyo itajumuisha masuala mbalimbali katika mnyororo wa haki jinai ikiwemo utolewaji wa taarifa za matukio ya uhalifu, masuala ya ushahidi, uchunguzi, uhalifu, ufunguaji wa hati za mashtaka, uendeshaji wa mashtaka pamoja na utoaji hukumu. Tumesema tuwe na sera mahususi ya masuala ya haki jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sera hiyo itaangalia usimamizi wa wafungwa magerezani na urejeshwaji wa wafungwa uraiani baada ya kumaliza kifungo au kupata msamaha wa adhabu ya kifungo. Kwa hiyo, haya pia ni maeneo ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi. Ni lazima tuwe na sera na tujitahidi kuona namna gani wanaporejeshwa uraiani hawa wahalifu wasirudie tena, maana tusipoweka utaratibu unakuta mwingine anafanya kosa anarudi tena, anafanya kosa. Kuna mtuhumiwa mmoja alipoenda magereza wenzake wanamwambia karibu nyumbani, maana yeye kufanya makosa na kurudi magereza ni vitu vya kawaida. Kwa hiyo, lazima tuwe na sera kuona namna gani masuala haya ya haki jinai yanaweza kuratibiwa na kudhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea pia na suala zima la usajili wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kupitia *RITA*. Jambo hili pia, katika Bunge letu kupitia michango tumewekewa msisitizo wa kutosha. Kwa hiyo, naendelea tu kusema kuwa, ushauri umepokelewa na hivi sasa tunaendelea kuimarisha mifumo ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu ikiwemo usajili wa vizazi, hususan usajili wa vizazi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametuelekeza, twende kwa Watanzania tukawasajili watoto walio chini ya umri wa miaka mitano bure, tusiwatoze, hiyo ni gharama ya Serikali, wana haki ya kupata cheti cha kuzaliwa. Anapoenda darasa la kwanza

anaulizwa cheti cha kuzaliwa, anapoenda Chuo Kikuu-*Loans Board* wanahitaji cheti cha kuzaliwa, anapohitaji *passport* cheti cha kuzaliwa. Kwa hiyo, tunao mfumo maalum kabisa wa kuhakikisha kwamba, tunatoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watanzania wote. Natumia nafasi hii kutoa rai kwamba, wazazi wahakikishe watoto wanapozaliwa, iwe ni ndugu au jamaa, wasisahau cheti cha kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyeti hivi vipo vya aina mbili, kuna kile cha *pink* ambacho mara nyingi tunakipata *clinic* au katika hospitali pale mtoto alipozaliwa na kuna kile ambacho huwa tuna-*print certificate* kwenye *printer*. Vyeti hivi vyote vina nguvu sawa, kiwe ni kile cha *pink* au kile kingine kwa hiyo, nawahakikishia Watanzania kwamba, Serikali iko imara kuhakikisha watoto wanapata vyeti. Tunapopata hizi takwimu ndio zinatuwezesha kujenga madarasa kwa sababu, tunajua ufikapo mwaka fulani watoto wenye umri wa miaka sita wa kwenda darasa la kwanza watakuwa ni watoto kadhaa. Tunaweza kuweka mipango yetu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu sasa hivi uandikishaji umetoka 13% na sasa hivi tuko 68% ya Watanzania wana vyeti vya kuzaliwa. Tunataka tufike 100%, kila mtoto anayezaliwa awe ana cheti cha kuzaliwa. Wapo wengine wanasahau kuchukua vyeti au wana haraka, lakini sasa hivi sio wengi wanaojifungulia nyumbani, wengi ni kwenye hospitali au *dispensary,* hivyo niwaombe wachukue vyeti vya watoto. Hiyo, inasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea tu kusema tumepata ushauri kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iendelee kuhakikisha kuwa uendeshaji wa mashtaka na usimamizi wa masuala yote ya kesi unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa lengo la kuhakikisha kuwa, haki inatendeka kwa wakati. Haya yote ni miongoni mwa vipaumbele vyetu na tutahakikisha yanatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ambao tumeupata ni kwamba, tuangalie ni namna gani tunaweza tuka-*prevent* zaidi makosa kuliko ku-*cure*, amesema Mheshimiwa Kakunda. Niseme tu

kwamba, tuko imara katika vyombo vyetu vya ulinzi na ndiyo maana Tume ya Kudhibiti Rushwa *(PCCB)* wao wanajiita *Prevention and Combating of Corruption* kwa hiyo, hiyo ndio *spirit*. Ni kweli tusiangalie tu kukinga, lakini tunapoweza kudhibiti kabla ya tukio la uhalifu kutokea na yenyewe ni miongoni mwa vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kusisitiza ni suala zima la Tume ya Utumishi wa Mahakama. Tunayo Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo inaendelea kuratibu masuala ya nidhamu na maadili kwa Watumishi wa Mahakama, ikiwa ni pamoja na kushughulikia kwa haraka mashauri ya kinidhamu dhidi ya watumishi wa Mahakama. Pale inapotokea watumishi wa Mahakama wanatenda shughuli zao pasipo utaratibu, upo utaratibu wa kupokea malalamiko hayo na katika kila wilaya na mkoa kuna Kamati za Maadili. Kwenye Wilaya Mwenyekiti wake ni *DC* na kwenye Mkoa Mwenyekiti wake ni *RC*. Kwa hiyo, pale ambapo kuna changamoto ya Watendaji wa Mahakama ni ruksa kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imeimarisha utendaji kazi kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya na kuendelea kutoa miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa Kamati hizo. Tumeshatoa mafunzo kwa majukumu ya Kamati hizo za Maadili kwa washiriki takribani 90 na wakati mwingine tunapata maswali hapa Bungeni kwamba, kuna baadhi ya maeneo watumishi wa Mahakama wanafanya ndivyo sivyo. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, nawahakikishia kwamba, tunazo Kamati na vyombo imara kabisa ikiwemo *PCCB* na Tume ya Utumishi wa Mahakama, hivi ni vyombo ambavyo viko imara kuhakikisha kwamba, utendaji kazi unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo pia napenda kulizungumzia ni suala zima la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Maoni yametolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, tunashukuru na tuseme tu kwamba, tutayazingatia. Maoni mengi ni juu ya kwamba ni namna gani tunaendelea kuiwezesha tume hii? Ni namna gani tunaendelea kuipatia rasilimali watu tume hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, hii ni tume muhimu sana na ni Tume ya Kikatiba. Kwa hiyo, ushauri umepokelewa na tutahakikisha kwamba, maoni na ushauri wote ambao viongozi Waheshimiwa wameutoa tunaendelea kuuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume inaendelea kuwasilisha andiko la mradi la kiasi cha shilingi bilioni 15. Andiko hili limepelekwa Tume ya Mipango ili kuweza kupewa fedha za maendeleo ya ndani. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na vyanzo vya ndani na sio vya nje tu. Pia, Tume imepata eneo la ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu, eneo la Chinyoya, Dodoma na kwa sasa inakamilisha hatua za manunuzi kwa ajili ya kuanza ujenzi kama tulivyokubaliana kwamba, Makao Makuu ni Dodoma. Hivyo, Ofisi zote zinapaswa kuwa Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Tume tayari ina kiwanja. Natumia nafasi hii kusema kwamba, mara tutakapopata nafasi ni muhimu Kamati yetu ikapata fursa kwenda kutembelea eneo hili. Pia, Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya watumishi mwaka hadi mwaka. Katika Tume hii na kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilipatiwa watumishi takribani 23 na kwa mwaka huu tunaokwenda 2024/2025, tume imeidhinishiwa kuajiri watumishi takribani 99. Haya yote ni kutokana na michango mizuri ya Wabunge, tunawashukuru sana kwa maoni waliyotoa, kuisemea Tume hii na kwa kweli, Tume ni miongoni mwa vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; kwa mwaka 2020 tulipata shilingi bilioni 6.7; mwaka 2021/2022 Tume ilipata shilingi bilioni 6.7; mwaka 2022/2023, Tume ilipata shilingi bilioni 6.7; lakini mwaka huu kutokana na kazi nzuri ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, Tume imeweza kupata shilingi bilioni 8.1 katika bajeti hii ambayo leo Bunge litakwenda kutuidhinishia, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni eneo la *Law School*. Tulibadilisha sheria tukasema tuwe *na Law School;* hiki ni chombo muhimu sana na *Law School* imekwishafanya mapitio ya mitaala ambayo imejikita katika kutoa

mafunzo kwa vitendo na mtaala huo mpya utaanza kutumika kuanzia Julai, 2024. Niishukuru sana kwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tuone namna ya kuboresha *Law School.* Pia, Tume ya Mwakyembe ilifanya kazi kubwa na nzuri sana. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa maoni mazuri na maboresho yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tu kusema kwamba, kwa mujibu wa Tume iliyofanya tafiti, maoni ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi ni kwamba *Law School of Tanzania* iko kisheria na kwamba mtu yeyote mwenye *LLB* anaweza kujiunga na *Law School*. Pia*, Law School of Tanzania* imekuwa ikiwatumia wataalamu wabobezi katika kutoa mafunzo. Kwa sasa *Law School of Tanzania* ina kanzidata yenye wabobezi zaidi ya 80 kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya kisheria. Baadhi ya wakufunzi ni Majaji ambao wanakwenda kufundisha, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tu kusema kwamba mapendekezo mengi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na Kamati, yanaendelea kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndoa; Sheria hii ni muhimu sana. Hapa Waheshimiwa wamesema tuone namna gani sheria hii inaletwa hapa na kusema kwamba umri wa kuoa au kuolewa uwe miaka 18. Sheria hii ilishawahi kuletwa Bungeni kupitia tangazo namba moja *volume* 102, tarehe 5 Februari, 2021. Sheria hii ilipofika hapa tukaelekezwa twende tukakusanye maoni. Tumekusanya maoni na tunaendelea kukusanya maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna *different schools of thoughts,* wapo wanaoafiki watoto wasiolewe kabla ya miaka 18 (mwiko kuolewa huko chini). Kuna watu wana dini zao, kuna watu wana mila zao, kuna watu wana desturi zao na kuna watu wa haki za binadamu. Wapo wanaosema tuliangalie, baadhi ya mila, desturi, dini kwa kuwa anaweza kwenda shule na sasa hivi tumewarudisha shuleni, hata akiolewa arudi shule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, omba pesa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba, mchakato unaendelea na hivi sasa tuko katika hatua ya kuandaa Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako liridhie taarifa hii na naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*..............................Sh. 9,367,681,804

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuna mshahara wa Waziri na tuna mchangiaji mmoja, Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kusema kweli wakati nachangia niliahidi kwamba nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, kiukweli wakati anatoa maelezo yake nimesikitika sana. Nimesikitika sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri akiwa kama mzazi na akiwa kama mwanamke mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikaa baraza kubwa sana. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri alialika Bunge zima ili twende kwenye kongamano kubwa. Walikuja kila aina ya viongozi waliotakiwa (wa kidini, wa kimila, wasomi kutoka vyuo vikuu) tukazungumzia hili suala na ikaonekana limekwisha na Waziri aliji-*commit* na ilikuwa *live* kwenye *Television* ya Taifa, aliji-*commit* kwamba yuko tayari kuleta sheria hii hapa Bungeni ili tuweze kuirekebisha ili kunusuru watoto wanaopata mimba katika umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishashika shilingi mwaka 2018, nilishika shilingi 2019 na wenzangu wameshika shilingi. Niseme tu leo kwa namna ambavyo nimesikitishwa na majibu ya Waziri kutokuwaonea huruma hawa watoto wa kike, naiachia Serikali suala hili ili waone kama jambo tunalolifanya lina tija kwa mustakabali wa watoto wa kike wa nchi hii au halina shida.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunafanya usanii kwenye maisha ya watoto wetu, tunafanya usanii masilahi ya watoto wetu wa kike*… **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, futa neno lako “usanii.”

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nifute nini?

**MWENYEKITI:** “Usanii.” Serikali haifanyi usanii.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, Serikali haifanyi usanii, futa neno lako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya ndivyo sivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa Mamlaka ya Kiti, tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi/Kicheko)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.......................Sh. 9,367,681,804
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………......Sh. 668,212,095
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…........Sh. 1,329,156,015
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……......................Sh. 450,600,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*...Sh 536,836,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* ….Sh. 371,463,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*………………………..…Sh. 638,727,100
Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*....Sh. 475,733,515
Kifungu 2001 – *Human Rights Division*…...…………Sh. 1,735,780,333
Kifungu 2002 – *Legal Aid Services Unit*……………...Sh. 9,979,279,872
Kifungu 2004 – *Public Legal Services Division*….....Sh. 4,175,083,276
Kifungu 2005 – *Natural Wealth and Resource Observatory Unit*………………………...Sh. 868,854,580
Kifungu 4001 – *Constitutional and Justice Monitoring Division*..........................Sh. 7,790,944,410

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 2,593,739,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…...….......Sh. 324,324,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit* …...........................Sh. 195,594,120
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*…….........................Sh. 562,873,500
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*….…..Sh. 125,827,123
Kifungu 1006 – *Management Information System Unit*……..…………………………Sh. 329,285,574
Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*……..………..………Sh. 281,345,000
Kifungu 2001 – *Complaints and Investigation Division*…………………….…………Sh. 1,161,087,000
Kifungu 2003 – *Public Education, Communication Research and Documentation*…..…Sh. 726,673,000
Kifungu 3001 – *Zanzibar Office* ………………….…….Sh. 605,166,136
Kifungu 3002 – *Mwanza Office*……………………….Sh. 297,763,453
Kifungu 3003 – *Lindi Office*……………………….…Sh. 218,204,151
Kifungu 3004 – *Pemba Branch*…………………..…Sh. 205,448,000
Kifungu 3005 – *Dar es Salaam Office*……………….Sh. 1,058,329,943

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………..Sh. 1,594,267,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…........….......Sh. 416,838,000
Kifungu 1003 – *Planning and Coordination Unit*…...…….Sh. 304,146,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……...........................Sh. 215,987,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.............Sh. 206,341,000
Kifungu 1006 – *Public Legal Awareness Unit*…..............Sh. 733,810,000

Kifungu 1007 – *Law Review Unit*……………………..........…....Sh. 806,011,000
Kifungu 1008 – *Law Research Unit*……………...........………Sh. 774,390,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..............................Sh. 88,949,559,123
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…… …Sh. 562,674,000
Kifungu 1003 – *Planning and Monitoring Division*...Sh. 6,508,234,600
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……….................Sh. 401,048,600
Kifungu 1005 – *Information, Communication and Technology Unit*.............................Sh. 3,005,413,492
Kifungu 1006 –*Information, Education and Communication Unit*........................Sh. 528,500,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*……Sh. 588,615,000
Kifungu 1008 – *Estates Management Unit*…………..Sh. 776,673,700
Kifungu 1009 – *Records Management unit*……..…..Sh. 407,185,000
Kifungu 1010– *Library Services* Unit……………..…....Sh. 353,559,900
Kifungu 1011 – *Legal Services Unit* ………………....Sh. 65,942,400
Kifungu 1012 – *Transport Management Unit*..........Sh. 1,766,018,900
Kifungu 2001 – *High Court Main Registry* ……….....Sh. 1,663,721,300
Kifungu 2002 – *Court of Appeal* ..........................…Sh. 7,002,433,336
Kifungu 2004 – *High Court Divisions*……………….........Sh. 205,000,000
Kifungu 2299 – *Commercial Court*……………………Sh. 1,338,808,000
Kifungu 2300 – *Land Court*………………...........…Sh. 1,294,961,000
Kifungu 2301 – *Labour Court*…………….............Sh. 1,162,318,440
Kifungu 2302 – *Case Management Division*………Sh. 820,331,508
Kifungu 2303 – *Complaints Management and Inspectorate*……………………………Sh. 607,953,900
Kifungu 2310 – *Mediation Centre*……………..….…Sh. 554,563,900
Kifungu 2326 – *Corruption and Economic Crimes Court*....................................Sh. 871,205,200
Kifungu 2327 – *Judiciary Delivery Unit*……….....…Sh. 471,940,000
Kifungu 2347 – *IJC Temeke*......................................Sh. 1,155,170,000

Kifungu 3001 – *Arusha Zone*……………….................…..Sh. 1,566,780,300
Kifungu 3002 – *Coast Zone*………………….....................Sh. 786,355,800
Kifungu 3003 – *Dar es Salaam Zone*………….….......Sh. 4,097,531,103
Kifungu 3004 – *Dodoma Zone*…………………….......Sh. 1,646,074,000
Kifungu 3005 – *Iringa Zone*…………………………......Sh. 946,445,600
Kifungu 3006 – *Simiyu Zone*………………………….....Sh. 678,232,100
Kifungu 3007 – *Kigoma Zone*………………………....Sh. 1,231,660,515
Kifungu 3008– *Moshi Zone*………………......................Sh. 1,273,264,000
Kifungu 3009 – *Lindi Zone*………………………… ...Sh. 591,133,000
Kifungu 3010 – *Mara Zone*……………………………....Sh. 1,377,804,900
Kifungu 3011 – *Mbeya Zone*…………………...…....Sh. 1,421,304,000
Kifungu 3012 – *Morogoro Zone*…………………......Sh. 1,474,101,300
Kifungu 3013 – *Mtwara Zone*……………………….Sh. 1,033,758,800
Kifungu 3014 – *Mwanza Zone*……………………....Sh. 1,973,315,100
Kifungu 3015– *Songea Zone*……………………..…….Sh. 967,475,400
Kifungu 3016 – *Sumbawanga Zone*……………......Sh. 968,466,500
Kifungu 3017 – *Manyara Zone*…………………….......Sh. 1,088,389,900
Kifungu 3018 – *Bukoba Zone*…………………….......Sh. 1,607,369,900
Kifungu 3019 – *Singida Zone*………………………......Sh. 587,377,902
Kifungu 3020 – *Shinyanga Zone*……………..….......Sh. 1,209,437,900
Kifungu 3021– *Tabora Zone*………………….……......Sh. 1,284,817,680
Kifungu 3022 – *Tanga Zone*………………….…..….Sh. 1,487,875,101
Kifungu 3023 – *Songwe Zone*………………………....Sh. 570,559,400
Kifungu 3024– *Katavi Zone*…………………………......Sh. 530,607,300
Kifungu 3025– *Njombe Zone*……………………….....Sh. 568,536,100
Kifungu 3026 – *Geita Zone*……………….……….......Sh. 1,128,548,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………..………..Sh. 32,205,524,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…......Sh. 1,066,827,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…..........................Sh. 810,257,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……......................Sh. 496,437,000

Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*......Sh. 442,475,000
Kifungu 1006 – *ICT and Information Unit* ................Sh. 504,328,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*….Sh. 320,475,000
Kifungu 1008 – *Research and Library Services Unit*……………………………………...Sh. 231,875,000
Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*…………...............Sh. 814,434,000
Kifungu 2002 – *Civilanization and Prosecutions*…....Sh. 3,202,955,000
Kifungu 2004 – *Regional Office Arusha*……………..…Sh 994,000,000
Kifungu 2005 – *Regional Office Dodoma*…………..…Sh. 3,513,105,000
Kifungu 2006 – *Regional Office Dar es Salaam*…......Sh.1,162,000,000
Kifungu 2007 – *Regional Office Iringa*………………..Sh. 706,000,000
Kifungu 2008 – *Regional Office Moshi*……………..Sh. 1,054,000,000
Kifungu 2009 – *Regional Office Kagera*………....Sh. 1,318,000,000
Kifungu 2010 – *Regional Office Mbeya*………..Sh. 1,051,000,000
Kifungu 2011 – *Regional Office Mtwara*……………....Sh. 775,000,000
Kifungu 2012 – *Regional Office Mwanza*…...….....Sh. 1,197,000,000
Kifungu 2013 – *Regional Office Ruvuma*…………..Sh. 695,000,000
Kifungu 2014 – *Regional Office Sumbawanga*…....Sh. 631,000,000
Kifungu 2015 – *Regional Office Tabora*…………….Sh. 933,000,000
Kifungu 2016 – *Regional Office Tanga*…………….Sh. 1,058,000,000
Kifungu 2017 – *Regional Office Shinyanga*…………Sh. 717,000,000
Kifungu 2018 – *Regional Office Singida*…………....Sh. 696,000,000
Kifungu 2019 – *Regional Office Lindi*………………..Sh. 749,000,000
Kifungu 2020 – *Regional Office Mara*…………......Sh. 655,000,000
Kifungu 2021– *Regional Office Manyara*…………..Sh. 781,000,000
Kifungu 2022 – *Regional Office Kigoma*…………....Sh. 965,000,000
Kifungu 2023 – *Regional Office Pwani*……………..Sh. 954,000,000
Kifungu 2024 – *Regional Office Njombe*…………..Sh. 577,000,000
Kifungu 2025 – *Regional Office Morogoro*……….Sh. 1,078,000,000
Kifungu 2026– *Regional Office Geita*……………….Sh. 825,000,000
Kifungu 2027 – *Regional Office Simiyu*……….…....Sh. 856,000,000
Kifungu 2028 – *Regional Office Katavi*…………......Sh. 531,000,000
Kifungu 2029 – *Regional Office Songwe*………….Sh. 531,000,000
Kifungu 2030 – *Regional Office Ilala*……………......Sh. 387,000,000
Kifungu 2031 – *Regional Office Kinondoni*………..Sh. 407,000,000
Kifungu 2032 – *Regional Office Temeke*……..…...Sh. 583,000,000
Kifungu 2033 – *Regional Office Tarime*…………...Sh. 392,000,000

Kifungu 3001 – *Fraud, Money Laundering and Corruption Offence*……………….Sh. 2,399,240,000
Kifungu 3002 – *Assets Forfeiture Transnational and Specialized Crime*……………..……Shs 2,564,500,000
Kifungu 3003 – *Case Management, Coordination of Criminal Cases*……..……………Sh. 5,709,945,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………….………..Sh. 7,484,512,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……....Sh. 536,954,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…..........................Sh. 411,347,284
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….....................Sh. 268,191,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…Sh. 354,952,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*…………………..…Sh. 1,003,569,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*….Sh. 299,258,000
Kifungu 1008 – *Library Service and Research Unit*…..Sh. 308,869,000
Kifungu 1009 – *Legal Registry Unit*……………...……Sh. 652,292,000
Kifungu 2001 – *Case Management and Quality Assurance*…………..…………………Sh. 1,585,599,200
Kifungu 2002 – *Arbitration Division*……………..……Sh. 2,268,116,238
Kifungu 2003 – *Litigation Division*..............................Sh. 5,577,060,278

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 5,346,774,480
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……….Sh. 801,263,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…........................Sh. 1,032,465,900

Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….....................Sh. 489,953,100
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*....Sh. 262,268,900
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit* .......Sh. 494,936,000
Kifungu 1008 – *Research and Library Service Unit*…..Sh. 209,762,600
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*………………………...Sh. 767,630,000
Kifungu 2001 – *Coordination and Advisory Service*..Sh.3,951,104,310
Kifungu 2003 – *Legislative Drafting*………………….Sh. 8,472,582,240
Kifungu 3002 – *Treaties and Contracts Division*…..Sh. 3,273,098,970
Kifungu 5001 – *Regional Attorney General's Office – Dar es Salaam*...................Sh. 212,374,000
Kifungu 5002 – *Regional Attorney General's Office – Arusha*………………………Sh. 163,874,000
Kifungu 5003 – *Regional Attorney General's Office – Mbeya*…………………………...Sh. 156,802,000
Kifungu 5004 – *Regional Attorney General's Office – Kilimanjaro*…………………….…Sh. 156,705,000
Kifungu 5005 – *Regional Attorney General's Office – Mtwara*……………….….……Sh.161,652,000
Kifungu 5006 – *Regional Attorney General's Office – Mwanza*……………………..…Sh. 163,198,500
Kifungu 5007 – *Regional Attorney General's Office – Kagera*…………………………Sh. 155,832,000
Kifungu 5008 – *Regional Attorney General's Office – Tabora*…………………………Sh. 159,726,000
Kifungu 5009 – *Regional Attorney General's Office – Tanga*…………………….……Sh. 155,283,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………………………Sh. 2,297,184,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……...Sh. 203,200,000
Kifungu 1003 – *Procurement Management Unit*…..Sh. 114,695,000

Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……....................Sh. 124,518,000
Kifungu 1005 – *Recruitment, Appointment and Confirmation Unit*……..…………...Sh. 670,410,000
Kifungu 1006 – *Ethics and Discipline Section*…….....Sh. 1,018,800,000
Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation*……………………………….Sh. 215,930,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*………..……………....Sh. 322,865,000
Kifungu 1009 – *Legal Service Unit*…………………...Sh. 174,100,000
Kifungu 1011 – *Government Communication Unit*.... Sh. 356,950,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………….............Sh. 1,314,506,000
Kifungu 1003 – *Planning Division* …...........................Sh. 450,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kifungu1001–*Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 9,943,517,000
Kifungu 2002– *Civilanization and Prosecutions*…….…Sh. 50,000,000
Kifungu 3001 – *Fraud, Money Laundering and Corruption Offence*..................................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kifungu *1001 – Administration and Human Resources Management*……...............................................Sh. 0
Kifungu *1003 – Planning and Monitoring Division*.............................................Sh. 88,440,500,000
Kifungu *1005 – Information, Communication and Technology Unit*.................................................Sh. 0
Kifungu *1006 –Information, Education and Communication Unit*.....................................................................Sh. 0
Kifungu *1008 – Estates Management Unit*……………...............Sh. 0
Kifungu *1009 – Records Management unit*……….....................….Sh. 0
Kifungu *2001 – High Court Main Registry* ……….........……......Sh. 0
Kifungu *2302 – Case Management Division*……….................Sh. 0
Kifungu *2303 – Complaints Management and Inspectorate*………….......………….…..…Sh. 0
Kifungu *2327 – Judiciary Delivery Unit*……....…..........................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu *1003 – Policy and Planning Division*…........Sh. 4,951,738,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation*……………………..…...Sh.522,058,000
Kifungu 2002 – *Human Rights*………………………………………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, wewe na timu yako pamoja na *AG* na timu yake kwa bajeti yenu

kupita. Sasa nendeni mkatimize wajibu mliotumwa na Serikali na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.32 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 30 Aprili, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*